ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Tisa – Tarehe 04 April, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*): Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kutoa maelezo mafupi ya Kamati ya *PAC*. Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*). Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Wapiganaji wanatakiwa wawe namna hii, kama nahodha hayupo, basi hata sarahangi aingie. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea nataka tukumbuke kwamba baada ya kazi kubwa iliyofanyika wiki iliyopita, kwa kujadili ripoti mbali mbali, tulijipanga kwamba leo hii shughuli zetu zimalizike na bado tuna ripoti nne hazijajadiliwa.

Kwa hivyo, naomba nichukuwe nafasi hii kwanza kuwashukuru wasaidizi wangu, Mhe. Naibu Spika, Wenyeviti wote wawili kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya ya kunisaidia kuendesha kikao hiki, siku ya Ijumaa mzigo ulikuwa mzito kidogo, kiasi cha kwamba wakati mwengine unauondoa kichwani uuweke begani. Ukaona kama hiyo haitoshi ukaurejesha tena kichwani, lakini hatimaye shughuli zimekwenda, nashukuru sana wasaidizi wangu kwa kunisaidia kuendesha kikao, ambapo taarifa niliyoipata kilikuwa kigumu kwa kiasi fulani.

Sasa kuendesha kikao haendeshi Spika, peke yake au yule anayekalia kiti, ni pamoja na nyinyi Waheshimiwa Wajumbe. Waheshimiwa Wajumbe mkikataa kikao kisiende, hivyo hakiendi, mimi ndivyo ninavyo amini hivyo. Mkikataa kwamba kikao kisiende vizuri basi hakiendi vizuri. Kwa hivyo, mimi nguvu yangu iko kwenu katika kuendesha kikao, ndio naamini kabisa hivyo, tena kwa wote mawaziri pamoja na *backbenchers* wengine.

Sasa naomba kwenu munisaidie kuendesha kikao hiki, tuna ripoti nne mbele yetu tuzijadili kwa ufanisi. Mtazamo ni kwamba leo tumalize kazi, ndio

mtazamo wenyewe. Tuliambizana hayo mapema na nikajinata na naamini Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, amejiandaa hivyo kwamba leo tufanyeni kazi, nimekubali na *Accounting Officer* wangu Katibu, nimemwambia leo aandae chakula mara mbili leo. *(Makofi)*

Sasa baada ya maandalizi hayo, mimi naomba munisaidie Waheshimiwa Wajumbe, tuendeshe kikao hiki kimalizike leo. Maana kesho kuna mambo mengine yamepangwa. Labda kama pasipobudi. Sasa hiyo pasipobudi sikutaka tufike huko, lakini tuendelee na kikao vizuri na kwa ufanisi mkubwa kama ilivyo kawaida yetu.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana. Nikiwatazama nyusoni mnaungana na mimi mkono, ili mnisaidie kuendesha kikao hiki. Nakushukuruni sana, sasa tuendelee na kazi.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari

(Majadiliano Yanaendele)

Mhe. Spika: Sioni kumbukumbu hapa mezani za wajumbe waliokwishajitokeza. Isipokuwa nianze kumwita Mhe. Mohammed Said Mohammed. Karibu sana, jitahidi uchangie, upange *point* vizuri na umalize majadiliano haya kwa upande wako kwa dakika 10, nisaidie sana Mheshimiwa Mjumbe.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia katika ripoti hii ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, ambayo imewasilishwa na Mwenyekiti wangu, Mhe. Mama Asha Bakari Makame.

Mimi nianze moja kwa moja kwenye suala la michezo. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba nianze kwenye michezo sehemu ya *ZFA*. Mhe. Spika, *ZFA* ni chombo muhimu, tukiwa katika serikali kuingia kwenye mchakato wa kuomba nafasi ya uanachama katika *FIFA*. Hiki ni chombo chetu, ni chombo cha michezo ambacho sote tunataraji kitatuezeshana kitatupeleka katika *FIFA*, lakini nina wasi wasi mkubwa Mhe. Spika. Wasi wasi wangu hata hiyo *CAF* tuliyokuwepo hivi sasa tunaweza tukafukuzwa.

Mhe. Spika, sasa hivi *ZFA* imekumbana na migogoro mingi sana hata kufikishwa katika Mahakama Kuu ya Zanzibar na chombo hiki hakitakiwi hata

kufikishwa katika Sheria za Mahakama. Mhe. Spika, tukiingia katika *FIFA* tunatarajia kuwe na angalau vipengele kadhaa.

Kwanza viwanja vyetu vinatakiwa viwe bora ambapo vitatusababishia na sisi kuingia katika *FIFA*. Lakini viwanja vyetu vyote viko katika hali mbaya ya kutisha sana kama vile Kiwanja cha Gombani. Kiwanja hiki tuliambiwa hivi karibuni tutapata zile nyasi badia, lakini kile kiwanja ni kibaya mno, kwa sababu hata rangi zake ni mbovu, za kutisha, seuze hizo nyasi bandia ambazo zimekuwa kama uzi zitafika leo, kesho na keshokutwa, tumeanza kupata wasiwasi.

Kiwanja cha Amani, nyasi ambazo zimetiwa pale ni mbovu na zimekosa hata rutuba ya kuweza kujulikana au kuleta ile haiba ya uwanja ambao unatakiwa uwe bora. Mhe. Spika, *tartan* za pale zimekufa kutokana na gwaride ambalo limechezwa pale katika sherehe za Mapinduzi, basi zimekuwa mbovu sana hata ile sehemu ya kukimbilia, kama unakwenda kuzoa basi unaweza hata kupata magunia mawili.

Niingie kwenye Kiwanja cha Mao-Tse-Tung. Mhe. Spika, kiwanja hiki tangu mimi ninacheza mpira kile kiwanja hakibadiliki, kiko vile vile kibovu. Tumetembelea pale tukapewa maelezo ambayo hayawezi kutekelezeka. Sasa tunaiomba serikali na wizara husika kupitia kwako Mhe. Spika, kama kutakuwa kuna *policy* ya kukichukua kile kiwanja basi kichukuwe kiwe chini yake, ili kiwanja kile kitengenezwe na kiwe na matengenezo bora kabisa.

Mhe. Spika, niingie kwenye Hoteli ya Bwawani. Mhe. Spika, hoteli hii ni dhamira nzuri ya muasisi wetu wa Mapinduzi. Kwa kweli ni hoteli ambayo ni bora na mpaka sasa ina jina, lakini sasa imekuwa na uozo mkubwa sana, kuanzia mikataba ya wafanyakazi, vyumba vyenyewe, ukodishwaji holela na kuna maofisi hayajulikani ni ya nini na hata tukipata walemavu tutashindwa kuwaweka. Kwa sababu ile sehemu ya chini yote imekodishwa maofisi, mikataba isiyoeleweka na haijulikani ukizingatia na hivyo vitu vyengine vilivyokuwepo.

Mhe. Spika, kubwa zaidi ukiingia tu katika ule mlango imara wa geti kubwa, pale unalipia Shs. 1,000/= ya kuingilia ndani. Lakini wale sio walinzi na ile risiti yao inasema, hoteli haitohusika na upotevu wowote unaopotea wa chombo chako, hilo moja.

Jambo la pili, tuliishauri kuwa zile pesa zipelekwe wizarani, ili zikaandikiwe risiti na zipelekwe Hazina. Kwa ushahidi mpaka leo zile pesa hazijapelekwa kokote, haziingii kwenye mfuko wowote, hilo linatusikitisha sana.

Mhe. Spika, niingie kwenye Shirika la Utalii, shirika hili ni zuri na serikali ilikuwa na dhamira nzuri sana ya kuunda shirika hili. Lakini sasa hivi shirika hili ni bovu, halina maana na halina ushirikiano wowote. Kuna nyumba ya *Living Stone* ile nyumba ni nzuri sana tunaweza kuweka makumbusho yetu pale yaliyokuwa bora kabisa. Hivi sasa kama ulivyo ushahidi wa wajumbe wote wanavyoona kuwa lile limetupwa kabisa.

Mhe. Spika, kuna Kisiwa cha Nanguji Pemba, kisiwa kizuri, kinaweza kikafanyiwa utalii mzuri. Lakini mpaka sasa hakuna chochote.

Mhe. Spika, Hoteli ya Uwanja wa Amani, vile vile seuze zile hoteli tatu za Pemba. Mhe. Spika, ukenda kutizama kwa ushahidi wako hata wewe mwenyewe, basi utalia ukiona lile shirika linavyodidimia.

Mhe. Spika, kuna Hoteli ya Kilimani *Bar*, hoteli hii iliwekwa pale kwa dhamira ya kujengwa *ZRB*. Lakini dhamira ile iliondoshwa na ikazungushwa uzio tu, shirika walikuwa na upeo mzuri wa kujenga *Diplomatic Club* pale, lakini mpaka sasa hakuna chochote ambacho kinaendelea. Kwa hivyo, tunaomba wizara husika ishirikiane na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia kwako Mhe. Spika, ili kuweza kuiboresha na kuweka katika hali nzuri na bora zaidi ile pale.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije kwenye Chuo cha Utalii. Chuo hiki ni hazina yetu ambapo sasa tunakimbilia kuingia katika mapato makubwa kwenye utalii na kupata wanafunzi au wafanyakazi bora wa nchini kwetu kuingia katika *Private Sector* za Utalii.

Lakini hivi sasa chuo kile ni kibovu mno Mhe. Spika pale alikuwepo mkandarasi alikuwa akijenga na anadai takribani shilingi milioni 24 na bado hajalipwa. Vile vile hakuna kilichojengwa chochote, hoteli inavuja na pale pamejengwa *foundation* tu na wala wanafunzi hawapati mafunzo kwa vitendo kikamilifu, kwa hivyo ile dhamira yote imekwisha.

Mhe. Spika, kwa haya yangu machache na kuheshimu muda wako, basi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Mjumbe, kwa kweli ametuwekea mfano, yaani ni *precedent* nzuri kuifuata kwa hali yetu na mazingira tuliyonayo. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tufuate mfano wa aina hiyo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuchangia Ripoti ya kamati ya Wizara ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza kamati hii ambayo inaongozwa na mama yetu Mhe. Asha Bakari Makame (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari) kwa kweli imefanyakazi kubwa ambayo inastahili pongezi, mbali na matatizo ambayo wameyapata wakati wa ziara zao hasa kwenye nyanja hizo za michezo kama Mhe. Mjumbe mwenzangu alivyotangulia kueleza.

Mhe. Spika, mimi nitaingia kwenye nyanja hiyo ya michezo kwanza nikiwa kama mdau mkubwa ambao ni uwanja wangu wa mambo ya michezo. Kwa kweli suala ambalo amelizungumzia Mhe. Mohammed Said Mohammed ni jambo la kweli, yaani matatizo yapo kwenye Chama cha Michezo, isipokuwa mimi nitazungumzia zaidi wizara husika ya michezo.

Tukiangalia viwanja vyetu vya michezo, yaani viwanja vyetu vya kuchezea mpira wa miguu, ambao ni mchezo unaopendwa ulimwenguni kote na hapa kwetu Zanzibar. Kwa kweli mpira wa miguu Zanzibar umeshuka katika kiwango cha hali ya chini kabisa na imefikia wakati hata watu viwanjani hawendi na Waheshimiwa Wawakilishi hapa ni mashuhuda, kwa sababu wao wanakwenda mpirani kipindi cha Mshindano ya Kombe la Mapinduzi tu na wala hawajui *League* ya Zanzibar na hata mashindano mengine yoyote yanayofanyika hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, sababu kubwa ambayo imewafanya watu pamoja na viongozi wetu wasiende kwenye mashindano ni kutokana na kiwango kibovu ambacho kinaoneshwa katika michezo hii. Kwa kweli sababu hii inatokana na Uongozi wenyewe wa *ZFA* pamoja na viwanja vyetu au miundombinu yetu katika mambo ya michezo.

Mhe. Spika, kipindi cha Mashindano ya Kombe la Mapinduzi kulikuwa na makocha mbali mbali kama vile wakigeni na walizungumza maneno na sisi wengine wachozi yalitutoka, kwa sababu anayekutukana si lazima atumie ile lugha ya matusi, lakini kuna maneno ni matusi moja kwa moja. Kwa hivyo, alizungumza kwamba huu Uwanja wa Amani si uwanja wa kuchezea mpira isipokuwa ni uwanja wa kuchezea mchezo wa ng'ombe, kwa kweli ni kitu cha kusikitisha Mhe. Spika.

Sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Sita chini ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wakati ule Mhe. Ali Juma Shamuhuna pamoja na Katibu Mkuu Dkt. Omar Dadi Shajaki walifanyakazi kubwa, kwa kuweza kupata mfadhili na kuujenga uwanja ule, ambao ilikuwa ni kilio cha Wazanzibari kwamba hatuna uwanja wa kuchezea mpira katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Kwa hivyo, tulibahatika na uwanja ukajengwa kwa gharama kubwa, jumla ya Dola Milioni 9 zilitumika kwa ajili ya kuufanyia ukarabati uwanja ule. Sasa nadhani Mhe. Spika pamoja na Waheshimiwa Wajumbe mtafanya hesabu Dola Milioni 9 ni sawa na shilingi ngapi kwa hivi sasa kwa fedha za Tanzania mbali na serikali kutoa shilingi milioni 100 kwa ajili ya kusaidia shughuli mbali mbali katika kuukarabati uwanja ule.

Lakini Mhe. Spika uwanja ule tokea umalizike bado haujafika mwaka, yaani uwanja ule haujachezewa *League* ya Zanzibar hata mechi moja, isipokuwa umechezewa Mashindano ya Mapinduzi *Cup*, *Africa Cup* pamoja na Kombe la Shirikisho tu. Kwa kweli uwanja hauchezeki na umekuwa kama nilivyosema awali uwanja wa kuchezea Mashindano ya Mchezo wa Ng'ombe. Kutokana na hali hiyo, hili ni jambo la kusikitisha sana, kwa sababu fedha nyingi zimetumika.

Kwa hiyo, naiomba wizara kupitia kwako Mhe. Spika, kwa sababu fedha zilizotumika ni nyingi, yaani kulikuwa kunahitajika matunzo makubwa kuhakikisha uwanja ule unaulea kwa ajili ya wanamichezo wetu katika kuinua kiwango chetu cha mpira hapa Zanzibar. Lakini hali halisi sote tunaiona na tunaifahamu, labda hivi sasa kwa vile kuna mvua hizi za siku mbili tatu ndio utakuta kuna majani kwenye uwanja ule na hali inasikitisha sana.

Mhe. Spika, mbali na Uwanja wa Amani pia Mhe. Mjumbe mwenzangu aliyetangulia alizungumzia uwanja wa Mao-Tse-Tung, ambako ndiko kunakochezwa League yetu hii ya mpito, maana sio *League* hasa. Kwa kweli ukienda Uwanja wa Mao-Tse-Tung utasikitika sana kuona watu wawili ndio wanaoangalia mpira pale, yaani watu hawana hata hamu ya kuangalia mpira kutokana na hali mbaya kabisa katika nyanja yetu hii ya mchezo wa mpira wa miguu na wizara ipo inaangalia tu.

Mhe. Spika, nakumbuka kikao kilichopita niliwahi kumuuliza Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo masuala kama haya ya michezo. Kwa hivyo, alihakikisha kwamba katika kipindi kinachokuja cha kikao basi masuala yale atakuwa tayari ameshayashughulikia, lakini mpaka hivi sasa hakuna lolote ambalo limeshughulikiwa na sijui Mhe. Waziri kwa nini anayamezea mambo haya ya utendaji wa *ZFA*, ambayo ni hali sote tunaifahamu.

Pamoja na hayo katika kuendeleza mpira wa miguu si viwanja viwili hivyo. kwa mfano, zamani tulikuwa tukitumia viwanja vya Mnazimmoja, Maisara na hivi viko katika hali mbaya. Mhe. Spika, lazima wizara pamoja na serikali kama kweli tunataka kuendeleza mpira wa miguu basi ni vyema serikali iwajibike kuhakikisha kwamba inatengeneza viwanja vya michezo vya

Mnazimmoja, ambavyo hivi sasa imekuwa ni bahari, kwa sababu maji ya bahari yanaingia kule na viwanja havichezeki na watoto hawana sehemu ya kuchezea.

Mhe. Spika, Zanzibar tumebahatika kuwa na vipaji. Kwa taarifa yako Mhe. Spika, gazeti la tarehe 01/04/2011 la Zanzibar Leo kwenye ukurasa wa katikati kuna taarifa ya kijana wa Kizanzibari anaitwa Adam Nditi ambaye baba yake alikuwa ni mchezaji wa Kikwajuni Eric Nditi. Kwa hivyo, kijana huyo hivi sasa anachezea Timu ya Chelsea na tayari anao mkataba wa kuchezea Timu ya Chelsea.

Kwa bahati nzuri gazeti hilo linalo na Mhe. Spika ukinipa ruhusu, basi niko tayari kuja kukuonesha, kwa ajili ya kuthibitisha kwamba yule mtoto hivi sasa anachezea Timu ya Chelsea. Kwa kweli ni faraja kubwa tena ni sifa kubwa za Zanzibar, yaani mtoto wa Kizanzibari anachezea Timu ya Chelsea na muda si mrefu tunamuona kwenye Television zetu akichezea *Premier League* ya Uingereza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hii ni kuonesha kwamba Wazanzibari tunavyo vipaji. Kwa kuthibitisha hayo Mhe. Spika, mwaka juzi vijana wa Zanzibar na wewe ndiye uliyewapokea pamoja na Mhe. Waziri husika katika Baraza la Wawakilishi la zamani pale Kikwajuni, Vijana wa Mkoa wa Mjini Magharibi waliweza kuleta Kombe la *Copal Coca Cola* kwa mikoa yote ya Tanzania na wao ndio walikuwa mabingwa na kombe likaja hapa. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwisho aliwaita watoto wale ni watoto wa Brazil, kutokana na kiwango cha mpira walichokuwa wakionesha. Kwa hivyo, hii ina maana kwamba Zanzibar tunavyo vipaji, lakini wale wakuendeleza vile vipaji hatuna na wizara inakaa tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika serikali iliyopita kulikuwa na migongano ya hapa na pale kwamba Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo Mhe. Ali Juma Shamuhuna hivi na vile, lakini hivi sasa Mhe. Ali Juma Shamuhuna hayupo tena na hali imekuwa mbaya zaidi.

Naiomba wizara pamoja na serikali kupitia kwako Mhe. Spika, iweze kuliangalia hilo na kuhakikisha kwamba tunainua vibaji vya mpira wa miguu hapa Zanzibar.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nataka niongezea kidogo kuhusu suala la utalii. Kwa kweli suala hili ndilo ambalo tunalolitagemea hivi sasa katika kunyanyua uchumi wetu za Zanzibar. Kwa hivyo, wizara pamoja na serikali

kwa jumla kuna haja ya kuangalia zaidi kuboresha, kwa sababu tusipoliangalia hili basi hali yetu ya kiuchumi itakuwa ni mbaya. Kwa maana hiyo, lazima wizara ijitahiki kuhakikisha kwamba inafanya ushirikiano mzuri na Kamisheni ya Utalii.

Vile vile naipongeza sana Kamisheni ya Utalii kwa kazi zao nzuri na wanajitahidi chini ya Mkurugenzi Ally Halil Mirza pamoja na uongozi wake wanajitahidi sana kuhakikisha kwamba wanaboresha katika suala hili la Utalii kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba nimalizie kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Wizara hii chini ya Mhe. Haroun Ali Suleiman kwa kweli ni sehemu muhimu sana katika kuendeleza vijana wetu kiuchumi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aweze kufuatilia sana katika ile mikopo ambayo wanapewa wananchi, ili iweze kurudi na kuwafaidisha wengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika ziara zetu za kamati tulitembelea Wilaya ya Micheweni. Kwa kweli maelezo tuliyoyapata kutoka kwa wananchi walisema kwamba, fedha zile ni ruzuku kutoka kwa Rais Abeid Amani Karume kwa kuangalia masikini hawana kitu, kwa hivyo kazi yao ni kula wali na samaki washibe tu basi, *Alhamdullilah.* Kwa hivyo, wao hawajui kuzirejesha fedha zile.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema kuwe na somo maalum la kuwafahamisha wale, ili na wengine waweze kufaidika. Baada ya kusema hayo, nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, mimi nataka nikuahidi kwamba dakika tatu sifiki kwa hivyo nafasi kubwa utaipata kwa dakika zangu.

Mhe. Spika, mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri tu kwenye ziara ya kamati hii tulipata taarifa kwamba kuna mfanyakazi wa Uwanja wa Mao-tse-tung alifukuzwa, labda kwa kudharau kamati au kwa kwenda kinyume na taratibu za kamati. Kwa hivyo, naomba kujua ni kipi ambacho sasa serikali inashindwa kuwajibisha wafanyakazi wengine hasa wale wa *ZFA* kuchukua nidhamu kama hii ambayo imefanywa pale Uwanja wa Mao-tse-tung. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii kuweza kuchangia Kamati hii ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Mhe. Spika, mimi nilikuwa nianzie katika suala la uwezeshaji, hili nataka kushukuru sitochangia hata kidogo. Mhe. Spika, kwa imani yangu ya dhati kwa Mhe. Waziri nina imani kwamba uwezeshaji utakuwa ni mzuri na sina mashaka

nayo, namwambia kwamba Jimbo la Kwahani limejenga matumaini makubwa sana kwake yeye.

Mhe. Spika, mimi zaidi nataka niende katika suala la Wizara ya Habari na Michezo. Mhe. Spika, wenzangu wamezungumzia zaidi katika vile viwanja ambavyo vinaeleweka kuwa ni vikubwa kama kiwanja cha Mao na cha Amani lakini kila jambo lina chanzo chake, hatuwezi kuwapata watu kwenda kucheza Amani kama hatujapata watu wa madaraja ya chini. Mhe. Spika, nilikuwa naiomba taasisi inayohusika iangalie viwanja vya madaraja ya chini, kwani viwanja havina viwango na viwanja hivi viko vyengine vinatumiwa ambavyo haviko katika maeneo yalikuwa mazuri.

Mhe. Spika, daraja la pili Wilaya ya Mjini mechi zinachezwa ndani ya Makao Makuu ya Jeshi, hiki ni kitu ambacho kwa tunapoelekea katika mwelekeo wa FIFA basi ningeliomba taasisi ikaliangalia kwa udhati kabisa. Mhe. Spika, kiwanja kile kinachochezwa Wilaya ya Mjini huwa kuna muda yanapigwa matarumbeta hivyo mechi inabidi zisimame. Lakini ukiachilia hilo kuna vitu ambavyo ukiingia mle uwanjani vinaleta usumbufu kwa waangaliaji wa michezo ile. Mtu akipigwa chenga basi kuna utaratibu maalum wa kushangiria, ukishangiria kwa nguvu unaambiwa ukang'owe majani au unapigishwa kichura.

Kwa hivyo, kwa huko tunakoelekea nchi yetu ambayo ina uhuru, tumejitawala na tunategemea michezo iwe mizuri. Kwa hivyo, naomba katika yale madaraja ya chini tuangalie vizuri ili tujenge viwanja ambavyovilivyokuwa na mwelekeo, viwanja ambavyo washangiriaji wetu watapata uhuru na fursa ya kufanya kama michezo inavyoruhusu.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nataka niende katika suala zima la Kamisheni ya Utalii. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza hili mara nyingi wamekuwa wakipiga kelele katika suala zima la mapato hususan Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Salmini Awadh Salmin, wameshapiga makelele sana kwamba serikali hii pesa zipo isipokuwa kuna matatizo ndio yanayosababisha kuweza kuikosesha serikali mapato. Mhe. Spika, inapokosa serikali mapato tunakosa kufanya kazi kwa ufanisi au kuziwezesha zile taasisi zinazohusika ili zikaweza kujiwezesha. Kwa hivyo, moja ya chanzo ambacho tunakitegemea katika nchi hii, chanzo ambacho kila mtu amekikodolea macho ni suala zima la utalii.

Mhe. Spika, suala la utalii sasa hivi katika serikali yetu imekuwa ni tegemeo lakini katika chanzo hiki kumekuwa kuna ubadhirifu mkubwa, ubadhirifu ambao unaikosesha serikali yetu mapato. Mhe. Spika, naomba wizara inayohusika ijaribu kuandaa mikakati ya kutosha na nimuombe Mhe. Waziri

wa Fedha juzi kwa kumnukuu alisema kwamba anajaribu kuzuia misamaha ya kodi. Kwa hivyo, mimi namuomba sio misamaha ya kodi pia ajaribu kufuatilia vyanzo vya mapato vya kwenye mawizara mengine. Pia kuna haja ya kuandaa timu iliyokuwa nzuri kufuatilia kadhia hii.

Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha kabisa ambalo limetokezea Novemba, 2010 katika Kamisheni ya Utalii, ni kwamba kuna mfanyakazi ameweza kufoji saini ya Mkurugenzi katika *section* ya leseni na miradi ya hoteli. Mhe. Spika, ameweza kufoji leseni hiyo ambayo ilikuwa na *amout* ya dola 7000 na wahusika walikuwa ni Hoteli ya Sea Cliff. Hii ni hatari kweli kweli kama mfanyakazi wa chini anafoji leseni kama amekamatwa na ameweza kutambulikana ni kwamba huyu ni mmoja lakini nina imani kwamba wako wengi wanafanya matendo haya kwani yanafanyika sehemu nyingi.

Mhe. Spika, ni kwamba hili ni suala la kutisha mfanyakazi yupo anaitwa Mohammed Maulid nafahamu kwamba taasisi hiyo imeshaanza kuchukua hatua ndogo ndogo, lakini kuna haja ya Mhe. Waziri wa Fedha kuandaa mikakati kupitia maeneo ambayo tunayategemea akayaangalie. Sio kwa ajili kusamehe kodi lakini pia kuangalia jinsi gani ya ukusanyaji wa mapato ulivyokuwa bora na kuweza kuisaidia serikali yetu ili kuondokana na hii kadhia ambayo kila siku tunapiga kelele kwamba serikali haina pesa. Kwa hivyo, naomba kwa kumalizia jambo hilo mimi nikae nakushukuru sana.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake na kunipa fursa hii ya kusimama hapa nakupongeza Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kidogo ili nisipoteze muda wako.

Mhe. Spika, mimi nitachangia sehemu hii ya uvuvi kwa sababu na mimi ni mvuvi kwa hiyo nitazungumzia habari ya uvuvi. Mhe. Spika, naipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wizara inayohusika kuwapa msaada wavuvi kama vile maboti, nyavu na misaada mengineyo. Mhe. Spika, ni kwamba wavuvi wetu wanapewa misaada na serikali kwa kadri ya uwezo wa serikali, lakini misaada hiyo inakuwa na migogoro mikubwa kwani wale wakubwa hupenda sana kuzuia misaada hii kwa manufaa yao. Kwa mfano, katika kamati yangu tulitembelea sehemu moja ya Mtambwe Kusini walipewa msaada wa boti lakini boti hii ilizuia na ndugu Sheha kwa sababu ya manufaa yake tu.

Mhe. Spika, mambo kama haya ndio yanayoleta migogoro ili wale wadogo wanapopewa misaada wakubwa huizuia kwa manufaa yao. Kwa hivyo, naiomba serikali na wizara husika iwakodolee macho wakubwa wanaozuia

misaada ya wananchi wadogo wakati wanapopewa misaada hii kwa kujiwezesha.

Mhe. Spika, wavuvi Zanzibar ndio uti wa mgongo kwa sababu wavuvi ndio wengi, kwa hivyo serikali wakati inapowawezesha wavuvi, wakubwa wahakikishe kwamba wavuvi hawa wanawezeshwa ili waondokane na umasikini. Pia serikali inawapa misaada hii ili kujiwezesha katika maisha yao.

Mhe. Spika, ningeliiomba serikali na wizara husika ziwaelimisha elimu ya uamini kwani elimu ya uaminifu sisi hatuna. Mhe. Spika, wakati serikali inapotoa misaada kama hiyo kuwapa wadogo uaminifu wa wakubwa sio ile kuisimamia, uaminifu wa wakubwa ni kwamba mali ya wadogo kuzifanya ni mali zao wakubwa. Kwa hivyo, jambo hili litizamwe sana na serikali, wizara husika wakati wanapotoa misaada hii juu ya wananchi ni kuangalia uhakika kwamba wananchi mali zao zinawafikia bila ya kuhangaishwa na waliokuwa wana nguvu.

Mhe. Spika, Zanzibar na Pemba wavuvi wetu ni masikini sana na wanahitaji misaada ili wapate kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa hivyo, naiomba serikali hivi sasa ipo haja sana yakuwapa misaada wavuvi, kutokana na hilo serikali imeshaweka sheria ya kuhifadhi mazingira katika bahari, na wavuvi wetu wengi sasa hivi ndio wanaotumia huo uvuvi wa haramu. Mhe. Spika, mimi naishauri serikali kwamba ifanye mpango inunue meli za uhakika ili wananchi wetu watiwe katika meli za uvuvi.

Mhe. Spika, ili nisipoteze muda wako naiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi ifanye mpango iwanunulie watu wa Matemwe meli ya uvuvi. Kwa sababu watu wa Matemwe ni watu 99 wanatumia bahari kwa hali ya kujitafutia maisha. Kwa hivyo, ikiwa watu wa Matemwe pamoja na Mtambwe nilikotembelea kama watanunuliwa meli ya uvuvi ya uhakika basi ule uvuvi haramu hautotumika.

Mhe. Spika, bila ya kupoteza wakati nawaombea wavuvi wanunulie meli za kuvua ili samaki tupate kusindika katika viwanda. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, ahsante sana asubuhi hii kupata nafasi ndogo ya kuweza kuchangia juu ya kamati hii. Mimi nianze moja kwa moja na Wizara ya Uvuvi na Mifugo, wizara hii imebahatika kupata misaada mingi ya kijamii kwenda kwa wananchi. Kuna mradi huu wa *PADEP* ambao uko sehemu kubwa watu wa shehia nyingi wamechagua ufugaji wa ng'ombe wa kisasa wa maziwa.

Mhe. Spika, kamati za vijijini hazina wataalamu, wataalamu, madaktari na wajuzi wa mambo hayo ya ufugaji wanatoka wizara hii husika. Lakini kwa

bahati mbaya nizungumzie shehia ninayoijua mimi tu, shehia hii ilichukua ng'ombe kutoka Arusha Mhe. Spika, zaidi ya asilimia 50 ya ng'ombe hawa wamekufa. Mhe. Spika, mimi pamoja na kuwa sio mtaalamu walipokuja tu niliona kuwa hawa sio ng'ombe bora, wale waliobahatika kuzaa kwanza ndama wote walikufa na baada ya kutegemea kupata maziwa kama walivyokuwa wakiahidi madaktari wakati wa mafunzo baina ya lita kumi na lita tano watu walikuwa wanapata lita tatu hivyo ni bora ng'ombe wa kienyeji kuliko huyu ambaye anaitwa wa kitaalamu. Mhe. Spika, mara nyengine wanasema ni sababu ya kutoshiba, mimi sababu hii siikubali moja kwa moja lakini wasi wasi wangu kwa wataalamu wa mifugo walipokwenda kununua kwa makusudi walitafuta ng'ombe ambao sio bora.

Mhe. Spika, ningeishauri wizara hii katika miradi yake iwatake wataalamu wake kuwa wakweli, watoe elimu ya kweli na wafanye kazi wakitegemea kuwa wanaowatumikia ni wananchi waliokuwa masikini na lengo la miradi hii ni kuwakwamua watu katika hali ya umasikini na kupata pahala bora kidogo. Mhe. Spika, lengo sio kuwabakisha pale walipo au kurudi chini zaidi kwa sababu ng'ombe hawa wanaotumwa matunzo yake ni magumu na ni mazito. Kwa hivyo, mtu kufanya kazi yote ile na hatimae ikawa hana tija badala ya kumuendeleza huwa unamvunja moyo. Kwa hivyo, ningeiomba wizara iwe makini kwa miradi hii ya kijamii.

Mhe. Spika, sasa nije katika Wizara ya Habari na Utalii katika sehemu ya utalii. Mhe. Spika, ni kwamba utalii hivi sasa ni moja katika njia yetu kuu ya kimapato, lakini tutazame pande zote mbili faida na hasara ipi itachukua nafasi kubwa zaidi katika shughuli hii. Mhe. Spika, ni kwamba utalii unaingiza fedha katika serikali lakini namna tunavyowaachia watalii wetu wa nje wanavyokwenda pia wanatubomolea maadili ya nchi yetu na hatimae tunasema kuwa maadili yameporomoka, lakini chanzo ni sisi serikali kuwa hatuna udhibiti maalum wa kuweza kuwadhibiti wageni wanaoingia kwenda na utamaduni, silka, mila na tabia za Mzanzibari.

Mhe. Spika, kwa kuwa haya hayazingatiwi hivi sasa mambo mawili haya faida na hasara yanakwenda sambamba na hatimae hasara zitakuwa kubwa zaidi kuliko faida tuliyoipata kutokana na mfumo huu tunaokwenda nao hivi sasa. Mhe. Spika, iko siku hasara yake itakujakuwa kubwa zaidi kuliko faida yake.

Mhe. Spika, sasa nije katika vyombo vya habari vya serikali mimi nataka niseme kuwa vyombo vyetu vya serikali ndio mdogo wa serikali. Mhe. Spika, kwa hivyo kuna haja ya makusudi wizara hii kuviboresha ili viweze kufanya kazi kubwa na nzuri zaidi ili vipambane na utitiri wa vyombo vya habari vya binafsi vilivyoingia hapa Zanzibar. Mhe. Spika, Televisheni ya Zanzibar na Sauti ya Tanzania ya Zanzibar lazima ziimarishwe ziwe bora zaidi kuliko

vyombo vyengine vyote vya habari vilivyopo, vyenginevyo hivi vya binafsi vikija vikichukua hatua kubwa zaidi watendaji wetu tuliokuwa nao hatimae watatutoka. Kwa hivyo, ningeomba wizara hii iandae mazingira ya makusudi ya kuwaendeleza waandishi wetu na wana habari wetu kufikia kiwango cha juu zaidi kuliko walivyo hivi sasa kwa kuwapatia mafunzo ya ndani na nje na vyombo vya kisasa vya habari.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba nimalizie hapo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii fupi pamoja na kuwa nina mengi ya kuzungumza kuhusu kuchangia ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati naomba kwenda haraka haraka kama iwezekanavyo. Kwanza Mhe. Spika, narejea tena ili jengo la Kilimani Bar, hili jengo kwa taarifa tulizonazo ni kuwa hivi sasa madirisha yanatolewa na kuwa Shirika la Utalii liliomba jengo hili ili wajenge holi la kimataifa ambalo naamini kama kazi hiyo ingeliwezekana hivyo serikali ingalifaidika pakubwa. Kwa hivyo, mimi nilitaka kujua kwa nini Shirika hili la Utalii hawakukabidhiwa jengo lile na hivi sasa linaendelea katika hali lilivyo.

Mhe. Spika, hili Shirika la Utalii katika uchunguzi wangu linawafanyakazi ambao elimu yao ni ndogo na umri wao ni mkubwa sana hivi sasa na shirika kwa maana ya shirika ni lazima libadilike. Kwa hivyo, ningeliomba ushauri wa Mhe. Waziri juu ya kuimarisha shirika hili kitaaluma. Mhe. Spika, Shirika hili la Utalii kwa bahati mbaya halina usafiri kwa hivyo ningeliomba nipewe maelezo litafanya kazi vipi kama halikuimarishwa.

Mhe. Spika, jambo jengine nizungumze kwa jumla juu ya mahoteli yetu ya serikali ninayoyajua mimi ni manne. Kuna Hoteli ya Bwawani, Wete, Chake-Chake pamoja na Mkoani. Mhe. Spika, sakata la Hoteli ya Bwawani ningelisisitiza tena kama ilivyoeleza ripoti kuwa ipo haja hii kamati husika iende tena ili ikafanye kazi kwa kupata taarifa ya kuisaidia serikali. Mimi ningelisema iundwe tume lakini utaalamu wa juzi naona ni bora iende kamati.

Mhe. Spika, kuna hoteli zetu za Pemba tatu, moja iko Wete, nyengine Chake-Chake na nyengine Mkoani, hii ya Wete na Mkoani ziko katika hali mbaya wala hatujui linaloendelea na ile ya Chake-Chake naona imegeuzwa Benki ya Barclays hivyo basi ningeliomba nipate maelezo.

Mhe. Spika, kwenye uvuvi nina mengi ya kuzungumza lakini kwa sababu ya wakati nizungumze kidogo kuhusu uhamasishwaji wa wananchi katika ufugaji wa samaki. Mhe. Spika, ufugaji wa samaki ni kazi ngumu inayotumia nguvu

nyingi sana na wananchi wengi ni lazima wajikusanye kwa pamoja kwa kutumia nguvu zao kuweza kukamilisha shughuli hiyo. Kwa bahati mbaya nimetembelea katika vikundi viwili vya ufugaji wa samaki nimeangalia mazingira, nimeiona kazi ngumu ya wananchi iliyotumika katika kuweka yale mabao.

Mhe. Spika, jambo ambalo nimelisoma kule ni kuwa vile vikundi vinatafuta site tu halafu wanaanza kazi yao bila ya kushauriana na taasisi husika kama mazingira na kadhalika. Kwa hivyo, nahofia upoteaji wa nguvu ule dakika za mwisho watu wa mazingira wakaja wakaamua vyenginevyo wakasema hapa hapafai. Kwa hivyo, ushauri wangu mimi ni kwamba ufugaji wa samaki uimarishwe, lakini wakati ule ule hatua za awali zichukuliwe ili mradi ukiendelea usiwe na matatizo ya baadae.

Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati sasa naomba niingie kwenye mifugo. Mhe. Spika, tuna mradi huu mkubwa wa kuzalisha mifugo yetu kwa kutumia sindano, tuna mradi mkubwa wa kuwaimarisha wafugaji kwenda kuchukua ng'ombe Tanzania Bara. Mhe. Spika, juzi Mhe. Waziri katika kujibu swali kuwa vile vikundi vinavyokwenda kuchukua ng'ombe kule Bara ili kuja kuzalisha huku ni kuwa vikundi vile vinafuatana na wataalamu wa kilimo. Mhe. Spika, wanapofika kule mtaalamu huwa hana kauli yoyote, kwa hivyo ni vikundi ambavyo hawana taaluma ya mifugo ndio wanaojichagulia mbegu wanazotaka na kuzileta huku na matokeo yake kwa sababu nimefanya uchunguzi kuona kuwa hakuna tija wale ng'ombe wengi wanakufa na wengine huwa hawana sifa zinazohitajika japo kuwa kimaumbile utaona hivyo. Kwa hivyo, ili tuendelee na fedha nyingi inayotumika naomba unipe muda kidogo kutoa mawazo yangu kuhusu hili.

Mhe. Spika, ufugaji huu tunaofanya kwa nia safi kabisa ya kuongeza tija kwa wananchi, kinyama, maziwa na kipato ni ufugaji wa kuunganisha mbegu kutoka Zanzibar na mbegu kutoka nchi nyengine. Mhe. Spika, kimaumbile dunia hii Mwenyezi Mungu alipoumba hivi viumbe kulikuwa na wengine hawana sifa za kuweza kuishi walikuwa wanapotea njiani na wale wanaobakia wa asili ni wale Mwenyezi Mungu aliowajaalia kuwa na sifa hizo.

Kwa hivyo, unapochukua mbegu kutoka nje ukaja ukachanganyisha na mbegu ya hapa kwa kupata sifa ambazo za hapa hawana, na kuzikiwa sifa ambazo zinahitajika kwa wale tulionao ili tupate kizazi ambacho kitakuwa na sifa za yale mahitaji tunayohitajia na ya kuishi, hivyo kuna mambo mengi ni lazima tuyachunguze kwa makini. Mhe. Spika, unapofanya *cross breeding* unachanganyisha mambo, nusu ya mbegu inayotoka nje na nusu ni mbegu tuliyonayo ya asili hapa tukitarajia kupata mbegu bora. Pia tutarajie kupata mbegu mbaya kwa sababu hiki kizazi kinachozaliwa hapa petu kikichukua sifa

za kile kinachotoka kule nje ambazo sifa zake za kule hapa hatuwezi ku-*invest*, pamoja na kuwa tuna tamaa kuwa atapata sifa za hapa basi wakati wote utaona kuwa kile kizazi hakiendelei, hii mara nyingi huwa ni hasara.

Mhe. Spika, nimetembelea katika ufugaji Mtambwe wale walikuwa na ng'ombe sita wamekufa mmoja mmoja mpaka wanabakia wawili na juhudi kubwa wanayoichukua. Mhe. Spika, tumekwenda katika ufugaji mwengine wa walemavu hapa Nyamazi wale alhamdulillahi wanaendelea vizuri, lakini bahati mbaya ng'ombe wale ambao walikuwa watoe maziwa mengi basi wanatoa lita mbili tu. Kwa hivyo, kuna mambo ni ya kitaaluma ni lazima tuyachunguze, kabla hatujaamua tunafuata mbegu ipi. Wenzetu katika nchi zilizoendelea mwanzo walipoanzisha mambo haya walikuwa wakipata hasara sana. Sasa hivi wanachukua uchunguzi wa hali ya juu na kujua matokeo na kuona kuwa kweli yakitoka matokeo hapana hasara. Ndio tukaona wenzetu wameendelea.

Namshauri Mhe. Waziri wataalamu wake wafanye utafiti wa hali ya juu, juu ya ile mbegu inayoingia nchi mwetu, kwa matatizo yeyote kwa *genetically* na *physical* itaweza kumudu kuendelea au laa. Tusichukue sifa tu, tukazichanganyisha wakati kimazingira huwa hazifai.

Juzi tulikuwa tuna Mswada wa Uhakiki wa Chakula na Lishe. Tunajua athari ya lishe yeyote ikipungua katika kiwiliwili inaleta athari yake. Wanayama wetu nao hawa vile vile wanahitaji sawa sawa na sisi. Wafugaji wetu wakishakupata ng'ombe maana yake ni kuwa kuna chakula maalum wakitumie ili waweze kukua na kupata mahitaji tuliyonayo.

Wafugaji leo hawana mfuko katika ushirika wao. Matokeo yake wanawalisha ng'ombe wao ambao walikuwa wapate chakula cha kutengenezwa maalum na cha kuchanganyisha cha majani. Wanachukua majani yetu haya haya tuliyonayo na hivi sasa wanasema mtichoo unaondoa matatizo yote.

Ukitizama ng'ombe wetu hawatoi maziwa yanayohitajika. Ng'ombe wetu hawatoi nyama kama inayohitajika na hawapati maisha kama yanayohitajika. Kwa hili ni lazima tuhakikishe kuwa tunajitahidi kufanya jambo ambalo tutawasaidia wakulima wetu, ile tija iliyokusudiwa iweze kupatikana.
Mwisho kuna jambo nililikutia katika Ushirika wa Walemavu. Daktari anayehusika na upandishaji wa ng'ombe, amekwenda mara tatu kwa ng'ombe huyo huyo mmoja, lakini hakufanikiwa ng'ombe yule kushika mimba mpaka ikabidi watafute madume ya kienyeji.

Ushauri wangu ni lazima mbegu tunayoitumia tuone kuwa ni mbegu inayoweza ku- *survive*, vyenginevyo tutakuja kuona kuwa tunafanya kazi kubwa, tunapoteza pesa nyingi na tija haipatikani.

Mwisho kwa hili ningemuuliza Mhe. Waziri mradi ukifanikiwa ndio sawa sawa. Lakini kama haukufanikiwa wana mpango wowote wa ku- *retain* hizi mbegu zetu za asili. Kwa hayo machache Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, namshukuru *Allah* kwa kutuweka hai, wazima na tukapata fursa ya kuzungumza asubuhi ya leo.

Mhe. Spika, kwanza naipongeza Kamati hii ya Uvuvi na Ushirikishwaji Umma kwa shughuli yao na kazi yao waliyoifanya. Mimi nina baadhi ya mambo kama manne (4) ambayo ni changamoto kubwa katika hizi wizara. Nataka kupata ufafanuzi kidogo wakati Waheshimiwa Mawaziri watakapokuja kutuelezea.

Kwanza katika Idara ya Mifugo na Uvuvi visiwa vyetu kuna asilimia kubwa ya wavuvi. Waliekewa mipaka kwa sababu ya kuimarisha hifadhi ya bahari ya ndani, ambayo kiwango kikubwa ilikuwa imetetereka sana kutokana na uvuvi uliokuwa sio wa mpangilio na ulioharibu mazingira. Ni mradi mzuri, mafanikio yake tunayaona na muda kila tukenda tutapata zaidi mafanikio yake.

Mhe. Spika, wananchi wetu ni masikini na wengi wanatumia vigarawa na vidau kwenda kuvulia. Wakiambiwa bahari ya karibu wasivue na nyavu zinakuwa hazipati kitu, basi mambo mawili yatatokea ama watakufa masikini au watafanya uvuvi uliokuwa hautakiwi.

Mimi namuuliza Mhe. Waziri ni utaratibu gani ambao ameuwandaa ili kuwatayarisha hawa wavuvi walioathirika katika ukanda huu wa hifadhi kwenda kuvua katika bahari kuu, ili yote mawili yasitokee. Wapate chakula chao cha kila siku pengine na ziada lakini pia waweze kulinda mazingira ambayo ni hifadhi kwa kizazi chetu kijacho.

Kuhusu Idara ya Mifugo kuna changamoto mbili kubwa. Wengi waliozungumza katika mambo ya mifugo. walizungumza hii mifugo ya *zero grazing* ambayo bila shaka ndiyo inayopewa uzito, kutokana na tija yake na mafanikio yake.

Mhe. Spika, kuna changamoto ambayo inajitokeza sasa hivi. Kama tulivyosema ardhi ni ndogo kwa Zanzibar na kila siku inavamiwa kwa ujenzi. Na huko machamba vile vile kuna matatizo ya kinyang'anyiro cha ardhi baina ya wakulima na wafugaji. Sasa sijui wizara kutokana na changamoto hiyo imejiandaa vipi kwa sababu sera yetu iliyopita juzi, ile sheria pamoja na sera yake zote tulisema uhakika wa chakula na lishe. Ina maana tunahitaji kupata

muhogo, ndizi, wali, lakini vile vile tunahitaji kupata na kitoweo kwa sababu ya lishe. Ili kuweka sawa baina ya wakulima na wafugaji, sijui Wizara kwa upande wake imejiandaa vipi ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo.

Mhe. Spika, vile vile katika mambo ya ufugaji imezungumzwa hapa kwamba kuna uwagiziaji wa ng'ombe kutoka Tanzania Bara hasa Arusha kwa kuja kutokana na miradi iliyoingia. Kuna mambo mawili mimi namuomba Mhe. Waziri atuelezee kidogo. Kwanza ile karantini ya sehemu ya kisiwa cha Pemba imefikia katika kiwango gani matayarisho yake. Kwa sababu pengine ng'ombe wengi hawa wanaoambiwa wanakufa sio kwa sababu ya matunzo lakini pengine hawakupata ile karantini inayotakiwa. Kwa hivyo wameingiwa na maradhi na pengine wanaweza wakayasambaza. Sasa kwa sababu Pemba haijapata eneo la karantini la uhakika, namuomba Mhe. Waziri atueleze.

Mhe. Spika, kwa miaka mitano iliyopita nikiwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi tulikuwa tunapiga kelele sana na mpaka tukafanikiwa kwa kununuliwa mtambo wa kutengenezea *nitrogen* katika Idara ya Mifugo. Jambo lililonistaajabisha kwamba hata mwaka huu bado tunasikia kwamba ndio kwanza panatayarishwa pa kuwekwa wakati mashine ile au mtambo ule umeshanunuliwa. Mhe. Waziri hebu aje atueleze ni lini mtambo ule unatarajiwa kutumika?

Kwa sababu mtambo umeshanunuliwa na pengine mitambo hii ina muda wake wa kutumika. Inaponunuliwa kama haitumiki unaweza ukaona kwamba labda itakuwa ndio salama pengine ndio hasara yake. Ikiwa kama mwaka huu ndio kwanza tunautafutia pa kuuweka halafu ndio uje utumike. Kwa kweli tutakuja kuingia hasara kubwa. Kwa sababu sisi wenyewe katika Kamati tumechukua miaka mitano kupiga kelele na kufanya hivi mpaka zikapatikana pesa za MDRI ndio zikanunuliwa ule mtambo. Naomba tuelezwe vipi mtambo huu lini utatumika?

Kwa Wizara ya Mhe. Harouna mimi naomba jambo moja tu. Hii wizara ni mpya sio kwa wananchi tu, hata sisi wawakilishi. Hatujawahi kusikia wizara kama hii. Mimi namuomba Mhe. Waziri amejiandaa vipi na kutoa taaluma ya kuweza kwanza kuwafahamisha wananchi. Kwa sababu mimi kama ni uwezeshaji na mimi nimo katika kutaka kuwezeshwa. Sasa je, Mhe. Harouna yupo tayari kuniwezesha. Atupe taaluma uwezeshaji wake ni wa aina gani na vipi na watu watarajie mipango gani?

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii na Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako mimi natachangia wizara moja tu nayo ni Wizara ya Habari. Moja kwa moja naanza na Hoteli ya Bwawani. Hoteli ya Bwawani hali yake ni mbaya sana, jengo lile lote vyumba sita tu ndivyo vilivyofanyiwa matengenezo. Kama tunavyojua kwamba hoteli ile ndio hoteli pekee ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wananchi pamoja na sisi viongozi tunaitegemea hoteli ile. Mimi naomba hapa Serikali ifanye yote lakini jengo hili au hoteli hii ifanyiwe matengenezo kwa haraka.

Mhe. Spika, kwenye hoteli hiyo hiyo nizungumzie suala la wafanyakazi. Wapo ambao wamedumu kwa miaka 13 na wengine wapo kwa muda wa miaka tisa. Wote hao wana mikataba ya muda mfupi. Miezi miwili mengine mpaka sita, ndio mkataba ambao wanafanya kazi wafanyakazi hao. Suala hili kila siku tunalalamikia juu ya wawekezaji kuajiri watu kwa muda mdogo sana na badala yake kuwakatisha mkataba.

Sasa sisi kama serikali sijui tunawafunza nini wawekezaji binafsi katika suala hili. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja kufafanua atueleze vipi malengo ya serikali katika hili. Tunamuomba mikataba ya kudumu iwepo kwani vijana wetu au watu wetu wanategemea kupata ajira ya kudumu ili waweze kukidhi hali ngumu ya maisha.

Mhe. Spika, hapo hapo hoteli ya Bwawani kumekuwa na migogoro mingi juu ya suala la ukodishwaji baadhi ya kumbi za starehe na mambo mengine. Mfano wa hayo mahakamani kuna kesi Nam. 7 ya mwaka 2009. Hii inamgogoro baina ya hoteli ile na wawekezaji hao kutokana na kukatishwa mkataba. Inawezekana ikapelekea hasara kubwa kwa serikali ikiwa hoteli hii itashindwa katika kesi hii.

Jengine Mhe. Spika, siku zote Baraza la Wawakilishi haliwezi kubishana sana na serikali isipokuwa tu kuwe na shaka. Shaka inapojitokeza mara nyingi tunakuwa wakali na inafika pahala tutake sasa iundwe Kamati ya kuchunguzwa. Si kitu cha rahisi tu kwamba Wawakilishi wakae waamke huko waje hapa leo waseme tunataka iundwe kamati ichunguzwe si kweli. Lakini inakuwa kuna shaka ya msingi. Inapojitokeza shaka ya msingi kwetu sisi Wawakilishi basi tunakuwa tunahoji na tunakuwa wakali katika suala hili.

Hili nalisema katika ukumbi mwengine wa Hoteli ya Bwawani katika mwaka wa 2010. Kampuni tatu ziliomba kufunga Mkataba katika moja ya kumbi zake Hoteli ya Bwawani. *Star Times* wao walitaka kwa shilingi milioni 34, Zenji FM wao walifika milioni 24 lakini *National Marketing* kwa milioni 15. Lakushangaza mimi mpaka sasa nina mashaka na nafikiri wajumbe wenzangu

na wao watakuwa na mashaka na hili. Mtu wa mwisho kabisa ambaye alitoa tenda ndogo milioni 15 yeye ndiye aliyepewa ukumbi kukodi.

Mashaka yetu sisi, siku zote serikali huwa inataka faida, hata mimi nataka faida na mwengine yeyote huwa anataka faida. Sijui Mhe. Waziri atatwambia zipi kwamba mkataba wa mwisho wa bei ndogo kwamba ndio waliokubaliwa wafunge nao mkataba wa ukumbi huu. Kwa hivyo hapa tunashaka ya msingi ambayo inatupa sababu yakusema na kuiuliza serikali.

Mhe. Spika, nimalizie mwisho kabisa katika wizara hiyo hiyo. Katika habari huku na nitawagusa wenzetu wa TVZ. Mara kama tatu mimi mwenyewe binafsi, tumeshuhudia TVZ ikirusha picha za ngono wakati wa usiku. Jambo ambalo wananchi wetu wanalilalamikia sana hili. Sasa Mhe. Waziri hii Wizara yetu ya Utamaduni ina maana ya kuupotosha huu utamaduni wetu au ndio kuuhifadhi huu utamaduni.

Mhe. Spika, baada hayo naomba nikae kitako.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji katika ripoti hii ya Mifugo. Kwanza naomba niipongeze sana Kamati hii ambayo inaongozwa na dada angu Mhe. Asha Bakari na Makamo Mwenyekiti wake Mhe. Mohammed Said wa Jimbo la Mpendae na wanakamati wengine.

Mhe. Spika, ni Kamati moja ambayo inaonekana ina wataalamu sana katika shughuli zao. Wanaisaidia sana wizara yangu katika shughuli zao. Wizara yangu inaahidi sana kushirikiana nao katika kuona usimamizi wao katika wizara yangu unakuwa na ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Spika, katika ripoti hii ya Kamati Mhe. Mwenyekiti alitoa maoni mengi, ushauri mkubwa ambao wizara yangu naahidi utaufanyia kazi sana. ili kuona malengo ya wizara yetu yanapata msukumo mkubwa. Ila katika maelezo yake naomba kusaidia mambo mawili.

Kwanza ni suala la hati miliki. Ni kweli mashamba yetu mengi ya mifugo mpaka hivi sasa hayajakuwa na hati miliki. Wizara yangu inalitambua hilo na tayari tumeanza jitihada za kuwasiliana na taasisi husika. Hata Mhe. Waziri hapa tayari tumeshazungumza hilo Mhe. Ali Juma Shamhuna. Ili kuona mashamba yetu yote ya mifugo yamekuwa na hati miliki. Kwa hivyo *observation* yake na ya kamati ni hakika na naahidi kwamba tutaifanyia kazi.

Eneo jengine naomba nilizungumze ni suala la ufugaji wa samaki. Katika hili pia namjibu Mhe. Salim Abdallah Hamadi wa Mtambwe. Mhe. Spika, ni kweli

suala hili wananchi wengi wanaonekana kuhamasika na ufugaji wa samaki. Ni eneo muhimu la kiuchumi ambalo wananchi wetu wanaweza kufaidika sana. Lakini bahati mbaya ni suala jipya katika uhalisia wake.

Wananchi wengi wameanza shughuli hizi na namna ambazo wanafanya kama ambavyo Kamati imeona ni kwa kubahatisha zaidi. Sisi Wizara tumeliona hilo na tumeliandalia mikakati. Moja ambalo tumeona tulifanye kwanza ni kulifanyia *feasibility study* suala zima la ufugaji wa samaki. Tayari wizara imeshawasiliana na washirika wa maendeleo kadhaa, tuliwasiliana na Serikali ya Norway, tumeona kwamba imeonesha uwezo wa kutusaidia. Imetuahidi katika hilo. Lakini pia tumezungumza na Shirika la FAO la Umoja wa Kitaifa. Nao wametujibu vizuri. Tumezungumza pia na wenzetu wa China wao wanauzoefu mkubwa katika hili. Na wao wametuahidi.

Mhe. Spika, suala hili ni suala muhimu. Utekelezaji wake unapaswa kufanywa mazingira ya nchi yetu yatazingatiwa. Tusipofanya hivyo huko mbele tutakuja kupata matatizo makubwa. Kupitia Baraza lako tukufu nawaomba wananchi wawe na subira katika suala hili. Wizara inataka kulifanya suala hili lakini katika kuangalia mazingira ya nchi yetu yatahifadhiwa zaidi.

Mbali na Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mhe. Abdi Mosi Kombo wa Matemwe. Kwanza kwa namna ambavyo yupo karibu sana na wizara yangu. Kwa kweli Mhe. Abdi ni miongoni mwa wawakiishi ambao wanakuwa na link kubwa baina ya vikundi vyake vya uvuvi na wizara. Mara nyingi tunawasiliana yakitokezea matatizo na tunajaribu kwa pamoja kuona namna gani tutayashughulikia. Tunampongeza sana Mheshimiwa.

Mhe. Spika, naomba kwanza tukubaliane kitu kimoja. Vikundi vya uvuvi vilivyokuwepo majimboni hivi moja kwa moja havipo chini ya Wiazara yangu. Hivi ni vikundi vipo kwenye mamlaka yao zaidi. Ni vikundi ambavyo vimeibuliwa na shehia na kupata baraka kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mikoa.

Kwa hiyo hivi viko zaidi kwao Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuliko kuwa chini ya Wizara yangu. Ombi langu kwao ni kwamba tushirikiane katika kuvilea tukiiwachie Wizara peke yake kwamba ndio walezi wa vikundi hivi. Sisi kama wataalamu, tupo tayari kutoa utaalamu ambao utahakikisha kwamba vikundi hivi vinaendelea. Lakini ulezi na ufatiliaji wa karibu itabidi tushirikiane baina ya Wawakilishi na wizara yangu ili kuona yale ambayo yamaibuliwa na vikundi vyenyewe yanapata ufanisi kwa maslahi yao na kwa maslahi ya nchi kwa jumla

Ombi la Mheshimiwa Mwakilishi kwamba wizara yetu inunue meli kwa ajili ya wavuvi wa Matemwe, tumelipokea na tutalifanyia kazi. Ni kweli kwamba uvuvi unaofanywa hivi sasa katika maeneo ya maji madogo umepitwa na wakati na tija yake ni ndogo.

Serikali wito wa wawakilishi kwamba sasa tuingie katika maji makubwa ni wito muhimu. Tumeanza kuufanyia kazi, lakini haijawa katika ngazi ya kusema hali iko hivi. Naomba watupe muda kidogo, ni suala ambalo tumeliona na tunalifanyia kazi na ikifika wakati wa kutoa ripoti Barazani Mhe. Spika, Baraza tutaliarifu rasmi ili wananchi wa Zanzibar waelewe hasa mikakati ambayo imepangwa ya kwenda katika maji makubwa.

Mhe. Mohammed Haji wa Matambile alikuwa na suala la ufugaji, kwamba wataalamu wa Wizara yetu walipokuwa wakienda kununua mifugo wameonekana kwamba wamefanya hiyana kidogo.

Mhe. Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Mwakilishi asilichukulie kama hivyo ambavyo analo. Kama nilivyozungumza masuala ya uvuvi na vikundi vya mifugo navyo ni vile vile. Vikundi vyote hivi viliibuliwa katika ngazi ya shehia kwa malengo yao. Sisi wizara tulichokifanya ni kuwasaidia kuwapa pesa katika *account* zao. Wao wafugaji katika vikundi vyao au wawakilishi wafugaji mara nyengine sio mara zote walikuwa wakija wizara kwetu au katika afisi zetu za Mifugo ya Wilaya wakachukua wataalam kwenda wakanunua ng'ombe, ama Arusha au Tanga au kwengineko.

Imetokea si mara moja wala si mara mbili, ushauri wa wataalamu wetu katika ununuzi wa mifugo hii ulikuwa haukubaliwi na vikundi vyenyewe. Kubwa ambalo mtaalamu wetu alikuwa ana hakikisha kuona mifugo ambayo inaingizwa ni ile ambayo haina maradhi. Yamefanyika mambo ambayo yameleta matatizo hasa katika uzalishaji wa mifugo.

Katika suala la kufa hili limechangiwa zaidi ama na matunzo hafifu au lishe. Mimi mwenyewe Mhe. Spika, nimeshawahi kutembelea vikundi vya ushirika nikaona mifugo imewekwa katika mazingira mabovu sana. Sasa hili usitegemee kama ng'ombe umchukue kutoka Arusha, halafu uje umuweke katika mazingira hatarishi kwa kweli ni lazima atapata matatizo, atapata minyoo, atapata maradhi na hatimae muda mfupi atakuwa amekufa.

Hili ni jambo la kuliangalia sana na nawaomba sana wafugaji wanapotekeleza shughuli zao za ufugaji basi wafuate maabizo na ushauri wa wataalamu kwa mifugo. Ushauri wa mwakilishi kwamba wizara iwe makini zaidi na hili. Tumelichukua na tutalifanyia kazi.

Suala kama hilo naliomba alichukue Mhe. Abdalla wa Mtambwe katika suala la mifugo. Katika suala la ufugaji wa samaki jibu la Mwenyekiti kwa suala la *feasibility study* pia alichukue hilo.

Mhe. Rashid Seif suala lake la kwenda katika bahari kubwa jibu ambalo nimemjibu Mhe. Mosi wa Matemwe, linamuhusu pia. Lakini kuhusu suala la karantini ya Pemba ikoje. Kwanza tuliangalia eneo la Wesha, lakini Wesha tulipata kikwazo kutokana na kwamba ni eneo ambalo linamafuta kwa hiyo sasa tumehamia eneo moja linaitwa Nziwengi. Tulipo ni kwamba eneo hili linamilikiwa na Wizara ya Ardhi. Wizara yangu inashauriana tayari na Wizara ya Ardhi kuhusu kulipata hili eneo. Tayari tupo hatua nzuri kwa hiyo si muda mfupi eneo la Kisiwa cha Pemba kitapata eneo la karantini rasmi.

Suala la mtambo wa *liquid nitrogen* Mhe. Spika, umenunuliwa tayari upo. Zilitumika karibu shilingi milioni 600 zimetumika. Mtambo tayari umefungwa na unafanya kazi. Hivi sasa Zanzibar hatununui tena *liquid nitrogen* kutoka Tanzania Bara. Tunayo ya kutosha. Wizara yangu imeanza pia kuwapatia watu wa Wizara ya Afya kwa ajili ya shughuli zao. Na taasisi yoyote ya serikali ndani ya Zanzibar na hata nje ya Zanzibar itayohitaji *liquid nitrogen*, tunayo nyingi wakati wowote ipo. Wanaruhusiwa kuja Idara ya Mifugo kwa ajili ya kuja kununua *liquid*.

Mhe. Spika, nakushukuru na narudia kusema kwamba naishukuru sana kamati imenisaidia sana kutekeleza shughuli za Wizara yangu, natarajia kwamba tutaendelea kushirikiana kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kusimama hapa nikiwa katika hali ya uzima, vile vile niishukuru Kamati chini ya ungozi wa Mhe. Asha Bakari Makame kwa kweli imefanya kazi nzuri na kubwa, niseme tu kwa kiasi kikubwa imenisaidia sana ningeomba wajumbe wenzangu pamoja na Mawaziri wenzangu wazione kamati hizi ni kama ni moja katika kutuongoza au kutuonyesha njia, kwa sababu sisi ni wachezaji inakuwa sio rahisi kuona kila kitu. Lakini yule ambae yuko nje yeye anakuwa na uwezo mkubwa wa kuona jinsi gani tunavyocheza kama ni vizuri au vibaya yeye atakuelekeza, kwa hivyo tusione kamati hizi kwamba ni moja ya njia ya fitna au vipi hapana, ukweli zinatusaidia sana na mimi kamati hii imenipa nguvu za kufanya maamuzi.

Lakini vile vile niwashukuru wajumbe wote ambao wamechangia na haasa wale walioigusa Wizara yangu nao vile vile nawapongeza kwa sababu wameonyesha hisia zao, wao ni wawakilishi na wamechaguliwa na wananchi

na wanatetea wananchi. Lakini vile vile niseme mimi kama ni serikali nafanya kazi kwa ajili ya watu kwa sababu hii ni serikali ya watu imechaguliwa na watu na kwa ajili ya watu, kwa hivyo tuko sambamba. Kila unaloliona ni wajibu tuelekekezane na tuongozane.

Labda nianze tu kwa yale ambayo yamenigusa na suala la kwanza ilikuwa ni suala la mgogoro wa *ZFA* ni kweli kwamba kulikuwa na mgogoro lakini kwa hivi sasa mgogoro huo haupo. Ningependa kuwafahamisha wajumbe tu kwamba sisi kama serikali inakuwa hatuingilii mambo ya michezo moja kwa moja kwa sababu hiyo ni moja katika masharti ya *FIFA* ni kwamba serikali isiingilie masuala ya michezo, michezo isiingizwe katika siasa. Lakini pamoja na hivyo tunahusika kwa njia moja au nyengine kwa sababu pamoja na kwamba *ZFA* ni chombo ambacho kinajitegemea lakini vile vile kipo chini ya serikali.

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe waelewe kwamba hivi sasa hakuna mgogoro. Ulikuwepo ni mgogoro ambao niliurithi na chochote ambacho unakirithi bila shaka inakuwa wewe ni jukumu lako ukiendeleze. Maana hata kama ulikikuta kwa baba yako lakini vile vile uangalie kwa sababu sio kwamba kila unachokikuta kwa baba yako kinaweza kikawa kizuri au kibaya unakiangalia. Mahusiano yalikuwa sio mazuri baina ya serikali na chombo hiki lazima niseme ukweli, lakini tulipokuja sisi tukaona hapana kwa nini tuvutane na ndio maana michezo ilidhorota kwa sababu mahusiano baina ya Serikali na *ZFA* hayakuwa mazuri, kwa hivyo tulichokifanya ni kuungana nao nijue kuna tatizo gani sasa tatizo ni mahusiano tu.

Mhe. Spika, nashukuru kwamba tumekaa pamoja na hivi sasa tumetatua kila kitu kulikuwa na kesi na kesi imefutwa haipo, hivi sasa *ZFA*_imeshafanya maandalizi ya kila kitu na mwisho wa mwezi huu watafanya uchaguzi wao mkuu ili kuhakikisha kwamba atunakwenda salama kabisa, lazima nitoe fisa kwamba *ZFA* imefanya kazi kubwa kwa sababu wao walijaribu kutafuta wafadhili ambao tunasikia *Zanzibar Feet Sentury* ambao ndio wameidhamini timu yetu ya taifa, na wao wakatushirikisha sisi serikali kwa hivyo ni taasisi tatu ni *ZFA, Zanzibar Feed Sentury na* Wizara ya Elimu, tunashukuru kwamba tumefika pahala tumefanikisha mpaka kutayarisha dina ambayo Mhe. Rais ndio alikuwa mgeni wa heshima na imetupatia sifa kubwa.

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano nae amekubali kuwa mgeni wa heshima katika dina kwa ajili ya kukusanya fedha hizo kwa ajili ya kuendeleza timu yetu ya Zanzibar Heros, kiufupi ni kwamba waheshimiwa wajumbe kwa hivi sasa hakuna mgogoro baina ya *ZFA na* Serikali kupo shuwari kabisa.

Lakini vile vile wajumbe waligusia kuhusiana na kiwanja cha Mao-tse-Tung ni kwamba hakiko hali nzuri hilo nakiri, lakini tuelewe tu kwamba moja katika masharti ya *FIFA* ilikuwa ni kwamba nchi yoyote ambayo inataka kujiunga *FIFA* lazima kile chama cha mpira kwanza kiwe na kiwanje chake mwenyewe, hilo ndilo lililofanywa Wizara imewapa kiwanja kile cha Ma-tse-tung tukawapa *ZFA* na Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman anaelewa hilo kwa hivyo ilikuwa ni lazima kiwanja cha Mao-tse-tung wapewe *ZFA* na wamepewa.

Mhe. Spika, *ZFA* ndio iliyotusababisha mpaka tukawa hivi sasa tunatarajiwa kuwa wanachama wa *FIFA* na ndio iliyotutoa changamoto mpaka tukawa na bendera ya Zanzibar, kwa sababu *FIFA* hairuhusu mtu kama hana bendera ya nchi lakini chini ya Maalim Harouna Ali Suleiman suala hilo likafanyika ikabidi Zanzibar sasa iende katika uanachama wa *FIFA* masharti yake ni lazima *ZFA* iwe na kiwanja halafu lazima nchi iwe na bendera,. Suala hilo limefanikishwa nashukuru kwa hivyo waheshimiwa Wajumbe naomba mujenge imani kwa *ZFA* chini yauongozi wangu tunakwenda vizuri na ishaalla mambo yatakuwa mazuri vile vile.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri una dakika tatu tu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo: Vile vile kuhusiana na suala la Bwawani nalo limegusiwa vile vile kweli kulikuwa na matatizo lakini nawahakikishia waheshimiwa wajumbe kwamba matatizo hayo hivi sasa tumeshayatatua na tumefanya mabadiliko pale ili kuhakikisha kwamba ile mikataba ya zamani tunaiangalia iko kiasi gani tukiona ni mizuri basi tutaendelea nayo. Lakini vile vile kulikuwa na suala la mkataba wa Disko ambao umetamkwa na Mhe. Mosi pale kwamba kuna mtu mmoja ambae alitoa dhabuni kubwa lakini hakupewa kapewa mtu mwengine, labda nieleweshe tu kwamba katika kutoa dhabuni kuna vigezo vyake walikuwa watu wanne kwa ufupi, kuna *Zanzibar National Marketing*, *Zanzibar Promotion* na zabuni ile ina vigezo vyake kwanza uwezo, halafu uzoefu na kiwango cha ile dhabuni yenyewe.

Kwanza anaangaliwa yule mtu anayetaka kuchukua ana uwezo gani, ana uzoefu gani halafu kiwango chake ni kweli aliyejitokeza mmoja alikuwa ni *Zanzibar Promotion* ambae alitoa dhabuni ya Shs. 35.000,000/= lakini kwa sababu hana uzoefu wowote yeye ni mwizi tu, sasa yule tuliyempa kwa Shs. 15,000,000/= yeye ana uzoefu wa miaka kumi halafu ana uwezo wa kuendesha baa na mziki ndio maana akapewa yeye na sio kwamba kapewa moja kwa moja tumempa muda wa kumuangalia, tukiona kwamba anakwenda sivyo basi tunabadilisha maamuzi na kumpa mtu mwengine kama atashindwa kufuata masharti yetu na masuala ya ajira sasa hivi tumeshayarekebisha, tumejaribu kuchukua majina ya watu wote ambao hawajaajiriwa tumeshapeleka utumishi

na wao baada ya wiki mbili hizo taratibu zitakuwa zimeshakamilika watakuwa wameshaajiriwa. Kwa hivyo suala la Bwawani naomba mlisahau limeshamalizwa na liko shuwari kabisa msiwe na wasi wasi.

Mhe. Spika, kuhusiana na suala la kilimani Bar hii haiku mikononi mwenu Wizara ya Fedha ndio waliochukua, kwa hivyo nafikiri atakuja kujibu Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi.

Kuhusu Kamisheni ya Utalii, utalii tuelewe kweli kwamba ni uti wa mgongo kwa hivi sasa na lazima tuutuze, lakini kama nilivyosema awali kwamba utalii wenyewe wanasema ni kama upanga wenye ncha mbili na wenye makali sehemu zote zote, kwa hivyo tutafaidika lakini wakati huo huo utaathirika. Kwa hivyo kikubwa ni kuangalia namna gani tunadhibiti ile *the second age* ili isitukate kuangalia utamaduni wetu, mila zetu na nilisema awali kwamba madhumuni ya kuweka mahoteli nje kabisa ya mji kwa sababu tulijua hayo kwamba tukiweka mjini zaidi kuna athari kubwa, ingawaje sio za kutokana na ile kasi kubwa ya mahoteli, ma- *tower* kwa kweli imetuzidi kwa sasa lazima tukubali.

Lakini tumo katika juhudi za kutafuta njia namna gani ya kudhibiti ili maadili yetu yasimong'onyeke, tumo katika juhudi hiyo waheshimiwa wajumbe naomba muniamini kwa sababu kiasi cha miezi mitatu tu au minne, kwa hivyo naomba angalau munipe miezi sita na naamini kwamba baada ya miezi sita basi mtaona mabadiliko.

Waheshimiwa wajumbe vile vile Chuo cha Utalii hivi sasa tunakiboresha na kama mnavyoelewa kwamba kipo pale kwa ajili ya kuwafunza watu wetu ili baadae waweze kufanya kazi katika mahoteli, kwa sababu kuna malalamiko kwamba wafanyakazi wengi sasa hivi ni kutoka nje nia na lengo ni kuelimisha vijana wetu ili baada ya muda waweze kufanya kazi katika mahoteli, sio jengine kwa sababu lazima tukubali kwamba mpaka sasa watu wetu wengi hawana taaluma hiyo lakini nashukuru hivi sasa vijana wengi wamejitokeza na baada ya miaka mitano nitahakikisha kwamba Wazanzibari wengi watakuwa wameajiriwa katika mahoteli haya.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni ubadhirifu wa mapato kwa kweli tumekaa na tumesema kwa vyoyote lazima tufanye mapitio ya mikataba yote ya mahoteli yote, hili siwezi kulifanya peke yangu lazima nishirikiane na Wizara ya Fedha kwa sababu yeye ndio mkusanji wa mapato hayo, kwa hivyo tutakaa ili tuone ile mianya yote ambayo inasababisha fedha kupotea. Mhe. Waziri wa fedha amenisikia na nimeshamueleza jambo suala hilo.

Suala jengine ilikuwa ni TVZ iboreshwe huo ujumbe nimeupokea na tumo katika hatua hiyo ya kuboresha TVZ vipindi vyetu na vifaa tayari nashukuru , lazima tukubali haya yanasababishwa na vifaa, halafu masuala ya picha za ngono hilo nalo tutalipiga vita na kuhakikisha kwamba hakuna picha za ngono ambazo zinaonyeshwa katika TVZ.

Mhe. Spika, suala la hoteli ya Bwawani tumesema kwamba ili kuiboresha kuwa katika hali nzuri hivi sasa tayari tumeshakaribisha muwekezaji ambae tutakuwa na ubia nae ili kuiboresha ile hotali.

Mhe. Spika, kwa sababu ya kuokoa muda mimi nifikie hapo natumai wajumbe wamenifahamu na naomba munipe subra, yote mliyoyataka tutayapata baada ya muda mfupi ujao. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi ya leo kunijaalia kupata nafasi hii ya kutoa ufafanuzi nap engine kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru sana mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Asha Bakari, mimi nikiwa mjumbe wa kamati hiyo vile vile tunaipongeza kamati yetu imefanya kazi nzuri na imetupa mwanga wa kuona huko tunakokwenda.

Mhe. Spika, Mhe. Rashid Seif amenipa suala moja ambalo ni muhimu sana na ningelilianza na hilo hofu yangu nikimpa tafsiri ya Wizara yangu nijiandae kuja kujibu masuala mengi sasa, lakini nitaitafsiri hii wizara ili aweze kuifahamu vizuri, kwa sababu ni kweli bado haijafahamika katika jamii yetu. Hii ni Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika, tunaposema kazi ni suala zima linalohisiana na mambo ya ajira na kazi nyengine ambazo zinafanyika katika sekta za serikali au katika sekta binafsi. Ni eneo ambalo limekuwa na migogoro hasa katika sekta binafsi kwa wafanyakazi wetu, ni vyema na Mhe. Rais ametumia busara kubwa na hekma akaianzisha wizara hii ili sasa ianze kushughulikia masuala haya matatu makubwa, kimsingi ni mawili kwa sababu ukitizama uwezashaji na vyama vya ushirika vinakwenda pamoja, suala la kazi na masuala ya uwezeshaji.

Suala la uwezeshaji ukiona tafsiri hasa ya *MKUZA* ni mpango wa kupunguza umasikini Zanzibar, katika hali ya kawaida ukitizama uchumi wetu kitakwimu tunapata taarifa za uhakika kwamba uchumi wetu unakua na sasa hivi kama sikosei nafikiri uko kwenye asilimia saba na kidogo. Lakini mwananchi wa kawaida hayaoni yale kwa sababu akiangalia kilichokuwepo pale nyumbani au mfukoni mwake hakioni ni sahihi, sasa tunapoambiwa uchumi unakua

mwananchi wa kawaida yeye haoni kwamba uchumi unakua kwa sababu anaona yeye bado ni masikini chakula chake cha kupanga kwa wakati.

Kwa hivyo Rais kaanzisha wizara hii ya uanzishaji wa wananchi kiuchumi kwamba sasa tuelekeze nguvu zetu katika kuwaimarisha na kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi watokane na huo umasikini tuliokuwa nao kwa muda mrefu, wizara imejipanga vizuri katika suala hilo si rahisi ukasema katika kipindi cha miaka mitano kila mwananchi tutamuwezesha katika kiwango kikubwa, lakini imani yetu tuliyokuwa nayo kwa mashirikiano ambayo tutayapata kwa nyinyi waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu masuala haya yanakuguseni kwa asilimia mia moja. Ndio maana pale niliposema tukianza ziara za kutembelea kwenye majimbo kwenye Wilaya na Mikoa ni vizuri sote tukashiriki kwa sababu tutaelewa zaidi matatizo ambayo yanawakabili wananchi na wewe kama ni kiongozi wa pale katika eneo lile utakuwa unaelewa kile ambacho kinahitajika kwa wananchi wako.

Lengo ni kuwaondoa katika hali ya umasikini na kuwapandisha angalau wafike pahali ambapo wajisikie kidogo kwamba sasa alhamdulillahi mambo yetu ni mazuri, lakini pia kwenye vyama vya ushirika tulikuwa na vyama vingi lakini kwa bahati mbaya vimekufa, vyengine vinachechemea lakini viko vyengine vinafanya vizuri sana. Tumeambiwa hapa kuna kile chama cha ushirika cha Limbani pale, Pujini kuna ushirika mzuri tu una wanachama kama ishirini na mbili na maeneo mengine.

Kwa hivyo, tunahitaji kuviimarisha na kuviwezesha vyama hivi ili viweze kufanya kazi, tatizo nililokuwa nalo kwamba Wizara hii ni mpya mpaka Julai, ndio nategemea nitapata bajeti yangu na ishaalla kwa Uwezo wa Mwenyezi Mungu ambao atatujaali na moyo aliokuwa nao Waziri wetu wa Fedha Mhe. Rais mwenyewe ameshaonesha nia ya kutaka kusaidia wananchi wetu, sasa waziri wa Fedha kazi yake ni kuhakikisha tu kwamba bajeti inayopatikana katika wizara hii kwenye suala zima la kuwezesha wananchi basi inatosheleza mahitaji. Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba Mhe. Waziri wa fedha kwa mimi hana matatizo sana.

Lakini naomba nitoe wito hapa niipongeze Wizara ya Katiba na Utawala Bora , niipongeze Wizara ya Elimu tayari wameanzisha ushirika ndani ya wizara zao nilipata bahati ya kufungua mkutano mkuu katika Wizara ya Elimu , nilipata bahati Mhe. Waziri alinialika nakushukuru na ukipata bahati nialike tu kwanda kufungua Mkutano Mkuu wa Wizara ya Katiba na Utawala Bora ina wanachama wengi na inatia moyo kwamba sasa hivi mpaka Benki zimeanza kuwaamini. Sasa naomba na Wizara nyengine zote zianzishe utaratibu wa kuwaambia wanachama wao waanzishe *SACCOS* hizi na Wizara yangu itahakikisha kwamba inawawezesha kwa kuwapatia mbinu na mikopo ili

waweze kujitosheleza kwa mahitaji yao ya kila siku, imani yangu ni kwamba watafanya hivyo.

Mhe. Spika, masuala yaliyozungumzwa kwa haraka haraka ni masuala ya mikataba, mikataba ina matatizo kwa wafanyakazi hasa kwenye mahoteli na maeneo mengine ya sekta binafsi mikataba mifupi mifupi inawapa kero sana vijana wetu na wananchi wetu wanaokwenda kuajiriwa pale, sasa tunataka tuwe na mikataba ya uhakika ambayo itakuwa inawapa haki na fursa wale vijana wetu na wafanyakazi wetu wanaokwenda kuajiriwa katika maeneo hayo. Imani yangu sekta binafsi watashirikiana na sisi katika hili na nashukuru sana kwamba umeonekana moyo mkubwa sana na kunaonekana wazi kwamba sasa hivi sekta binafsi wamejua sasa pana pahala pa kwenda kueleza matatizo yao na sasa tukasaidia matatizo hayo, mikataba itaangaliwa upya nashukuru sana hilo kamati imeliona na naipongeza sana na kweli ni eneo moja ambalo lina matatizo.

Lakini pia katika sekta hizo hasa kwenye mahoteli baadhi ya hoteli na baadhi ya wafanyakazi waliopewa majukumu katika hotali hizo hawaelewi au pengine hawatambui au kwa kufanya makusudi, nasikitika sana kwa tukio ambalo limetokea kwa kamati hii inayoongozwa na Mhe. Asha Bakari ilipokwenda kwenye hoteli ya *LAGEMA* Meneja wa pale au msaidizi wa Meneja au mhusika wa siku ile hakuwapa mashirikiano mazuri, kama Waziri Abdilahi Jihad alivyosema ameanza kuchukua hatua na sisi tulichukua hatua siku ya pili yake tulipopata habati tulimsimamisha yule Meneja aliyefanya mambo yale.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba ni mgeni hatusemi kwamba mgeni asipewe haki na fursa lakini pia ilikuwa aheshimu utaratibu wetu ambao serikali tumejipangia, hizi kamati zinakwenda kwa lengo la kutusaidia mambo sisi wananchi wetu ili kuweza kupata faida kubwa na maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, niongeze kidogo kwa sababu ni wizara mpya hii.

Sasa napenda nizungumzie masuala ya *AK* na *JK* mifuko hii imeanzishwa ni kweli ina matatizo bado haijawafikia walengwa bado kuna bilioni 2.2 ziko Benki hazijatoka, sasa si vyema pesa zile zikaendelea kukaa benki nimesema na nitaendelea kulifuatilia, suala hili kuhakikisha kwamba pesa hizo tunazipata na ikiwezekana basi zisimame moja kwa moja pamoja na wizara yenyewe kwa kusaidiwa na benki yenyewe.

Kuna mapendekezo yametolewa kwamba Wizara ya Vijana iwe chini ya Wizara yetu, kuna mapendekezo yametolewa kwamba mifuko iwe chini ya mamlaka ya Wizara. Hili suala la kwamba vijana wawe chini ya Wizara yetu Mhe. Makamo wa Rais anasikia lakini mimi siwezi kuliingilia hilo kwa sababu haya maamuzi yako nje ya uwezo wangu, ishaalla wataliona linapofaa. Lakini suala la vijana linahitaji kuangaliwa kwa umakini kwa sababu kama kuna eneo ambalo linataka kuwezeshwa kwa kiwango kikubwa ni suala la vijana.

Mwisho Mhe. Spika, kwa vile umenambia nikatishe suala la semina kwa wajumbe ili kuwaelimisha zaidi wao wajumbe, ishaalla katika kipindi kinachokuja cha bajeti niliahidi na leo natoa tamko kwamba tayari tumeshazungumza na *ILO* na wako tayari kutufanyia semina angalau ya siku mbili ili kuwapata taaluma waheshimiwa wajumbe hawa, ili baadae waende kwa wananchi wao wakawape taaluma zaidi ili waweze kujikusanya na kuweza kuwawezesha.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. (Mhe. Asha Bakari Makame) Mhe. Mwenyekiti nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uamuzi ambao wa kutuundia wizara nyengine mbili Mifugo na Uvuvi, pia na Wizara ya Uwezeshaji ameona kwamba kuna umuhimu katika wizara hizi ambazo zitamsaidia mwananchi wa taifa hili.

Lakini pia Mhe. Spika, nadhani nisichukue muda kutokana na wakati nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuwashukuru wajumbe wote wa Baraza lako tukufu waliochangia, nikianza na.

1) Mhe. Said Moh'd
2) Mhe. Nassor Salim Ali
3) Mhe. Hija Hassan Hija
4) Mhe. Ali Salim
5) Mhe. Abdi Mosi Kombo
6) Mhe. Moh'd Haji
7) Mhe. Salim Abdalla Hamad
8) Mhe. Rashid Seif Suleiman
9) Mhe. Ussi Jecha simai.

Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba maoni na mapendekezo ambayo yametolewa na waheshimiwa na kwasababu mawaziri husika amejibu hoja zote takriban, kwa hivyo natoa imani kwa kamati yangu kwamba kipindi

kitakachokuja chengine haya yote yaliyotolewa hoja katika Baraza lako tukufu tutasimamia na kuhakikisha yanatekelezwa ipasavyo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa wale wanaokubali mikono juu, wanaokataa, hakuna aliyekataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Ripoti inapokelewa rasmi na Baraza na iko tayari sasa kufanyiwa kazi na serikali kwa yote yale yaliyomo ndani ya ripoti hiyo, nakushukuruni waheshimiwa wajumbe wote pamoja na .

RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO NA UJENZI

Mhe. Spika: Waheshimwa Wajumbe, kabla ya Mwenyekiti hajaendelea, mwenyekiti huyo ana uzoefu mkubwa anaweza kuwasilisha kitu kwa masaa mawili, anaweza kufanya hivyo kwa muda mfupi na leo kwa sababu ya mazingira yetu naamini atatumia ufundi wa kuwasilisha ripoti kwa muda mfupi.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi (Mhe. Makame Mshimba Mbarouk): Mhe. Spika, kamati yangu ya Mawasiliano na Ujenzi majukumu yake yametajwa katika Kanuni ya 109 kama ifuatavyo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

b) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji bajeti na hotuba nyengine za waziri alizotoa Barazani.

c) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kitaifa na miradi ya wananchi juu ya wizara husika.

d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya serikali kwa wizara husika na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kushughulikia jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

f) Kufikiria Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

g) Kuchambua ahadi zote za wizara zilizo chini ya kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ilianza shughuli zake za kufuatilia utekelezaji wa Kazi za Maendeleo za wizara zifuatazo:

- Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
- Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki nne kwa utaratibu ufuatao:

i) Pemba kuanzi tarehe 20/12/2010 hadi tarehe 31/12/2010

ii) Unguja kuanzia tarehe 28/02/2011 hadi tarehe 11/03/2011

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao amabyo yamewezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:

1.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Rashid Seif Suleiman	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Shawana Bukheit Hassan	-	Mjumbe
4.	Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Mjumbe
5.	Mhe. Subeit Khamis Faki	-	Mjumbe
6.	Mhe. Salum Amour Mtondoo	-	Mjumbe
7.	Mhe. Hassan Hamad Omar	-	Mjumbe
8.	Ndg. Mussa Kombo Bakari	-	Katibu
9.	Ndg. Aziza Wazir Kheir	-	Katibu

Mhe. Spika, kamati ilifanya kazi zake kwa utaratibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya wizara pamoja na taasisi zake na baadae kutembelea na kukagua utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na taasisi hizo.

WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI

Mhe. Spika, kamati yetu ilitembelea taasisi mbali mbali zilizo chini ya wizara hii na kukagua miradi mbali mbali inayotekelezwa na taasisi hizo zilizo chini ya wizara. Baada ya kutembelea na kuona utekelezaji wa shughuli mbali mbali

za wizara pamoja na taasisi zake, kamati ilitoa maelekezo, maoni na ushauri kwa wizara na taasisi zake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli hizo.

Mhe. Spika, muhtasari huu umebainisha baadhi ya mambo ambayo kamati yetu inaainisha kuwa ni muhimu sana kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Mambo hayo ni kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

Mhe. Spika, kutokana na kuwepo kwa matumizi ya ardhi yasiyozingatia mipango mizuri ya ardhi kwa kila shughuli, kamati yetu inaelekeza kuwa idara zinazohusika na ramani, upimaji na mipango miji na vijiji kwa kushirikiana na taasisi nyengine, kuhakikisha kuwa Ramani za Miji zenye kubainisha maeneo ya Kilimo, Makaazi, Viwanda na Mahoteli zinafanyiwa mapitio kwa wakati na kufuatwa kikamilifu ili kuwa na sura nzuri ya miji yetu. Kamati inasisitiza kuwa baada ya ramani hizo kufanyiwa mapitio, zigawanywe katika ngazi mbali mbali zinazohusika katika masuala ya uidhinishaji wa matumizi ya ardhi zikiwemo halmashauri za miji, kwa lengo la kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

Mhe. Spika, nchi yetu imekumbwa na migogoro mingi ya ardhi iliyosababisha mlundikano mkubwa wa kesi za ardhi. Migogoro hii inatokana na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa uadilifu kwa baadhi ya watendaji wa idara zinazohusika na masuala ya ardhi. Kwa msingi huo, kamati yetu inazishauri idara zinazoshughulikia masuala ya ardhi kufanya kazi kwa kuzingatia maadili na sheria zilizopo ili kupunguza migogoro ya ardhi inayowasilishwa katika Mahakama ya Ardhi.

Miongoni mwa maeneo ambayo Kamati yetu inasisitiza Idara hizo kuyafanyia kazi na kutatua matatizo yaliyopo kwa kuwapa haki zao wale wote wanaostahili ni pamoja na maeneo ya Vitongoji, Pemba na Pwani Mchangani, Matemwe, Kijichi na Mbweni kwa upande wa Unguja. Kwa upande wa suala la eneo la Pwani Mchangani, kamati ilitoa msisitizo katika eneo hilo kuwa utaratibu wa kufuata ni ule uliotolewa na tume iliyoundwa na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini na kutoa ripoti yenye uhakika ya wamiliki wa maeneo hayo yaliyolalamikiwa katika eneo la Pwani Mchangani. Aidha, kamati inasisitiza kuwa huo ndio utaratibu wa kufuata ili kuepusha matatizo mengine kutokea.

Mhe. Spika, hapa tumpongeze sana Mhe. Waziri wetu Mhe. Ali Juma Shamuhuna kwa kuchukua jitihada kushirikiana na kamati na kuweza kulitatua suala hili na wananchi kuweza kujisikia sasa hivi wakati wowote kuwa wanaweza kupewa mali yao.

Mhe. Spika, kamati yetu ilibaini kuwepo kwa kesi nyingi za masuala ya ardhi zilizofunguliwa Unguja na Pemba ambazo zinasikilizwa na Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi kwa upande wa Unguja na Naibu wake kwa upande wa Pemba. Kamati inakubaliana na kilio cha Mahkama hiyo kuwa kesi hizo zote kusikilizwa na watu wawili pekee ni mzigo mkubwa na hivyo kuchelewesha utoaji wa haki kwa wananchi. Kwa kuwa sheria inaruhusu kuwepo kwa Mahakimu wa Mikoa wa Mahkama hizo za Ardhi, kamati inaiomba wizara husika kuharakisha taratibu zitakazoweka mazingira mazuri yatakayowezesha kuteuliwa kwa Mahakimu wa Mikoa wa Mahkama hiyo ambao watasaidia katika kuondoa mrundikano wa kesi zinazohusiana na mambo ya ardhi.

Mhe. Spika, aidha kamati hii inazitaka idara husika kuwa sheria inayotoa ukomo wa haki ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya makaazi na matumizi mengine inafuatwa katika utoaji wa haki ya matumizi ya maeneo hayo kutotoa viwanja zaidi ya vile vilivyoruhusiwa kwa mujibu wa sheria. Jambo hili linasisitizwa na kamati yetu kutokana na kuwepo kwa hofu miongoni mwa wananchi kuwa baadhi ya watu wanapewa haki ya matumizi ya ardhi katika maeneo mengi, wakati wananchi walio wengi wanakosa haki hiyo.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo kamati yetu inahisi kuwa ni muhimu ni suala la maji. Hii ni changamoto kubwa inayoikabili Mamlaka ya Maji, wizara na serikali kwa ujumla kutokana na upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Unguja na Pemba kutokua na uhakika wa kupatikana. Suala hili la maji limekuwa likileta usumbufu mkubwa kwa wananchi kwa kuhangaika na kutumia muda mrefu katika kutafuta huduma hii muhimu.

Kamati imeguswa zaidi na tatizo la maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi, ambapo tayari fedha nyingi zilishatumika katika mradi uliotegemewa kuondosha tatizo la maji katika maeneo hayo. Kamati ilijulishwa kuwa miongoni mwa mambo yanayosababisha tatizo la maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi hata baada ya mradi wa maji kukamilika ni kuwepo kwa mitandao ya mabomba ya maji yaliyochakaa na hivyo kuvujisha maji mengi. Pia kamati ilijulishwa kuwa tatizo la maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na maeneo mengine linatokana na kuungua kwa pampu zilizopo katika visima vya maji.

Kamati inaelekeza mamlaka kuhakikisha inamaliza changamoto ya upatikanaji wa maji Mkoa wa Mjini Magharibi hasa baada ya mradi wa maji kumalizika na zaidi mamlaka iwe na Mpango Mkakati wenye kutekelezeka haraka iwezekenavyo, utakaomaliza kabisa tatizo hilo katika Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na maeneo yote ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, pia kamati yetu imeguswa na suala la uchakavu wa baadhi ya Nyumba za Maendeleo zilizojengwa na serikali, uchakavu huo unaweza

kuhatarisha afya na usalama wa wananchi wanaozitumia nyumba hizo. Hivyo, kamati inaelekeza kufanywa kwa ukaguzi wa nyumba za maendeleo ikiwa ni pamoja na Nyumba za Maendeleo, Kengeja; ili kuona kama nyumba hizo zinaweza kukalika na pia kufanya tathmini ya gharama za matengenezo na kuzitengeneza nyumba hizo.

Wakati kamati yetu inatembelea baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, iliguswa sana na hali ya ufinyu wa nafasi kwa taasisi hizo kutekeleza majukumu yake, usafiri kwa ajili ya taasisi hizo pamoja na kutokuwepo kwa wafanyakazi wa kutosha watakaowezesha majukumu ya taasisi hizo kutekelezeka kwa ufanisi. Kamati inashauri wizara kuzifanyia kazi changamoto hizo haraka iwezekanavyo ili kuleta ufanisi kwa taasisi hizo katika kuwahudumia wananchi.

Mhe. Spika, kwa upande wa Shirika la umeme Zanzibar, (*ZECO*) Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi imesikitishwa sana na deni ambalo shirika hilo linadaiwa na Shirika la Umeme la Tanzania (*TANESCO*) linalofikia kiasi ya Shilingi Bilioni 40, deni ambalo limetokana na *TANESCO* kuipandishia umeme *ZECO* kwa asilimia 168 ukilinganisha na asilimia 21 ambayo *TANESCO* imewapandishia watumiaji wengine huko Tanzania Bara.

Kamati imesikitishwa na kitendo cha *TANESCO* kupandisha umeme kwa kiwango cha juu sana kiasi hicho kwa Shirika la Umeme la Zanzibar kuliko ilivyopandisha kwa wateja wadogo waliopo Tanzania Bara. Zaidi, kamati haikufurahishwa na kitendo cha *TANESCO* kukaidi kupunguza ongezeko hilo hata baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kutoa agizo kwa *TANESCO* kushusha kiwango hicho kwa Shirika la Umeme Zanzibar.

Kamati inashauri kuwepo kwa jopo maalum litakalowahusisha watendaji wa shirika pamoja na taasisi nyengine zitakazoweza kusaidia, kwa lengo la kukutana na uongozi wa Wizara ya Nishati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na *TANESCO*. Hata hivyo, kamati inasisitiza kuwa shirika lijiandae kwa kuwa na nyaraka za kutosha (*working paper*) kwa ajili ya kujenga hoja madhubuti wakati wa kikao hicho. Kamati kwa upande wake, iko tayari kusaidia katika kutoa msukumo ili kumaliza tatizo hili, kwa kukutana na uongozi wa Wizara ya Nishati ya Muungano.

Mhe. Spika, katika kulipa uwezo Shirika la Umeme ili liweze kutoa huduma kwa ufanisi, kuna haja kubwa kwa Taasisi za Serikali kulipia gharama za umeme wanazotumia. Taasisi hizo za serikali zimekuwa hazilipi madeni yake kwa Shirika la Umeme ambapo hadi sasa taasisi hizo zinadaiwa kiasi cha shilingi bilioni nne, mbali ya deni ambalo shirika linazidai taasisi binafsi na watumiaji wengine wa huduma hiyo. Kamati yetu inaishauri serikali na taasisi

zake kujitahidi kulimaliza deni hilo ili shirika liweze kujiendesha kibiashara na kutoa huduma zake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu masuala ya nishati, kamati yetu inaishauri Idara ya Nishati inayohusika na masuala ya nishati na serikali kwa ujumla kuchukua hatua za ziada na kuharakisha suala la uchimbaji wa mafuta ili Zanzibar iweze kuchimba mafuta yatakayosaidia kukuza uchumi wa nchi hasa baada ya Baraza hili kuridhia Zanzibar kuanza uchimbaji wa mafuta.

WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Mhe. Spika, kwa upande wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kamati yetu pia ilipata maelezo na kutembelea idara na taasisi mbali mbali zilizo chini ya Wizara hii. Kamati imeainisha baadhi ya mambo muhimu kama yanavyofafanuliwa katika muhtasari huu hapa chini.

Mhe. Spika, Zanzibar ni visiwa vinavyotegemea sana usafiri wa bahari, kamati ilitembelea Shirika la Meli na kubaini kuwa mpango wa shirika wa kuuza meli za serikali ambazo zimechakaa na kununua meli mpya hadi sasa umekwama kutokana na kutonunua meli yoyote mpya, baada ya zile za zamani kuuzwa. Hali hii inapelekea kudhoofika kwa hali ya shirika kutokana na kutegemea meli mbili pekee na huduma za uwakala kama vyanzo vya mapato, ambapo meli hizo pia zinaelekea kuharibika kabisa na hivyo kuhatarisha mustakabali wa shirika.

Mhe. Spika, kamati yetu ilijulishwa kuwa mpango wa ununuzi wa meli mpya yenye uwezo wa kupakia abiria 1200 na mizigo yenye uzito wa tani 50 kwa njia ya mkopo ambao ungelipwa katika kipindi cha miaka tisa ambao una thamani ya Dola za Kimarekani milioni 25 (US $ 25,000,000) umekwama kutokana na kutoridhiwa na serikali baada ya kuonekana gharama za ununuzi wa meli hiyo ziko juu.

Mhe. Spika, pamoja na maelezo yaliyotolewa, kamati inashauri serikali kuupitia tena mpango wa shirika wa ununuzi wa meli mpya kwa njia ya mkopo, mpango ambao utasaidia katika kulirudishia shirika hadhi yake kwa kuwa na meli ya uhakika itakayoliingizia mapato shirika hilo. Pia azma hiyo itazidi kutoa unafuu wa usafiri kwa wananchi wa Zanzibar na jirani. Hivyo kamati inadhani ununuzi wa meli kwa njia ya mkopo kwa hivi sasa, ndio njia nafuu itakayoweza kufanikisha azma hiyo. Ikiwa njia hii ya mkopo wa ununuzi wa meli mpya itaonekana ni ngumu kutekelezeka, basi kamati yetu inaishauri serikali kutafuta njia nyengine mbadala, ambazo zitaweza kufanikisha azma hiyo kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, kuhusiana na bandari ambayo ni sehemu muhimu kwa nchi yetu, kamati baada ya kupokea taarifa ya shirika na kutembelea baadhi ya maeneo ya Bandari ya Malindi ilibaini kuwepo kwa changamoto kubwa ya kuwepo kwa mlundikano wa makontena katika bandari hiyo, hali ambayo imekuwa ikisababishwa na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na uchelewaji wa wafanyabiashara na taasisi nyengine katika kuondosha mizigo yao. Sababu nyengine inayochangia hali hiyo ni upungufu wa zana za kisasa za kunyanyulia makontena katika bandari zake, zana ambazo kamati ilifahamishwa kuwa zina gharama kubwa. Pamoja na hali hiyo, kamati ilipata fursa ya kuona namna baadhi ya zana mpya za kunyanyulia na kupanga makontena ya mizigo zilizonunuliwa na shirika, zinavyoweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, kamati ilifahamishwa changamoto kubwa ya kuzidiwa kwa uwezo wa Bandari ya Malindi katika kutoa huduma kwa meli za mizigo na abiria zinazotoka nchini na nje ya nchi. Hali hiyo inapelekea haja ya kuwa na bandari nyengine kubwa zaidi itakayoweza kutoa huduma hizo. Katika kutatua tatizo hilo, shirika limeiarifu kamati yetu kuwa limefanya jitihada ya kutafuta mkopo utakaowezesha kujengwa kwa bandari katika eneo la Mpigaduri itakayotumika katika kutoa huduma kwa meli za kigeni. Hata hivyo, kamati imejulishwa kuwa juhudi hizo zimekwama kutokana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ilitakiwa kudhamini mkopo huo kutoka Benki ya Exim ya Uchina. Kushindwa kufanya hivyo, kamati inaishauri serikali, kutoa msukumo mkubwa katika kufanikisha suala hilo ili bandari iweze kujengwa katika eneo la Mpigaduri.

Mhe. Spika, maeneo yote yanayolizunguka eneo la bandari ni muhimu kuhifadhiwa kwa kuwekewa alama maalum. Kamati ilipotembelea Shirika la Bandari imepata taarifa kuwa, maeneo mengi yanayomilikiwa na Shirika Unguja na Pemba hayana hati miliki, na kwa kuzingatia kasi ya uvamizi na ujenzi wa maeneo mbali mbali kinyume na sheria, Kamati inaendelea kulisisitiza shirika na wizara kwa ujumla, kulipa umuhimu mkubwa suala hilo na kuhakikisha maeneo yote ya bandari yanapatiwa hatimiliki ili kuyalinda maeneo hayo.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo kamati imetoa maagizo ni katika Mamlaka ya Usafiri Baharini kuongeza juhudi katika kufanya ukaguzi wa vyombo mbali mbali vya baharini ili kujiridhisha kuwa vyombo hivyo ni vizima na vinaweza kufanya safari zake bila ya matatizo. Jambo hili ni muhimu kwa ajili ya kuwahakikishia usalama abiria wanaotumia vyombo hivyo pamoja na mizigo yao. Aidha, kamati inaitaka mamlaka kuchukua hatua madhubuti zitakazohakikisha kuwa vyombo vya usafiri baharini vinapakia abiria kwa mujibu wa uwezo wa vyombo hivyo ili kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza pale vyombo hivyo vinapopakia abiria na mizigo kupindukia uwezo wa vyombo hivyo.

Mhe. Spika, wakati wa ziara ya kamati katika mradi wa ujenzi wa uwanja mpya wa ndege wa Abeid Aman Karume, kamati ilijulishwa juu ya kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa msamaha wa kodi kwa vifaa vinavyokusudiwa kutumika katika mradi huo kama vile saruji na vifaa vyengine. Kamati ilielezwa kuwa kumekuwa na uchelewaji wa kupata misamaha ya kodi kwa vifaa hivyo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, jambo ambalo linaweza kuzorotesha kasi ya ujenzi wa uwanja huo.

Kamati inaishauri Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuchukua juhudi za kufanya mawasiliano na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ili kurahisisha suala hilo la misamaha ya kodi kwa vifaa vya ujenzi wa uwanja mpya wa ndege. Ili kurahisisha suala hilo, wahusika wanaosimamia ujenzi huo wawasilishe mahitaji ya vifaa vyote vinavyotarajiwa kuingizwa nchini kwa ajili ya ujenzi na hivyo kuhitaji msamaha wa kodi ili viombewe msamaha huo.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa viwanja vya ndege katika kuongeza mapato na kukuza uchumi na kurahisisha huduma za usafiri kwa wananchi, kamati inaishauri idara na serikali kwa ujumla, kuchukua hatua za haraka ili kuufanya uwanja wa ndege wa Pemba uweze kutumika wakati wote kwa kuuwekea taa zitakazowezesha ndege kutua na kuruka wakati wa usiku. Pia kamati inasisitiza kumalizwa kwa ujenzi wa uzio katika eneo hilo la uwanja kwa ajili ya kuhifadhi eneo lote la uwanja, lakini kubwa zaidi kuhakikisha usalama kwa ndege zinazoruka na kutua katika uwanja huo.

Aidha, kamati inashauri suala la genereta la akiba uwanjani hapo lipatiwe ufumbuzi ili huduma zinazohitajika ziweze kutolewa uwanjani hapo hata wakati umeme unapozimwa. Kamati inaishauri serikali kuyamaliza matatizo hayo kwa kuzingatia kuwa matatizo haya yamekuwa ya muda mrefu na kamati hii imekuwa ikufuatilia juu ya masuala hayo hayo ya taa na uzio katika uwanja huo kwa miaka mingi sasa.

Mhe. Spika, kamati imepokea taarifa za ujenzi wa miradi mbali mbali ya maendeleo, miradi ambayo itawasaidia sana wananchi katika kukuza hali zao kiuchumi,hata hivyo kumekua na matatizo katika ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaovunjiwa nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara pamoja na fidia kwa Mamlaka ya Maji, Shirika la Umeme na Kampuni ya Simu ya *TTCL*, kutokana na gharama za kuhamisha miundombinu ya maji, umeme na simu. Hili linatokana na miradi mingi kutokuwa na kifungu cha kulipa fidia.

Katika miradi ya ujenzi wa barabara ambayo serikali inapata mikopo, kamati inashauri kuwa gharama za fidia ziingizwe moja kwa moja au kwa njia nyengine yoyote, katika thamani ya jumla ya mkopo ili iwe sehemu ya mkopo

huo, kwa ajili ya kuufanya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara usichelewe kutokana na kukosekana malipo ya fidia kwa wananchi watakaovunjiwa kupisha ujenzi wa barabara hizo. Kamati inashauri kuwa mikopo inayotolewa na taasisi ambazo mikopo yake haihusishi malipo ya fidia, gharama hizo ziingizwe kwa njia nyengine yoyote, vyenginevyo serikali ijipange mapema kutenga fedha kwa ajili ya malipo ya fidia.

Mhe. Spika, kamati ilipata maelezo ya kina kuhusiana na miradi mbali mbali ya ujenzi wa barabara nchini,pamoja na ujenzi huo kuendelea vizuri lakini kuna Upungufu katika suala zima la usimamizi wa Wakandarasi wanaojenga barabara mbali mbali zinazofadhiliwa kupitia miradi hiyo jambo linalopelekea kucheleweshwa kukamilika kwa barabara hizo. Kamati ilibaini kuwa wasimamizi hawatoi taarifa mapema kwa wizara mapungufu yaliyopo kwa mkandarasi kama vile uhaba wa wataalam na vifaa vinavyohitajika katika ujenzi, mapungufu ambayo yanaathiri kasi ya ujenzi wa barabara hizo.

Kamati inashauri kuwa serikali iwe na usimamizi madhubuti katika miradi ya ujenzi, utakaowakilisha vyema maslahi ya serikali kwa lengo la kuifanya miradi hiyo ya ujenzi imalizike kwa wakati na kwa kiwango kinachohitajika kwa mujibu wa mkataba baina ya mjenzi na serikali. Usimamizi huo utasaidia katika kumfanya mjenzi kuwa makini na kazi yake na hatimaye miradi hiyo ya ujenzi wa barabara kumalizika kwa wakati na kwa kiwango kitakachozifanya barabara zinazojengwa kudumu kwa muda mrefu. Aidha, kamati inashauri kuwa wizara iwe na kiwango kimoja kwa barabara zote zinazojengwa Zanzibar na kila mjenzi asimamiwe ili barabara zinazojengwa zifikie kiwango hicho.

Mhe. pika, kamati yetu ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zinazoikabili Kampuni ya simu ya *ZANTEL* ambayo ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni mmoja wapo wa wamiliki wa kampuni hiyo. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuzorota kwa zoezi la uwekaji wa mabango. Suala hili Mhe. Spika, naomba niliondoe kwa sababu limekwishazungumzwa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alilichukulia jukumu kusema kuwa ataunda tume ili kulifanikisha. Mhe. Spika, hili naomba niliondoe.

HITIMISHO

Mhe. Spika, katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, kamati imetoa maelekezo na ushauri wake ambao tunaamini kuwa utasaidia katika kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu ya serikali na kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Maelekezo na maoni hayo yalitolewa na kamati kwa dhamira ya kuwawakilisha

vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao na kwa mujibu wa sheria yanapewa kipaumbele.

Mhe. Spika, mwisho Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi inawashukuru uongozi wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano chini ya mawaziri wake, makatibu wakuu wake na watumishi wote wa taasisi za wizara hizo, ambapo ushirikiano uliotolewa na watumishi hao, umeiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa sana.

Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Pandu Ameir Kificho na Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim na watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwanza kwa kuiwezesha kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa ushauri walioupatia kamati yetu katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mtakubaliana nami uwezo mkubwa nilioutaja wa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ripoti hii ya uwasilishaji ilikuwa ndfu lakini ameiwasilisha kwa muda wa dakika ishirina na kidogo hivi. Sasa tujadili ripoti hii na nianze kumkaribisha Mhe. Subeti Khamis Faki baadae Mhe. Rashid Seif Suleiman. Wakati huo huo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tunakwenda kupumzika kidogo nje tukumbuke kurudi ili sijeikashusha *quorum* tukashindwa kuendelea na shughuli yetu. Mhe. Subeti endelea.

Mhe. Subeti Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa na mimi kuchangia ripoti hii ya kamati. Mhe. Spika, kwanza mimi nianze na suala la Wizara ya Ardhi, Makazi, Maji na Nishati na naomba nianze kwa kuzungumzia suala la umeme. Suala la umeme wazee wa kale walisema kwamba, “Mtumai cha ndugu hufa masikini”. Mhe. Spika, nasema hivi kwa kuiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba wakati sasa umefika wa kufanya jitihada za makusudi kupata umeme mbadala katika visiwa vyetu vya Zanzibar. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Spika?

Mhe. Spika, nasema kwa masikitiko, ndugu zetu wa *TANESCO* wanatupandishia bei au wanaipandishia bei ya umeme *ZECO* ambao umeme huu ni matumizi ya wananchi wa Zanzibar bila ya huruma na imani. Kwa sababu kupandisha bei kwa asilimia 168 badala ya asilimia 21 kwa kweli ni masikitiko makubwa. Suala hili kama alivyozungumza Mhe. Mwenyekiti kwenye ripoti yetu, suala hili limekuwa ni sugu na lina muda mrefu, namuomba

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kupitia kwake, suala hili serikali ilione ni suala muhimu na ilitilie mkazo ili kulipatia ufumbuzi. Kwa sababu sasa hivi tunadaiwa shilingi bilioni 40 mwisho wake umeme Zanzibar utakuja kukatwa, tutakuja kufika pale nyuma tulikorudi.

Namuomba Mheshimiwa suala hili alione kama si suala la masihara. Pamoja na rais kuliingilia kati, lakini wao bado wanaandika deni ile ile na hawarudishi nyuma. Kwa hivyo,

Mhe. Spika, suala hili serikali lazima ilivalie njuga kupatiwa ufumbuzi, mkisema kwamba suala hili lizungumzwe kwenye kero za Muungano litachukua muda na likichukua muda deni ndio inazidi kuongezeka na ikiongezeka tunaweza kujakaa giza tena. Kwa hivyo, suala la msingi ni kuachana na kutumaini cha ndugu tukatafuta chetu. Sasa kuna haja ya serikali kusimama kwa kina kabisa ikaona kwamba kuna mpango wa makusudi kupata umeme mbadala Zanzibar ambao utakuwa ni umeme wa kudumu, kuliko kung'ang'ania umeme huu wa ndugu zetu kwa sababu mwisho wanatufanya hivyo. Sisi tunawatumainia ndugu zetu lakini wao hawana huruma na sisi.

Kwa sababu ilikuwa waone kwamba sisi ndugu zao watuonee huruma, lakini sisi kama wateja wakuu *TANESCO*, *ZECO* ni mteja wake mkuu wa umeme, lakini yule mteja mkuu ndio anayeongezewa bei kuliko watu wengine.

Mhe. Spika, hili suala naiomba serikali ilione kama ni suala muhimu kweli kweli na cha msingi ni kupata umeme mbadala Zanzibar wa kudumu.

Mhe. Spika, jengine ni suala la kesi za ardhi. Kama Mhe. Mwenyekiti alivyozungumza kwenye ripoti suala la kesi hizi za matatizo ya ardhi zimekuwa nyingi sana na kwa kweli Baraza lililopita tuliambiwa kwamba kila mkoa itawekwa Mahakama ya Ardhi ili kuzipunguza. Hatuwezi kuwalaumu watu wawili kuhukumu kesi ambazo kila leo suala la matatizo ya ardhi linaongezeka. Kwa hiyo, kesi zimerundikana wanajitahidi kuzifanyia kazi lakini bado kuna umuhimu wa wizara kusimamia kuwaomba watu wa Mahakama kuongeza mahakimu wa ardhi ili kesi hizi zitatuliwe na zipunguzwe.
Kwa sababu matatizo ya ardhi kila leo yanaongezeka, kwa hiyo ni muhimu kwa aliyekuwa na kesi yake anataka atatuliwe ili ajue haki kama ni yake au si yake. Sasa suala hili halitaki kuwekwa muda mrefu kwa sababu tukichelewesha watu wanaweza wakachukua sheria ambayo si ya kwao. Kwa hiyo, hili naomba muone kwamba lina umuhimu kuongeza mahakimu ili kesi hizi za matatizo ya ardhi zimalizike.

Mhe. Spika, jengine ni suala ambalo nitalizungumza kwa masikitiko kidogo. Mhe. Spika, Kamati za Baraza la Wawakilishi zinafanya kazi kwa mujibu wa

sheria. Sasa Mhe. Spika, sisi tunafanya kazi kwa ajili ya Baraza la Wawakilishi zima, hatufanyi kazi kwa ajili ya kuwa mtu ni kazi yake binafsi. Kwa hiyo, kamati zako Mhe. Spika, zina uwezo wa kumwita mtu yeyote ambapo inaonekana kuna tatizo na kufanya suluhu. Sisi sio wahasihu, sisi tunakwenda kama kufanya suluhu.

Mhe. Spika, masikitiko yangu ni kwamba Mhe. Waziri juzi alipokuwa akizungumza hapa alisema kwamba Kamati ya Baraza la Wawakilishi hazina haki ya kumwita mtu bali ina haki ya kuwaita mawaziri wakazungumza nao. Sasa Mhe. Spika, sisi tunakwenda kwenye kamati tunawakuta watendaji tunazungumza nao tunapanga tunakwenda huko bila ya waziri kuwepo na hiyo ndio ilivyo. Tukiona kama kuna haja ya kumwita waziri basi tutamwita waziri pale ambapo tutaona pana shida ya kumwita waziri.

Lakini Mhe. Spika, sisi tulikwenda kufanya kazi zetu kutokana na kuona kuna matatizo. Matatizo yaliyokuwepo ni *Zantel*, *Tigo*, watendaji wa Baraza la Manispaa na baadhi ya wengine. Kwa hiyo, sisi tukamwita Mkurugenzi wa Mawasiliano, tukawaita watu wa Zantel, tukawaita watu wa Baraza la Manispaa, pamoja na watendaji wengine waliokuwepo. Tukawaita ndani ya Baraza la Wawakilishi katika chumba namba mbili cha Kamati za Baraza la Wawakilishi.

Tulipoingia Mhe. Spika, tulizungumzia nao kama watendaji kama kamati yako kwa sababu tulikwenda Pemba tukaona kuna matatizo ya ardhi tukawaita watu wa Vitongoji tukazungumza nao tukalipatia ufumbuzi suala na hapa tukaona kuna haja ya kuwaita ili tuje tuzungumze nao tupate ufumbuzi.

Lakini Mhe. Spika, linalosikitisha ni kwamba kamati zako tunafanya kazi kwa mujibu wa sheria tunaomba utulinde. Leo lililokuja hapa masikitiko yangu ni kuambiwa kama watendaji wa Baraza la Manispaa tuliwatukana na sisi hatukuwatukana. Tuliwaweka tukazungumza nao tukawaambia tupeni *document* zenu, tupeni mikataba. Wakatoa mkataba wa *Zantel*, halafu tukawauliza je, hawa Tigo wana mikataba. Jamani kwa nini mnavunja mkataba au kama wana mkataba watupe.
Kwa kweli wale watu wa mikataba wakatuthibitishia kama *Zantel* wana mikataba, *Tigo* hawana. Walikwenda kupachuliwa mabango yao siku ya Jumapili, tukawauliza kwa nini hawa Jumapili sio siku ya kazi mlikuja kuwapachulia, lakini hawa wa Tigo walipachika siku ya kazi msiwapachulie na hawana mikataba kwa nini. Wao wenyewe wakathibitisha kama wale mkataba hawana. Tukawauliza je, hawa *Zantel* mkataba umeshavunjwa, bado haujavunjwa, kwa nini mkawapachulia.

Mhe. Spika, cha msingi sisi tulichowaambia watu wale kwamba waheshimiwa heshimuni mikataba yenu kwa sababu unapovunja mikataba mtakuja kuitia serikali kwenye matatizo. Kwa sababu ukivunja mkataba ukishtakiwa utalipa mapesa mengi.

Mhe. Spika, tulizungumza nao kistaarabu, leo cha kusikitisha ni kuja kuambiwa kamati yetu kwamba wale watu tuliwatukana. Mhe. Spika, nakuomba kwa heshima kubwa kamati zina haki ya kumwita mtendaji yeyote. Tunakuomba Mhe. Spika, kamati mzilinde msiwape *power* watendaji wakatudharau. Kwa sababu hiyo tukiwapa *power* watendaji watudharau sisi Kamati ya Baraza la Wawakilishi na ikidharauliwa kamati limedharauliwa Baraza zima la Wawakilishi.

Mhe. Spika, watendaji tunazungumza nao, leo mtendaji anazunguka anamwambia waziri tumemtukana na waziri anakubali moja kwa moja. Mhe. Spika, hii inanisikitisha, kamati zako zipe *power* zilinde, Baraza lako litadhalilishwa. Haiwezekani sisi tumeshafanya kazi kwa mujibu wa kanuni halafu tuje tuambiwe tumemtukana mtendaji. Sisi tumtukane mtendaji kwa mujibu gani. Sisi tumewaambia mnapoweka mikataba iheshimuni.

Walikuwepo watu wa aina mbali mbali, alikuwepo Mkurugenzi wa Mawasiliano na yeye akawaambia. Mimi ikabidi sasa nichunguze mikataba yetu baina ya barabara na sisi. Leo Mhe. Spika, watendaji wanakuja wanasema tumewatukana inasikitisha kweli kweli. Mhe. Spika, naomba niheshimu muda wako naomba nimalizie hapo. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, napenda nichukue muda mdogo lakini nitoe zile changamoto kubwa ambazo ziko katika wizara mbili hizi na ambazo zingesaidia sana kutatua matatizo ya wananchi. Mhe. Spika, nikianza na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Ujenzi na Nishati kuna changamoto kama nne hivi. Kwanza ni suala zima la utumizi wa ardhi. Kama vile ambavyo tulizungumza huko nyuma wizara ina changamoto ya kuweka mipaka sahihi ya matumizi ya ardhi za majenzi, viwanda, mahoteli, kilimo na mengineyo kwa maslahi ya nchi hii.

Kwa hivyo, mimi namuomba sana Mhe. Waziri na baadae Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kama kuna kiwango kidogo cha kuongeza kuhusiana na suala zima la upimaji wa ardhi, basi ni afadhali tufanye mapema kuliko kungojea tumechelewa sana na baadae ardhi kuitafuta inakuwa ni tabu. Kwa sababu pale ardhi imeshatumika vibaya si rahisi kuipata tena ardhi ile.

Tumeona matumizi mabaya ya ardhi katika maeneo mengi na hususan ardhi ya kilimo inakwenda na baadhi ya sehemu. Kwa hivyo, suala hili ni changamoto kubwa kwa sababu lina matokeo sio mazuri katika siku za mbele.

Mhe. Spika, suala la pili nataka nitaje sentensi moja tu kwa sababu limeshazungumzwa kuongeza nguvu katika Mahakama za Ardhi ili kesi ziende haraka. Watu wanavunjika moyo kabisa lakini kwa sababu pana haki yake mtu anashindwa kusema kwamba siendi. Lakini tarehe zinakuwa ni nyingi sana za kupigwa mbele kwa sababu bado hatujajiweka sawa katika kushughulikia Mahakama ya Ardhi.

Utafiti unaonesha kwamba Wilaya ya Magharibi ingepata Mahakama yake. Kwa hivyo, kama vile ambavyo imeshatayarishwa sasa hivi kwa Wilaya ya Wete basi Wilaya ya Magharibi ingepata Mahakama yake mambo kidogo yangepungua hapa ya mjini.

Lakini Mhe. Spika, changamoto nyengine kama ambavyo wananchi wengi wanaiona ni upatikanaji wa maji hasa katika maeneo ya mjini Unguja na sehemu nyengine. Masuala haya inabidi yakaliwe kitako kidogo kwa sababu yana sehemu tatu. Kwanza suala zima la upatikanaji wa umeme sahihi kwa sababu pampu nyingi zinaungua kutokana na umeme ambao hautulii.

Lakini la pili ni suala la miundombinu yenyewe ya kupelekea maji imechakaa sana na mingine hata haijulikani. Tulikuwa tunajaribu kuwauliza ni njia gani ambayo wanatumia kuweza kuzijua zile *network* za zamani kwa sababu wale mafundi wengi wa zamani wameshastaafu. Utaratibu mpya ni kutumia *satellite*, lakini kwa sababu mingine haijaungwa karibuni ni ya zamani hata hiyo *satellite* itakuwa haiwezi kuona. Kwa hivyo, nadhani kama ambavyo walitwambia wataalam ni vizuri kwamba *network* yoyote inayowekwa sasa hivi basi iwekewe na vifaa ambavyo vitaangaliwa vile vile katika mitambo ya *satellite*.

Mhe. Spika, suala la upatikanaji wa umeme katika kisiwa cha Pemba tunaishukuru sana serikali kwa kupitia Serikali ya Norway kwamba umeme mwingi umepatikana lakini matumizi yake bado ni madogo sana. Kwa hivyo, tunaomba serikali iwafikirie sana kuwakopesha wananchi umeme kwa sababu sasa hivi wananchi wengi wakati serikali mshahara wa ngazi ya chini ni shilingi laki moja mwananchi wa chini kabisa anatarajiwa alipe shilingi laki tano na thalathini elfu ili aweze kuungiwa umeme.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, utaona ni ugumu kiasi gani uliopo kwa sababu kabla ya hapo inabidi anunue vifaa vyote vya kufanyia *fitting* na halafu tena ndio aombe kuungiwa umeme. Pamoja na kwamba shirika linatoa mkopo lakini

mkopo ule bado ni mkubwa kwa sababu analipa kuanzia asilimia 50 mpaka 60. Kwa hivyo, kwa wananchi si rahisi sana kumudu hali hiyo.

Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri atueleze kama kuna mpango wowote ambao wameufikiria wa kuweza kuwapa nafuu wananchi waweze kuunga umeme kwa wingi. Kwa sababu sasa hivi utaratibu unaotumika ni kuunga umeme wa TUKUZA moja kwa moja.

Lakini Mhe. Spika, suala hili la deni la umeme kwa *TANESCO* baadhi yetu tunavyojua kwamba ukiomba umeme kuununua pahala ambapo sio sehemu yako *(bulk purchase)* kuna mikataba yake. Kwa hivyo, ningeliomba wizara ikawa na utafiti kidogo wa kuona kwamba mikataba ya nchi mbali mbali inafanywa vipi na sisi tutakwenda kujitetea vipi. Hivi karibuni tulipata taarifa kwamba Kenya wamenunua umeme rahisi kutoka Ethiopia na wako tayari kuuza katika soko la Afrika ya Mashariki. Sasa tukifanya utafiti utatuwezesha kuweza kupata ule uhalisia wa mambo na tunaweza kwenda kujitetea.

Lakini suala la urais wa Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete unamalizika mwaka 2015 na aliyetoa amri ile kwamba ilipwe asilimia 21 ni yeye. Wasi wasi wetu ni kwamba kwa sababu *TANESCO* wanaendelea kulileta hili deni bila ya kuzuia isijekuwa ukimaliza suala la urais wa Mhe. Kikwete akaja mwengine akasema anayelitambua ni lile la *TANESCO*. Kwa hivyo, naiomba sana serikali iweze kulishughulikia suala hili ndani ya urais wa Mhe. Kikwete ambaye alitoa agizo la kuwaachia Zanzibar ilipe asilimia 21 na sio asilimia 168. Suala hili kama ni *official* basi Zanzibar iwe na mikataba ambayo *TANESCO* itakuwa hawana tena njia ya kutokea katika mikataba hiyo.

Mhe. Spika, suala la mwisho katika wizara hii napenda nichangie kidogo mjadala uliopo kuanzia kipindi cha karibuni kuhusu Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe imetiliana saini na *UNESCO*. Wataalam wanasema Zanzibar ingeweza kufuata masharti au ikajitoa mapema ili iweze kulinda heshima yake. Sasa naomba sana wizara na serikali ikiwa tunaona kwamba serikali inajiweza kuleta maendeleo zaidi badala ya kukaa na mkataba wa hifadhi ya Mji Mkongwe ni bora kama wataalam wanavyosema tujitoe na mapema tulinde ile heshima yetu.
Lakini tukiona kwamba tunahitaji kuwa na mkataba na *UNESCO* kwa hifadhi ya Mji Mkongwe basi ni afadhali tuweze kukubaliana nao na tuendelee katika hali ya kukubaliana nao. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Mhe. Spika, pili

nimpongeze Mwenyekiti mwenzangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk pamoja na kamati yake kwa kazi kubwa waliyoifanya na kuwasilisha kitaalam sana ripoti yake. Mhe. Spika, mimi nina mambo manne katika ripoti hii na mengi yatagusia jimbo langu kwa sababu muda mrefu sijapata kuzungumza.

Mhe. Spika, kwanza niishukuru serikali na kuipongeza kwa jitihada kubwa wanayofanya kuwatafutia wananchi maji yaliyokuwa salama. Nashukuru kwenye jimbo langu tumepata mradi wa majimbo matatu, Kitope, Bumbwini na Mfenesini, mradi ambao unasaidiwa na wenzetu unaoitwa *ACRA*. Huu mradi kwa kuutazama umekamilika kwa sababu mabomba yamesambazwa yameshafukiwa, mashine zimeshafungwa kwenye visima, tangi limeshamalizika, vijana wameshaelimishwa jinsi ya kukusanya mapato, lakini sasa unakaribia mwaka haujafunguliwa na zogo limekuwa jingi.

Sasa Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hebu atwambie pana siri gani, pana utaalam umekosewa, pana muda maalum umewekwa ndio huu mradi ufunguliwe, ama tatizo gani, ili wananchi wa majimbo matatu wapate faraja. Kwa hivyo, naomba hili Mhe. Waziri kama hulitambui basi unong'one na watendaji wako tupate jibu ili liwape moyo wananchi.

Lakini pia katika mradi huo wa *ACRA* katika jimbo langu umeacha kijiji kimoja Mkanyageni kwenda Mndo. Upande wa mradi wa awamu ya pili wa Wajapan umepita Kijichi kutokea Mndo na tayari watu wa Bububu na Kijichi wamefaidika. Lakini watu wa Mndo kwenda Mkanyageni hawamo kwenye ACRA wala hawamo kwenye Japan.

Kwa hivyo, naomba na hili wizara baadae tukae pamoja ili niweze kuwatatulia matatizo wananchi wangu wa Mkanyageni, ambao hawakutiwa kwenye mradi wa ACRA wala mradi wa Wajapan wa awamu ya pili. Hili pia ni tatizo na wananchi wanasumbuka sana kupata maji katika eneo hilo.

Jengine Mhe. Spika, nije kwenye suala la eka. Tulibahatika Mfenesini kulikuwa na mradi wa minazi kwa muda mrefu sana Selemu. Wananchi wa baadhi ya maeneo yale walinyang'anywa na kuwekwa miradi ya maendeleo na tukaambiwa kama mradi utakuja kufa basi wananchi wale wanaweza wakarejeshewa maeneo yao. Lakini kwa bahati mbaya maeneo yale wamepewa wenzetu wakubwa, sisi hatukukataa na tukaomba basi tutafutiwe maeneo mengine, kwa bahati nzuri yamepatikana katika sehemu moja inaitwa Mbuzini Nguruweni. Mhe. Waziri Kiongozi aliyeondoka aliunda kamati akasimamia upimaji wa eka hizo, tayari zimepimwa na eka zipo, lakini kuna kigugumizi cha kugaiwa.

Kwa hivyo, nina wasi wasi mabadiliko ya awamu ya sita kwenda ya saba, wajanja wakatumia njia hiyo na kuwapa watu wasiohusika. Naomba suala hili wizara ilifuatilie ili tujuwe wananchi wa Mfenesini na Mbuzini watapewa lini eka zao katika eneo ya Nguruweni ili kuondosha matatizo.

Jengine Mhe. Spika, ni suala la umeme. Umeme wenzangu wamezungumza, lakini tulisikia hapo nyuma walikuja wataalamu kufanya utafiti juu ya umeme wa kuzalisha kwa upepo pamoja na maji ya bahari, ili kuondosha huu usumbufu tulionao. Lakini hadi hii leo hatujapata taarifa yoyote. Sasa naomba na suala hili kama jawabu lipo basi tupewe ili tuweze kupata faraja.

Vile vile Mhe. Spika, wenzetu wa Shirika la Umeme walisema kwamba kutokana na umeme wa kusoma mita watu wanaiba sana umeme. Kwa hivyo, wamekusudia katika maeneo yote wafunge TUKUZA. Walitoa mfano kwa sehemu watakazoanza kwa haraka haraka ilikuwa ni sehemu ya Bububu na sehemu ya Kwerekwe. Nashukuru Kwerekwe kituo kimeshajengwa na kimeshafunguliwa watu wananunua umeme wa TUKUZA, nadhani wameshafungiwa.

Lakini Bububu sina hakika watajenga pahala gani au kituo kitafunguliwa wapi, kwa sababu bado mradi huo haujaanza. Je, nataka niulize na kwa upande wa Bububu suala hili litafanywa lini?

La mwisho kabisa Mhe. Spika, nije katika suala la barabara. Nashukuru serikali imetusaidia kujenga barabara ya Mfenesini kwenda Bumbwini. Tatizo lililojitokeza kwenye ujenzi wa barabara hii ni kwamba mazao ya wananchi thamani iliyotiwa ni ya zamani sana, tangu ukoloni. Utakuta mtu ana mgomba na mgomba ule una miche sita, lakini unahesabiwa mgomba mmoja tu yaani ule mgomba mama, watoto wake wote hawahesabiwi. Au jimbi utakuta moja lina matoto lakini wale wote hawahesabiwi. Sasa yale ni mambo ya zamani sana.

Kwa hivyo, ningeshauri kwanza serikali ingetazama bei ya sasa hivi ikabadili katika sheria ya tangu ukoloni, ili wananchi inapofanywa maendeleo na wao kidogo wapate kutononoka. Lakini maendeleo yanafanywa wananchi wanazidi kudidimia, itakuwa sio lengo zuri kwa serikali. Kwa hivyo, nashauri wizara itazame bei ya mazao kama mnazi, muembe, mpea, migomba, majimbi na mengineyo ili wananchi wapate kutononoka kwenye barabara, lakini na kwenye vyakula vyao.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, hivi sasa tunashukuru serikali kujenga barabara ya awamu ya pili njia ya Benjamini Mkapa, hii barabara iliyotoka Amani kwenda Daraja Mbovu Mtoni au Kwa Maalim Seif. Barabara inajengwa haraka haraka

sana, lakini ina tatizo moja hii ya zamani iko juu sana na hii mpya inachimbwa sana kwenda chini. Halafu hawaweki *level* kwa haraka ikakaa sawa sawa na ile ya zamani, wanachukua eneo kubwa inakuwa ni hatari mashimo makubwa upande mmoja kwa usafiri wa barabarani pamoja na watu wanaokaa katika maeneo yale.

Kwa hivyo, nashauri ujenzi hatuukatai, lakini wangekwenda hatua ndogo ndogo wakakamilisha halafu ndio wakasonga mbele. Kwa wanavyokwenda sasa hivi, wakati wowote inaweza kutokea hatari na maafa na kwa mvua zinazokuja. Kwa hivyo, nashauri kwamba ile sehemu ambayo wameshaichimba sana basi ingefukiwa mpaka ikakaa sawa, halafu wakaendelea kwenda mbele. Kuliko kuchukua eneo kubwa sana wakaliwacha nyuma shimo kubwa huku wanaendelea mbele tu na hizo mvua zinazokuja inaweza ikaleta maafa. Huo ndio ushauri wangu.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, pia naunga mkono kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini, ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii tena kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Makame Mshimba Mbarouk pamoja na kamati yake. Nawapongeza sana kamati hii.

Mhe. Spika, mimi nitachangia mambo mawili katika ripoti hii. Jambo la kwanza ambalo nitachangia Mhe. Spika, ni suala la umeme. Kumetokea tatizo la umeme ambalo limetukabili katika nchi yetu hii na hata hapa Barazani ni mashuhuda tunakuwa tunapata tatizo la umeme kukatika katika.

Mhe. Spika, nakumbuka katika kipindi kile cha tatizo la umeme ambalo lilitukabili karibu miezi kadhaa iliyopita na baadae kwa juhudi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikaweza kulitatua tatizo lile. Lakini katika kipindi kile Mhe. Spika, serikali ilitamka kwamba itanunua majenereta ambayo yatasaidia wakati wa matatizo yanapotokea ya ukatikaji wa umeme.

Sasa Mhe. Spika, sijui kwa nini wakati kipindi hiki ambacho tuko katika matatizo haya ya umeme majenereta yale ambayo tuliambiwa, hatuyaoni kutumika. Sasa sielewi kuwa majenereta yale yapo au hayapo. Kwa hivyo, ningeomba wizara husika itueleze ili tujuwe kipi kinachoendelea katika matatizo haya ya umeme.

Mhe. Spika, katika tatizo hilo hilo la umeme mbali kwamba tatizo linaendelea, lakini kuna tatizo ambalo hata ya kununua ule umeme wenyewe. Mhe. Spika,

watumiaji wa umeme ni wengi, yaani wananchi wa Zanzibar wengi wanatumia umeme, lakini wakati wanakwenda kununua umeme wananchi wanapata tabu. Utakwenda pale kwenye vibanda vya kununua umeme Mhe. Spika, unakuta kuna foleni kubwa sana. Sasa sioni kwa nini wizara pamoja na shirika isiweze kusambaza huduma hizi kwa njia rahisi ya kujenga vibanda vya kuuzia umeme huo.

Mhe. Spika, katika ripoti ya kamati hii ambayo nimeiona hapa, kuna tatizo la ulipaji wa madeni katika taasisi za serikali. Mhe. Spika, takriban bilioni 4 taasisi za serikali zinadaiwa na Shirika la Umeme. Suala hili linawapa mzigo wananchi, kwa sababu Shirika linapata tabu, inakuwa mzigo mkubwa, kwa hivyo inapunguzia nguvu za shirika kuweza kuendesha Shirika hili la Umeme.

Kwa hivyo, ningeomba wizara kufuatilia kwa kina ili kuhakikisha kwamba taasisi zetu za serikali basi zinafungwa zile mita za TUKUZA ili kuweza kudhibiti kutokulipa huu umeme.

Mhe. Spika, jengine nije kwenye suala la maji ambalo ni tatizo sugu katika nchi yetu, hasa katika maeneo ya mjini. Mhe. Spika, serikali au wizara imefanya juhudi katika kuondoa tatizo hili la maji kwa kuleta wataalamu na wahisani kutoka Serikali ya Japan au China ili kutusaidia katika kuondoa tatizo hili la maji. Lakini tatizo liko pale pale.

Lakini Mhe. Spika, mimi mwenyewe kwa kushirikiana na mbunge wangu tunaona kwamba maji yapo, lakini kuna sehemu watu wanakosa maji, tatizo ni nini. Basi Mhe. Spika, tuliweza kubadilisha mabomba mengine na tukaweka mabomba mapya.

Mhe. Spika, katika jimbo langu kwenye maeneo ya Gulioni na Mwembeladu, baada ya kubadilisha mabomba yale na kuweka mapya, basi wananchi sasa hivi wanapata maji. Sasa mimi nadhani tatizo pia ni miundombinu, hivyo naiomba wizara iweze kubadilisha mabomba na kuweka mapya, yale mabomba ya zamani hayafai, yanafanya kutu ndani, kwa hivyo yanazuia hata yale maji kupita.

Kwa hivyo, ningeiomba wizara, kwa sababu hata kamati hapa imeeleza kuwa tatizo hilo lipo. Kwa hivyo, wafanye bidii kuweza kubadilisha miundombinu katika maeneo ya mjini.

Mhe. Spika, katika maeneo ya mjini, hususan katika maeneo ya majumba ya Michenzani. Sote tunayajua majumba ya Michenzani yanapokosa maji basi inakuwa shughuli ni pevu. Majumba yananuka.

Mhe. Spika, tatizo ambalo linayakabili majumba yale hasa jumba nambari 2 na nambari 4 ni tatizo kubwa la maji, hayana maji, hata yale maji ya mgao hawayapati. Sasa utashangaa kwa nini majumba mengine yanapata lakini yale hayapati. Suala hili naiomba wizara kuweza kuliangalia kwa kina ili kuhakikisha kwamba maeneo ya mjini hasa katika majumba ya Michenzani yanapata maji.

Mhe. Spika, baada ya kusema haya, na mimi naunga mkono ripoti hii ya kamati kwa asilimia mia moja, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rahaleo.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Mimi nitachangia zaidi kuhusu usafiri wetu wa ndani hivi sasa.

Mhe. Spika, hivi sasa tuna usafiri mkubwa ambao tunautegemea hasa Pemba ni wa ndege. Usafiri huu una matatizo makubwa ambao naona nichangie labda Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hawajaangalia matatizo yake yakoje.

Mhe. Spika, ndege hizi tunazozipanda kuelekea Pemba hivi sasa kuna matatizo makubwa ambapo rubani wa ndege anakuwa mmoja tu. Utakuta kwamba uzima hautegemei kuwa baada ya dakika tano sitobadilika na uzima wangu au vipi. Ndege zile utakuta zinapaa sana, lakini utaona rubani yule ni mmoja tu hana msaidizi wake.

Kwa hivyo, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wangekaa na kuliangalia hili suala kuwa usafiri wa Pemba una matatizo makubwa hasa kwa upande wa ndege, hivyo urekebishwe. Ni lazima ndege ziwe na rubani wawili ili waweze kujiamini kama wanavyojiamini hivi sasa.

Mhe. Spika, unajua inapotokezea tatizo angani, mfano rubani akapata presha rubani yule au anapoumwa na tumbo sijui atamuachia nani abiria wake wa kuweza kuwasaidia kufika safari yao. Kwa hivyo, ningeomba suala hilo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilirekebishe na liweze kufanyiwa mabadiliko mengine.

Mhe. Spika, tatizo letu la barabara ni kubwa sana hasa katika Jimbo langu la Koani kwa watu wanaoishi kisiwani Ng'ambwa. Sijui kuna tatizo gani Uzi/Ng'ambwa lisiwekwe daraja la kudumu miaka yote. Tangu ilipoundwa dunia barabara ile ya Uzi haijafanyiwa marekebisho yoyote hadi leo. Utakuta wanaishi watu tena wengi ambao hawana mawasiliano mazuri ya kutoka Uzi Ng'ambwa na kuweza kufika katika maeneo mengine, sielewi kuna sababu gani lisiwepo daraja ambalo halichukuwi hata kilomita tano, lisiweze kujengwa kwa muda mfupi.

Utakuta Tanzania hii kuna madaraja ya kilomita 50 ya madaraja na watu wanafanikisha, sasa itakuwaje daraja dogo kama hili liwe limeshinda kwa zaidi tangu karne za miaka hiyo. Mimi naomba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hili suala waliangalie upya ili kulidhibiti sehemu ya Uzi ili ipate mawasiliano mazuri ya usafiri.

Mhe. Spika, hakuna sababu kwamba hata angalau pantoni ya kuweza kuvuka pale lisiwepo na utakuta mara nyingi wananchi wa Uzi wanazaa njiani. Kwa hivi sasa utakuta mawasiliano ya usafiri wa gari nyingi haziendi Uzi kupeleka abiria, wanasema hali ya barabara ni mbovu na hakuendiki. Ni afadhali serikali ingeamua wazi kuweza kupatiwa pantoni kama nchi nyengine likaweza kufanya mawasiliano mazuri, kama inashindikana hilo daraja kujengwa kwa muda mfupi. Hayo ni matatizo ambayo nayachangia kwa kutokana na barabra.

Mhe. Spika, sasa nichangie masuala ya umeme. Umeme hivi sasa ni mgumu sana hasa kwa mita zetu za hivi sasa. Ni afadhali watu wote tungeunga mkono kwamba hii TUKUZA kwa mnyonge inasaidia hasa kujua matumizi yake anayotumia. Kama mtu atakuwa hana pesa kwa siku ile, basi analala giza kwa siku moja na siku ya pili anajua vipi afanye mawasiliano ya kupata umeme. Mita zinasumbua sana wanyonge, pengine bei unayowekewa sio unayotumia na watu wengi ambao hawawezi kutengeneza umeme basi hawafahamu kwamba mimi naweza kutumia umeme kiasi gani.

Kwa hivyo, naomba utaratibu wa umeme ubadilishwe na nchi nzima bora tuwekewe mita za TUKUZA basi tutakuwa tunajiamini kwamba tuna umeme wa uhakika kuliko huu uliopo sasa.

Mhe. Spika, kama tunavyoongezewe madeni na umeme kutoka Bara, pengine sisi hapa wenyewe mtu anaongezewa bei ya umeme wakati hafahau kuwa mimi nimetumia mwezi huu kiasi gani na mwezi unaokuja kiasi gani. Afadhali tuwe na TUKUZA, ili tupate kujiamini kwamba uwezo wangu ni kuwa natumia Shs. 200/= kwa siku au Shs.1,000/= kwa siku.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia kwa mia kwamba inavyokwenda ni sahihi. Ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu katika maelekezo ya kamati ambayo ndugu yetu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, amekwisha kuitolea maelezo.

Kwanza kabisa nachukua nafasi hii kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa namna tunavyokwenda na shughuli zetu. Vile vile nachukua fursa hii

kumshukuru Mhe. Makame Mshimba, Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi pamoja na wajumbe wote wa kamati hii kwa kutayarisha ripoti safi kabisa na makini kabisa, ambayo inaweza kutoa dira ya mwelekeo wa maendeleo katika Zanzibar yetu.

Mhe. Spika, kwa kuanzia nitaanza na suala la uzito wa serikali katika kutoa hati kwa taasisi na baadhi ya maeneo ya ardhi. Mhe. Spika, nahisi wakati umefika sasa kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuweza kuzipatia hati zile afisi ambazo ni za serikali na maeneo ambayo yanamilikiwa na serikali ili taasisi hizo ziweze kumiliki hati zake.

Vile vile ningependa kuchukua fursa hii kuzungumzia suala la wale wakaazi wa nyumba za maendeleo. Kwa mfano nyumba za Michenzani, Kiwajuni na Kilimani. Kwa taarifa tulizonazo ni kwamba kuna mapendekezo ya wale watu ambao waliweza kukabidhiwa nyumba hizi ili waweze kupatiwa hati za kumiliki nyumba zile. Sasa muda umekuwa ni mrefu na hati hizi bado hawajamilikishwa hawa watu. Tunaiomba taasisi na wizara husika ili iweze kulifuatilia suala hili na tuhakikishe kwamba suala hili linakamilika.

Jengine Mhe. Spika, katika kuchangia hoja hii ni suala la umeme. Kusema kweli Mhe. Spika, Zanzibar ni kisiwa kidogo sana na tatizo la umeme ambalo linatukabili linatusababishia uchumi wa nchi yetu kuweza kuzorota kwa namna moja au nyengine. Nahisi kwamba wakati sasa umefika kwa wizara husika kuweza kutengeneza utaratibu wa kutupatia umeme wa uhakika kwa Zanzibar kwa kuweza kutumia bahari ambayo imetuzunguka.

Mhe. Spika, baada ya kumaliza suala la umeme, sasa nije katika suala la maji. Mhe. Spika, suala la maji kwa Mkoa wetu wa Mjini na Magharibi bado ni tatizo. Tatizo hili Mhe. Spika, sisi tunashindwa kufahamu kuwa linatokea wapi na chanzo chake ni nini, kwa sababu wananchi wetu wanapopata matatizo ya maji katika maeneo husika, tunapokwenda katika Idara ya Maji kuonana na viongozi pamoja na baadhi ya watendaji, basi tatizo lile linaweza kutatuliwa kwa muda wa siku mbili au tatu, halafu baadae tatizo lile linarudia tena. Sasa tunashindwa kufahamu tatizo la maji katika mji wa Zanzibar linatokana na nini. Tuseme ni miundombinu au watendaji wenyewe, au mazalisho ya maji.

Ni ukweli usiofichika Mhe. Spika, kwamba mazalisho ya maji yamepungua, hilo tunalifahamu. Mazalisho ya maji yameondoka kutoka lita milioni 31 kwa saa hadi sasa tunakwenda kwenye lita za uzao milioni 5 mpaka 6 kwa saa. Tatizo hilo tunalielewa na tatizo hili linatokana na kiangazi pamoja na matatizo mengine ya miundombinu ambayo tunayo.

Kama hii haitoshi Mhe. Spika, wananchi wetu wanafika pahala sasa wanakuwa wanatushangaa na hawatuamini tena katika suala hili la maji, hususan pale wanapokaa baada ya wiki tatu au nne hawajapata maji, tunapokwenda katika idara au wizara husika siku mbili au tatu baadae wakapata wananchi maji siku mbili au tatu hawapati tena wanarudi tena katika matatizo yale yale. Kwa hivyo, tunaomba kufahamu hasa tatizo la maji linatokana na nini katika hiyo idara inayohusika.

Jengine Mhe. Spika, ni suala la uchakavu wa nyumba zetu za maendeleo. Zamani tunakumbuka tunapopatwa na matatizo katika nyumba zetu za maendeleo hizi, basi tulikuwa tunakwenda kule Idara ya Ujenzi, tukifika kule tunapata mafundi wanakuja kushughulikia zile nyumba na nyumba zinabaki katika hadhi yake nzuri na za kupendeza. Lakini kwa sasa Mhe. Spika, hizi nyumba zimekuwa chakavu na hazishughulikiwi tena.

Kuna hatari baada ya kipindi kifupi kuna baadhi ya varanda zitaanza kumong'onyoka pamoja na vile vyuma vilivyokuwa vimejengewa vikaanza kuleta athari kwa wakaazi wa nyumba hizi. Sasa sijui Mhe. Waziri anayehusika katika taasisi hii ana mpango gani juu ya hizi nyumba za maendeleo ambazo zamani zilikuwa zinafanyiwa ukarabati pamoja na matengenezo na sasa zimeachwa zinaendelea kuharibika zaidi.

Jengine Mhe. Spika, ni upatikanaji wa hati za umiliki wa ardhi kwa baadhi ya maeneo. Mwanzo kule nilikuwa nimelizungumzia hili. Kuna baadhi ya wananchi bado wanaendelea kulalama kupata hati zao, ziwe za nyumba au ardhi ambazo walikwisha kupewa na serikali toka wakati wa mzee Karume mwenyewe.

Mhe. Spika, jengine nataka kuchangia katika suala la ujenzi wa vikuta vya Forodhani. Mhe. Spika, katika miaka ya nyuma tulipokuwa tunafuatilia taarifa za Baraza hili, tulipata kueleweshwa kwamba kulikuwa utaratibu wa kuweza kuweka vikuta pembezoni mwa bahari kule Forodhani. Lakini cha kustaajabisha ni kwamba sasa muda umekuwa mrefu vikuta vile havijawekwa na pana athiri sana watoto wetu wanaokwenda kucheza katika maeneo yale. Kwa kupitia wizara husika tunaomba suala hili Mhe. Spika, liangaliwe kwa kulinda usalama wa watoto wetu kwenye maeneo ambayo wanacheza wanapokuwepo katika maeneo ya Forodhani.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, namalizia kwa barabara za ndani zilizokuwepo ndani ya jimbo letu. Mhe. Spika, watu wa Nungwi watazungumzia suala la barabara ambayo inatokea Kinazini kuelekea Nungwi unadhifu wake pamoja na umakini wake. Lakini kwa watu wa Kikwajuni watazungumzia suala la barabara zao za ndani.

Kwa wakati huu Mhe. Spika, wakati umefika sasa katika bajeti yetu inayokuja wana wa Kikwajuni nao waonekane kwa barabara zao za ndani. Kwani imekuwa ni kero kubwa na inawaudhi wananchi wanaokaa katika maeneo yale.

Baada ya michango hiyo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja pamoja na maelekezo ya kamati hii na pamoja na wananchi wa Jimbo la Kikwani, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi nachukua nafasi hii kukushukuru na kumpongeza kamanda Mshimba kwa kuleta ripoti yake ambayo ni nzuri na ambayo nadhani wajumbe wataiona kuwa iko makini.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda naomba nichangie katika maeneo matatu. Eneo la kwanza Mhe. Spika, ni huduma za uungaji wa umeme. Mhe. Spika, wimbi la uungaji wa umeme kiholela Zanzibar limeongezeka. Mafundi vishoka wanaendelea kuwaathiri wananchi wetu wanyonge. Ukienda pale shirikani Mhe. Spika, kila siku mafundi wake wanafanya operesheni na kutoa huduma za umeme majumbani kwa mita ambazo nina hakika zinapatikana shirikani.

Mhe. Spika, Zanzibar hakuna kiwanda cha mita, hakuna maduka ya binafsi ambayo yanauza mita. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ukifuatilia hasa utaona kwamba mita ambazo shirika wamezifelisha ndizo mita ambazo Wazanzibari wanyonge wanafungiwa na hatimaye wanaingia hasara sana.

Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa watu waliopata kadhia hiyo, lakini siumii katika hilo. Nimeumia kwamba nimekwenda kuwakuta Wazanzibari zaidi ya 60 wameathirika. Shirika ukiwauliza hii mita ni ya kutoka wapi. Wanakuambia hii mita ilikuwa ni yetu lakini haifai. Sasa kwa nini Wazanzibari wafungiwe mita ambazo ziko nje ya utaratibu.

Mhe. Spika, mimi ninavyoamini kwamba mafundi vishoka wanapata baraka kwa baadhi ya mafundi wa shirika. Lazima wizara ichukuwe hatua ya kuwadhibiti wataalamu wa shirika kutoa mita holela kuwafungia wanyonge. Mzanzibari kupata huduma ya umeme kwa shilingi 800,000/= halafu baadae ukamkatia, kisha akaanza tena hatua za mwanzo hiyo ni hatari kubwa. Mhe. Spika, mimi nasema kwamba suala hili ni zito na lazima serikali ilipigie vita.

Mhe. Spika, jengine ni suala la viwango vya gharama za uungwaji wa umeme. Ukifanya utafiti juu ya Wazanzibari wanaoomba huduma hii ya umeme bei zao zinakuwa ni tofauti sana, baina ya Unguja na Pemba na hata Unguja kwa Unguja. Kuna baadhi ya wananchi wetu wanapata bei kubwa na wengine wanapata bei ndogo katika masafa ambayo hayalingani. Naomba shirika kwa

kupitia wizara hii litusaidie kuwaokoa Wazanzibari ambao kwa kipindi hiki wanakabiliwa na hali ngumu ya maisha.

Jengine Mhe. Spika, ni huduma za mkopo wa uungwaji wa umeme. Shirika lilitangaza kwamba wanatoa huduma ya mkopo wa uungwaji wa umeme. Tunaomba kujua tu ni kwa kiasi gani Wazanzibari wanafaidika. Kwa sababu vijijini wale Wazanzibari wanyonge wengi wanahitaji huduma hii, lakini bado hawajapata huduma hii ya mkopo wa uungwaji wa umeme.

Suala jengine Mhe. Spika, ni Idara ya Leseni za Usafiri, niende moja kwa moja kwenye bei za usafiri wa magari hapa Zanzibar. Mhe. Spika, kila siku serikali imekuwa ikisema kwamba itadhibiti ongezeko la bei za abiria kiholela, lakini nadhani kwamba zoezi hili linashindikana. Wamekuwa wakizungumza sana na wamiliki wa dala dala, lakini bado Wazanzibari wanapata usumbufu na hasa wanafunzi wa Kizanzibari.

Mhe. Spika, leo asubuhi Morogoro madereva wamepandisha bei ya magari kutoka Shs.300/= mpaka Shs.500/=, jambo ambalo linawasababishia wanafunzi kupata usumbufu. Wanafunzi wameamua leo asubuhi kujipanga barabarani na kuvunja magari yote ya abiria. Mhe. Spika, nadhani wizara ijitahidi suala hili walidhibiti ili isije ikafikia hatua hizo za kula hasara kwa matajiri wetu wa magari.

Mhe. Spika, jengine ni suala zima la usafiri wa baharini. Zipo taarifa kwamba meli yetu ya MV Maendeleo baadhi ya siku husafiri kwa injini moja, jambo ambalo ni hatari kubwa. Vile vile kuna baadhi ya siku meli hii hufika Pemba saa tatu, kwa sababu inasafiri kwa injini moja. Naomba Mhe. Spika, wizara ituambie kama meli hii imeshindwa kusafiri kwa injini mbili, kwa nini wasipige marufuku. Kwa sababu kuna siku meli hii itasababisha majanga makubwa, kwa sababu ya kuvumiliana na kutoleana macho.

Jengine Mhe. Spika, ni suala zima la udhibiti wa magendo ya tiketi za abiria. Mhe. Spika, Wazanzibari ni wanyonge. Mzanzibari kumkatisha tiketi ya Shs. 18,000/= mpaka Shs.30,000/= ni hatari kubwa. Kwa nini serikali inashindwa kudhibiti bei ya tiketi za abiria. Jambo hili Mhe. Spika, linatufanya Wazanzibari, hata mimi kuamini kwamba tiketi za abiria ni sehemu ya mradi, haiwezekani kwamba serikali ishindwe kuzuia magendo ya tiketi wakati kuna utaratibu mzuri tu. Idadi ya abiria tunawajua, idadi ya vyombo ambavyo vinachukua abiria na uwezo wake tunajua. Lakini kwa nini tiketi za abiria zizuiliwe baadae Wazanzibari wauziwe kwa bei ya juu, jambo ambalo linasababisha unyonge mkubwa sana kwa abiria wetu. Mhe. Spika, idara lazima hapa iwajibike na ituambie kwa nini tiketi za abiria Unguja na Pemba zinapanda kiholela siku hadi siku bila ya udhibiti.

Mhe Spika, mwisho kabisa niende kwenye Idara ya Anga. Mimi niwapongeze kwa kumaliza ujenzi wa kifaa na hivi sasa wanaendelea na ujenzi *terminal* ya jengo jipya la abiria. Naomba kujua Mhe. Spika, labda ujenzi huu wa *canopy* ulifadhiliwa na nani, kwa sababu mwaka juzi tulipokuwa kwenye kamati ya PAC, walituambia ni fedha ya serikali ndio ambayo imejenga *canopy* ile. Hivi sasa idara hii hii inatuambia kuwa ni fedha za wafadhili. Sasa hebu tuambieni wizara ni fedha za nani, ni za serikali au za wafadhili.

Jengine Mhe. Spika, wametupa taarifa kwamba Idara ya Anga wamempa mwekezaji eneo la kiwanja kuweka *perking.* Naomba kujua ni mwekezaji gani na hivi kweli Mhe. Spika, hapa Zanzibar hatuna uwezo wa kujenga *perking* pale uwanja wa ndege, mpaka apatikane mzungu kutoka nje. Kwa hivyo Mhe. Spika, idara lazima itupatie majibu ili tuweze kuridhika.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, kama nitakukaribisha kwangu ukifika nyumbani kwangu ukumbini ukiona uchafu, basi chumbani na chooni hakuingiliki. Mhe. Spika, uwanja wa ndege nje ni pachafu na kuna mashimo mengi ambayo yanahatarisha wageni wetu. Hivi karibuni mzungu pale uwanja wa ndege wa Zanzibar alianguka kwa sababu ya mashimo. Nadhani Mhe. Spika, idara inakusanya fedha kwa hivyo wazibe vile viraka pale uwanja wa ndege, vyenginevyo ni aibu na itatusababishia mapato kupotea.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono kabisa hoja hii ya Mhe. Makame Mshimba kamanda wangu pamoja na wananchi wangu, ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi na mimi nikaweza kupata nafasi ya kuchangia mawili au matatu juu ya ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Makame Mshimba, Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na wajumbe wake wote kwa kuandaa ripoti nzuri, ambayo imegusa maeneo mbali mbali na taarifa mbali mbali, niwapongeze sana.

Mhe. Spika, kamati hii imepewa majukumu mazito na kwa sababu inasimamia wizara nzito ambazo zinagusa huduma za wananchi moja kwa moja. Mhe. Spika, mimi nitachangia maeneo mawili makubwa kwa sababu ya kuokoa muda. Pamoja na kwamba ripoti hii imesheheni mambo mengi ambayo yangehitaji kupata michango yetu.

Mhe. Spika, Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji, na Nishati imepewa majukumu mazito. Suala la kushughulikia ardhi ni suala zito, suala la

kushughulikia maji ndio tatizo kabisa, lakini hata suala la kushughulikia umeme nalo limekuwa tatizo. Kwa hivyo, nimpe pole sana rafiki yangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna kwa kupewa wizara hii nzito na kwa kweli anahitaji awe mstahamilivu sana kutoka kwetu na kwa sababu sisi tuna majukumu mazito ya kuwashughulikia wananchi. Majukumu aliyopewa ni majukumu yanayomgusa yeye moja kwa moja.

Kwa hivyo, mimi nitazungumzia kwanza suala la matatizo ya Mamlaka ya Maji yaani ZAWA. Kwa mujibu wa ripoti hii Mhe. Spika, Mwenyekiti, amezungumzia juu ya majukumu ya Shirika hili la ZAWA ambalo moja ni kutoa na kueneza usambazaji wa maji kwa uhakika nchini. Hilo ni moja kati ya jukumu lao.

Mhe. Spika, bado jukumu hili halijaweza kutekelezwa ipasavyo. Tunaamini wanajitahidi, lakini kama alivyozungumza Mhe. Mahmoud kwamba hatujui tatizo lao ni nini. Wananchi wetu bado wanasumbuka sana na upatikanaji wa huduma hii, pamoja na kwamba takwimu zao zinaonesha kwamba asilimia 80 ya wananchi wanaoishi mijini wanapata maji, sikubaliani na takwimu hizo. Kwa sababu mimi katika Jimbo langu la Magomeni kuna matatizo makubwa sana ya maji na nimeshawahi kufika kwa Mhe. Waziri mara kadhaa, lakini inaonekana bado ufumbuzi wa tatizo la maji katika Jimbo langu la Magomeni haujaweza kutatuliwa. Ndio maana inabidi kila linapoguswa suala hili, sisi kama wawakilishi wa wananchi ni lazima tulizungumze.

La kushangaza Mhe. Spika, kama alivyozungumza Mhe. Mahmoud kwamba utakuta pahala kuna siku maji yanatoka ya uhakika, lakini baada ya muda mkubwa unakuta maji hayapo.

Mhe. Spika, katika jimbo langu kuna mradi unaitwa Mradi wa SEMUSO, ambao ni mradi wa siku nyingi. Tokea ulipozimwa umeme wakati ule wa miezi mitatu, basi maji yalikuwa hayapatikani, lakini la kushangaza mpaka wananchi wakashangaa, juzi siku ile palipofanyika mkutano wa hadhara pale katika viwanja vya Kibanda Maiti, basi tangi lile la maji yalijaa mpaka yakamwagika. Wananchi wakauliza kuna nini kulikoni. Tangi ambalo zaidi ya tokeka ulipozimwa umeme kulikuwa hakuna maji. Lakini juzi limejaa maji. Baada ya kumalizika yale yaliyojazwa kwenye tangi tena ikawa ndio mwisho mpaka leo maji hayajaweza kupatikana.

Sasa hapa ndipo tunapofikia pahala tunajiuliza kuna tatizo gani. Kwa kweli Mhe. Waziri tuna tatizo la maji na hili linahitaji kushughulikiwa ipasavyo, ili tujuwe tatizo linalowakabili wananchi wetu la maji linatokana na nini.

Mhe. Spika, kuna bomba kubwa la nchi 8 ambalo limepita katika eneo langu, baada ya kumuomba Mhe. Rais mstaafu aliyepita kwamba hakuna *line* yoyote iliyoungwa kutoka katika mradi huu wa Japan ambalo limepita katika eneo langu. Kwa bahati nzuri Mhe. Rais aliyepita alitoa fedha kiasi cha Shs.25,000/= na kuwakabidhi watu wa Mamlaka ya Maji, likapitishwa bomba la inchi 8. Toka wakati huo bomba lile limetandikwa na lina maji sasa hivi, lakini Idara ya Mamlaka ya Maji imeshindwa kuyasambaza maji yale katika maeneo husika. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri tatizo hili analifahamu na mimi wajibu wangu kulizungumza kwamba bado hakujachukuliwa hatua zinazostahiki ya kuyasambaza yale maji kwa wananchi.

Kwa hivyo, mabilioni haya yaliyotajwa hapa ambayo yametolewa na wenzetu wa Japani, kwa kweli ni mabilioni mengi. Mhe. Spika, bilioni 032,063 inasikitisha kuona kwamba bado kuna matatizo ya maji katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi. *(Makofi)*

Suala jengine kwenye maeneo ya umeme kama alivyotangulia Mhe. Nassor Salim Ali kwa kweli amenifilisi. Kwa mfano, hivi sasa tunayo matatizo ya umeme katika eneo letu, lakini jambo la kushangaza ni kwamba serikali ilinunua majanareta 32 kwa ajili ya umeme wa dharura. Majanareta hayo yalizunduliwa na Mhe. Rais aliyemaliza muda wake na kwamba yatakuwa pale *standby* kwa ajili ya umeme wa dharura.

Kwa hivyo, jambo la kushangaza hivi sasa kumekuwa na mgao wa umeme na mgao huo wa umeme hautokani na ule wa Baraza, yaani ni mgao wetu sisi wenyewe wa ndani. Sasa wananchi wanajiuliza haya majanareta ya akiba ambayo tumeyaweka pale kwa umeme wa dharura yanafanyakazi gani. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, tunahitaji tuelezwe kama mabovu au hatuna uwezo wa kuyahudumia ama vipi, kwa sababu tunapofanya jambo wananchi wanaona na huwa wanatuuliza sisi Wawakilishi wao, lakini mara nyingi tunakuwa hatuna majibu. Kwa hiyo, tunataka tuelezwe haya majanareta 32 yaliyonunuliwa kwa ajili ya umeme wa dharura, sasa mpaka leo inafika pahala tunakwenda kwa mgao na yale yapo pale yanamatatizo gani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu hili suala la mgao wa umeme huu unaokwenda muda wa saa moja na nusu katika kile eneo utadumu kwa muda gani. Kwa kweli tumeambiwa mgao huu hautokani na tatizo lilioko kule Bara, yaani *TANESCO* na huu ni mgao wetu wa ndani. *(Makofi)*

Vile vile ripoti imezungumzia juu ya suala la umeme mbadala. Kwa kweli suala hili imekuwa ni hadith tu, tokea Baraza lililopita na mpaka hili

tunaelezwa kwamba Shirika la Umeme liko mbioni kutengeneza umeme mbadala, serikali itatumia umeme wa jua, mvua na mambo mengine. Lakini bado tatizo la umeme halijaweza kutatuliwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atakapokuja kufanya majumuisho atueleze nini mipango ya serikali katika kuhakikisha kwamba tunapata umeme mbadala badala ya huu uliopo hapa.

Kwa kweli tunavyo vianzio vingi, Mhe. Spika sisi wawakilishi wako au Wenyeviti wa Kamati katika awamu ile iliyopita tuliwahi kufanyiwa semina na ndugu zetu wale ama Norway au Sweden nimesahau kidogo. Sasa wao wamefanya *research* hapa kwetu Zanzibar na walisema kuna njia nne ambazo zinaweza kutusaidia kupata umeme, walisema kwamba umeme unaotokana na jua kwa mujibu wa vipimo pamoja na utafiti wao basi hapa unawezekana. *(Makofi)*

Vile vile walitueleza kwamba umeme unaotokana na nguvu za upepo. Kwa mfano, upepo unaovuma maeneo ya Kusini mwa Unguja, Makunduchi Jimboni kwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika Mhe. Haroun Ali Suleiman. Kwa kweli, walisema upepo upo mwingi tena wa kutosha, ambao unaweza kutoa umeme wa kutosha kwa ajili ya kusaidia Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia umeme ambao unatokana na takataka. Kwa hiyo, walitueleza kwamba zipo taka za kutosha zinazozalishwa mjini, basi zinaweza kutoa umeme wa kutosha kwa ajili ya Visiwa vyetu vya Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa upande wa umeme wa mawimbi ya bahari walitueleza hauna uhakika, kwa sababu nchi chache sana ndio zinazotumia umeme unaotokana na mawimbi ya bahari na haujawa na uhakika. Lakini hivi vianzio vyengine vya umeme vina uhakika na wamefanya *research* ya kutosha, isipokuwa walikuwa wanasubiri ridhaa ya serikali kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo. Sasa leo bado inaendelea kuwa ni hadith tu kwamba tutafanya hivi na vile na bado tunaendelea kupata matatizo katika masuala ya umeme.

Ukosefu wa umeme Mhe. Spika, unasababisha mambo mengi. Kwa mfano, viwanda vinapata matatizo, tunapotembelea maeneo ya viwanda kama vile Kiwanda cha *Drop of Zanzibar*, moja miongoni mwa matatizo yao ni kukatika kwa umeme na baadhi ya viwanda vyengine. Sasa tunapofikia pahala kwamba viwanda hivi haviwezi kwenda vizuri maana yake na huu uchumi wetu utakuwa hauko katika hali nzuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kweli wizara yake ni ngumu na amepewa majukumu mazito na yupo peke yake na anahitaji msaada wa kutosha, ili kumuwezesha haya majukumu yake aweze kutekeleza vizuri, kwa sababu wananchi wanahitaji sana huduma hizi tena ni muhimu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo na kutokana na muda, basi mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono hoja na Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, awaelezee wananchi wa Magomeni ni lini watapata maji ya uhakika na wao waishi vizuri kama watu wengine. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa mchango wangu. Waheshimiwa Wajumbe, kuna wachangiaji watatu waliomba baadaye baada ya kusema mwisho atakuwa Mhe. Salmin Awadh Salmin ambapo nataka niitetee kauli ile kutokana na mazingira yetu.

Kwa hivyo, niombe radhi sana Waheshimiwa Wajumbe wafuatao:-

1. Mhe. Asha Bakari Makame namuomba radhi sana,
2. Mhe. Salim Abdalla Hamad namuomba mno ndugu yangu anisaidie, kwa sababu mazingira yako magumu mno na
3. Mhe. Hassan Hamad Omar, nyote kwa pamoja nakuombeni radhi. *(Makofi)*

Sasa naomba twende kwa Waheshimiwa Mawaziri na nimkaribishe Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati naye atoe mchango wake kujaribu kufafanua kidogo baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe zilizotolewa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa muhtasari wa majibu ya maswali yaliyotolewa na Waheshimiwa Wawakilishi wakichangia waraka huu ambao umewasilishwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi).

Waheshimiwa Wajumbe waliochangia ni wanane naomba nisiwataje kwa kuhifadhi muda. Lakini michango mingi ilijikita katika masuala yale ambayo Mhe. Salmin Awadh Salmin aliyaita mazito, magumu tena ni muhimu. Kutokana na hali hiyo Mhe. Mjumbe ameonesha nia ya kunionea huruma kwa mzigo mzito niliopewa.

Mhe. Spika, kuna usemi unaosema “Mzigo mzito sasa hapewi tena Mnyamwezi anapewa Mtumbatu”. Kwa bahati mbaya mimi ni mmoja miongoni mwa hao

Watumbatu na mzigo huu nimekabidhiwa, lakini mzigo huu hautokuwa mzito kwa mashirikiano nitakayoyapata kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe wote. *(Makofi)*

Kwa kweli nakubali michango yote iliyotolewa ambayo imetolewa kwa umakini sana, michango ambayo imewagusa sana Waheshimiwa Wajumbe hawa kwa sababu wanawawakilishi watu wao.

Nianze na lile suala la *TANESCO* na hili limejadiliwa na Wajumbe wengi. Mhe. Spika, *TANESCO* kutupandishia bei ya umeme kutoka asilimia 21 hadi 168 kwa vigezo ambavyo havitambuliki, yaani ni maamuzi ya ajabu na hata mimi yanayona ya ajabu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe wametutaka tujitahidi kulisawazisha suala hili, kwa sababu deni linalimbikana na limekuwa kubwa. Kwa maana hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba kwanza hili deni sisi hatulikubali, kwa sababu sisi tunalipa asilimia 21 ambayo Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoshauri kwamba sote wawili, yaani Tanzania Bara na Zanzibar tulipe kiwango kimoja. Sasa wenzetu wamekuwa wakaidi kusikiliza hata maagizo ya Rais na sisi pia tunakuwa kidogo wakaidi kukubali kulipa madeni ya kiholela. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala hili tunalishughulikia na hivi karibuni Mkurugenzi akifuatana na wataalamu wake wamefanya mikutano kadhaa, mkutano wa mwisho ilikuwa wamepewa majukumu sasa *TANESCO* na *ZECO* kulimaliza suala hili na hatimaye lililetwe serikalini kwa maana ya serikali zote mbili. Nadhani tuwape muda kidogo ili waweze kulishughulikia na hatimaye tutapata kusawazishwa. *(Makofi)*

Jambo jengine ambalo lilitawala lilikuwa ni matumizi ya ardhi. Mhe. Spika, nakubali kabisa kwamba kuna migogoro mingi sana ya ardhi, pia ipo migogoro ya Mahakama ya Ardhi. Vile vile hoja za Wajumbe kwamba Mahakama hazitoshi, nazikubali, Mahakimu hawatoshi, nakubali.

Kwa hivyo, ninachoahidi ni kuwa tuko mbioni kulitatua kidogo kidogo kwa kadri ya uwezo utakavyoturuhusu, kulitatua tatizo la Mahakama kwa maana ya nyumba na *furniture*, pamoja na kushirikiana na Jaji Mkuu pia tutalitatua tatizo la kupatiwa Mahakimu.

Mhe. Spika, bahati nzuri sana hivi sasa vijana wetu wengi wamesoma taaluma hii ya sheria, hivi karibuni wameapishwa baadhi ya Mahakimu na tatizo hili nahakika baada ya muda si mrefu nalo tutalipunguza na wala hatuwezi kuliondosha kabisa, isipokuwa tutalipunguza. *(Makofi)*

Kuhusu deni la umeme *TANESCO* tayari nimeshalizungumza. Mhe. Ali Abdalla Ali alizungumzia kuhusu upimaji wa eneo la Nguruweni. Kwa kweli eneo hili lilipimwa si kwa ajili ya watu maalum wa eneo maalum, isipokuwa lilipimwa kwa ajili ya watu wenye kuhitaji maeneo ya kulima na wala sio maeneo ya kukaa.

Kwa hivyo, ikiwa tokea kupimwa bado halijatolewa Hati Miliki na halijagaiwa, basi nakubali kwamba tutalichukulia hatua za haraka na kulifuatilia suala hili na kujua limefika wapi na hatimaye tutekeleze yale ambayo Mhe. Mjumbe aliyotushauri.

Mhe. Spika, kabla sijasahau na ninakuomba uniruhusu katika suala hili la kupimwa kwa ardhi. Kwa kweli nimeanza kupokea barua mbali mbali za Waheshimiwa Wawakilishi wa sasa wanaomba viwanja vyao na wao wapewe. Kwa hiyo, nataka nitamke wazi kwamba wale ambao bado hawajaniletea, basi wanitelee kwa haraka, ili niorodheshe na kwenda kupima. Kwa maana hiyo, kwenye kikao kijacho cha Baraza la Wawakilishi Waheshimiwa Wajumbe hawa niwakabidhi maeneo yao ya kujenga kule Tunguu. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu mradi wa *ACRA*. Mhe. Spika, nataka nimthibitishie kwamba kazi iliyobakia ni ndogo sana na mradi huu tutaufungua mwezi wa Juni, ili watu wa maeneo yale aliyoyataja hawana maji, basi wayapate maji kwa ukamilifu.

Kuhusu umeme mbadala umezungumzwa sana. Mhe. Spika, nataka nizungumze suala hili kwa wale wote waliochangia masuala ya umeme mbadala. Kweli jambo hili limezungumzwa muda mrefu, lakini tukubali suala la umeme mbadala ni jambo la taaluma sana, yaani ni jambo linalotaka kufanyiwa utafiti wa kutosha. Kwa mfano, tunasikia ule utafiti uliofanywa kule Makunduchi kwa Unguja na Micheweni kwa Pemba, kuna mawimbi makubwa sana tena mazito yanayoweza kutoa umeme kwa kutumia mawimbi hayo.

Lakini bado hatujathibitisha *megawatts* ngapi mawimbi hayo yanaweza kutoa umeme unaotakiwa. Kwa kweli umeme tunaotumia sasa ni *megawatts* 45 mpaka 50 kiwango ambacho kimepita kile kiwango cha waya wetu unaotoa umeme Bara kutuletea Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, hivi sasa ni hatari kuendelea kutumia waya ule kwa kuzalisha umeme bila ya kupata umeme mbadala na hilo tunalikubali sote na tunalishughulikia kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Katika hali hii ya kutafuta umeme mbadala mpaka hivi sasa sehemu mbili tumeziona zinatupa tamaa, kwa sababu watafiti tuliwakabidhi kazi hizi

wanatuhakikishia na wametuthibitishia kwa ushahidi kwamba wanaweza kuzalisha *megawatts* 50 mpaka 100. Mhe. Spika, wataalam hao wanafanyakazi hiyo Oman, Dubai pamoja na Malaysia. Kwa hivyo, utafiti huu nadhani ndio tunaoutegemea sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi karibuni na wawekezaji wa aina hii wanaoweza kutuzalishia kwa kutumia jua, yaani *Solar Power megawatts* 50, pia tumezungumza na wanaoweza kutumia *gas megawatts* 50 mpaka 100. Sasa umeme wa vianzio hivi viwili vinatupa tamaa kubwa sana. *(Makofi)*

Pamoja na serikali kutukubalia maana mambo haya lazima yapite serikalini, Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, basi baada ya kutukubalia tutatoa taarifa kwamba sasa umeme mbadala umefika na muda si mrefu tutaanza kuutumia na kujilinda katika utegemezi wa umeme unaotoka *TANESCO* ambao upandaji wake sio ushukaji wake hautabiriki. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, nakuongeza dakika mbili.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakuomba uniongeze na dakika mbili nyengine, ili nimalize haraka.

Kuhusu suala la maji. Mhe. Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia kuhusu matatizo ya maji, kwa sababu ni mazito na sote yanatugusa kwani maji ni uhai.

Kwa kweli wapo waliochangia na kusema labda miundombinu, yaani mabomba mabovu yanavuja na kadhalika, ni sahihi kabisa, pia wapo waliochangia wakasema kuwa nadhani kima cha maji yamepungua, ni sahihi kabisa. Hayo ndio mambo mawili ambayo yanatutanza, kwa sababu tumeshatembelea sana na tumeshaumiza vichwa vyetu sana, lakini tulipofikia sio pabaya.

Mhe. Spika, *JICA* wamekuja na *proposal* ambayo tumeikubali kimsingi, isipokuwa ina sharti moja ambalo ningependa nilizungumze. Kwa kweli sharti lao na hata Balozi wa Japan alikuja juzi na nilionana naye, yaani ni sharti moja tu kwamba tulifika kulipia kiwango cha asilimia 40 cha maji na sasa kiwango kile kimeshuka kimefika asilimia 10.

Kwa hivyo, wanataka kile kiwango tukipandishe na kionekane kinapanda tena, ili waweze kuanzisha mradi wao wa kusambaza miundombinu ya maji na kuendelea na awamu ya pili ya kuongeza visiwa vya kuzalisha maji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hapa kuna kitendawili tunaanza na nini, tunaanza na kulipa au kupata maji. Sasa tumezungumza sana na wenzetu wa *JICA* pamoja na Japan

watukubalie, yaani watupe miundombinu na waanze miradi yao wanayotaka kutusaidia na tatizo la maji likiondoka basi wananchi watalipa maji. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wameondoka na kitendawili hivyo, kwamba tunakwenda kufikiria kwamba tuanze kwa kukupeni maji au muanze kutulipa sisi kwanza. Sasa hilo ni tatizo na *Inshallah* tutalisawazisha.

Mhe. Spika, mwisho kuhusu nyumba za Michenzani na kule Kengeja Pemba pamoja na nyumba nyengine zimechakaa sana. Kwa kweli suala hilo tumeshalisikia na limezungumzwa sana, Nyumba Block No. 2 na 4 hazipati maji na kwa nini nyengine zinapata na nyengine hazipati.

Vile vile suala hilo tumeshalisikia na tayari tumeshatuma watu kwa ajili ya kufanya tathmini ya marekebisho hayo, baada ya kupata hiyo tathmini basi tutaingiza kwenye bajeti yetu ili tupate fedha za kufanya marekebisho hayo.

Mwisho kabisa kuhusu michango yote iliyotolewa na Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwa kweli yote inazungumzia maji pamoja na hotuba ya Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi) pia nayo imezungumzia sana kuhusu maji. Mhe. Spika, nakubali kwamba tatizo la maji ni kubwa tena ni sugu na wala sitaki kuahidi kuwa mimi nitaliweza kulimaliza kwa haraka.

Lakini nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Spika, kwa miradi yetu ya maji ilioko njiani, juhudi za mafundi wetu na kadhalika, basi watustahamilie pamoja na kutuvumia na kweli tuko mbioni sana kulitatua tatizo la maji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa wale wanaochimba visima kila pahala kwa ajili ya kuondoshea wananchi wao matatizo ya maji, kwa upande mmoja nawapongeza, kwa sababu wanafanyakzi nzuri ya kuisaidia wizara yangu pamoja na serikali kwa jumla. Lakini nawaomba niwatahadharishe wakati wanapoamua kufanya hivyo, basi ni vyema watushauri maana wanaweka badala ya kupata maji wakapata virusi vinavyotokana na vinyesi, kwa sababu visima vinachimbwa mitaani na matatizo yake tutapata maradhi ya kipindupindu. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, basi naomba tushauriane wakati wa kuchimba visima, yaani wanapotaka kuchimba kisima tushauriane kama ni pahala pazuri au pana matatizo ama ikiwa matatizo ya maji ni makubwa. Kwa maana hiyo, tutawaruhusu ilihali tunafuatilia kuwatafutia dawa za kuua hivi viluwiluwi pamoja na vijidudu vinavyosababisha maradhi haya kwa kutiwa dawa kwenye visima vyao.

Mhe. Spika, baada ya majibu hayo naomba nikushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa ufafanuzi juu ya mambo adhimu kabisa, ambayo Wajumbe wa Baraza hili wamechangia kwenye Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi) pamoja na wajumbe wake wote, kwa kazi nzuri kabisa waliyoifanya wakati wa shughuli za kamati. Lakini zaidi namna walivyokuwa wazi katika kutoa maoni, maelekezo pamoja na ushauri wao kwa nia ya kujenga. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ripoti hii imechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 9. Lakini miongoni mwa wajumbe hao walioigusa moja kwa moja Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni wajumbe 6. Kwa kweli nataka niwashukuru sana, naamini kama Mhe. Spika, ungewapa nafasi ya kuwapa muda basi wangesema zaidi. Kutokana na wakati wajumbe hao 6 sitowataja, lakini naomba kupitia kwako Mhe. Spika, wachukue shukurani zangu za dhati pamoja na wizara yangu.

Kwa hivyo, nianze na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Mwenyekiti wa Kamati) ambaye amezungumzia kuhusu Shirika la Meli kuhuwishwa na kupata meli mpya, pia alielezea na suala la kukopa meli au kuchukua mkopo wa kununua meli mpya.

Sasa kwa kifupi tu Mhe. Spika, hivi juzi tarehe 29 Machi, 2011 wakati nilipokuwa nikijibu swali la nyongeza lililotokana na swali Nam. 23, basi namuomba Mhe. Mwenyekiti pamoja na wajumbe wengine kupitia kwako Mhe. Spika, waende kwenye hansard ya tarehe hii na watapa ufafanuzi kama ambao ningetaka kuutoa leo.

Mhe. Spika, kuhusu bandari ni kweli kuna mrundi, lakini ni mrundiko wa makontena kama unaangalia Bandari ya Zanzibar, nataka nimueleze Mhe. Mjumbe, kwamba juzi katika mahusiano haya ya Wizara za SMT na SMZ tulikuwa na Wizara ya Uchukuzi, basi walikuwa Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja Wakurugenzi wake na tuliwapa nafasi ya kutembelea kwenye bandari yetu.

Kwa hivyo, kwenye majumuisho ya mkutano wetu walisema wao wamenyanyua mikono na wasingeweza katika kipindi hiki kushindana na ile *efficiency* na Bandari ya Zanzibar. Mhe. Spika, kwa kweli wao makonteni

walikuwa wanachukua siku 23 tokea kupakuliwa mpaka kutolewa, sasa wamejitahidi kwa nguvu zao zote hadi sasa wametoka siku 23 mpaka 13.

Lakini kwa upande wetu sisi tunao uwezo wa kulitoa kontena katika kipindi kisichozidi siku tatu, labda iwe wenye makontena yale hawajakamilisha nyaraka, ikiwa umekamilisha nyaraka zao, basi Mhe. Spika nakuhakikishia ni siku moja, mbili na wala haizidi siku tatu. Kwa hivyo, mrundikano upo kwa muono wa Mwenyekiti, lakini ukilinganisha na Bandari ya Dar-es-Salaam sisi tuko mbali sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la Bandari ya Mpigaduri juhudi za serikali ni kujenga bandari mpya tena ya kisasa ambayo inayoitwa *Hub Port*. Kwa kweli ni bandari ambayo mizigo inaletwa pale na wengine wanachukua, wengine wanaweka kwa ajili ya kusafirisha nchi nyengine na juhudi zinaendelea. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hapa kidogo nataka nitofautiane na Mhe. Mwenyekiti kwamba SMT imekataa kutoa au kudhamini huu mkopo wa *Exim Bank*. Mhe. Spika, bado hatujafika huko kuiomba serikali au kudhamini mkopo kwa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, naomba nifanye marekebisho hayo tu. Kwa maana hiyo, juhudi zinaendelea na ninaamini kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watadhamini kabisa mkopo huu kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar na hiyo ndio imani yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu suala la Hati Miliki kwa bandari na minara. Kwa kweli hilo tutalishughulikia kwa nguvu zetu zote na ni agizo kabisa la serikali. Kwa hivyo, tunatekeleza agizo la serikali katika kufanikisha masuala haya.

Vile vile kuhusu msamaha wa kodi kwa vifaa vya ujenzi wa *Airport* na suala hili tumeshazungumza na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na tumefika mbali. Kwa hivyo, naomba nilihakikishie Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba hadi sasa hatujakwama mahala na wajenzi wenyewe wametuthibitishia kuwa wanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, kuhusu suala la barabara na fidia za vipando na kwamba serikali katika bajeti zake au kwenye kuomba mikopo wangeingiza *component* hii ya fidia. Kwa kweli mikopo ina masharti yake, lakini moja katika masharti ambayo tumekumbana nayo ni kwamba suala la fidia kwa mali na vipando vyengine suala la serikali, kwa hivyo kwanza ukubali hilo. Kwa hivyo hili kwa kuwa tunajua ni sharti hatungeweza kuwaambieni jamani na hili lichukueni hawatokubali, na hadi sasa serikali haijakwama kiasi hicho wamejitahidi kwa mujibu wa bajeti yetu na uwezo tumeanza kulipa fidia na sera ya serikali hatutomvunjia mtu yoyote nyumba yake kabla hatujamlipa.

Mhe. Spika, lakini kwa vipando tunawaomba sana wananchi wajue kwamba kama ni barabara ni kwa ajili ya naendeleo yao na hakuna mtu ambae hatalipwa, lini watalipwa hili ni uwezo wa serikali kuhusu majumba hatuwezi kuvunja kabla ya mwenye nyumba kulipwa fidia iliyokisiwa na serikali.

Mhe. Spika, suala la kumalizika miradi ya barabara kwa wakati hili mimi naliita suala mtambuko linahusu mjengewa, mjenzi na ambae amedhamini mkopo ule, ama ni mkopo au msaada lakini hawa watatu kama watakubaliana vizuri hakuna mradi ambao ungechelewa. Lakini matatizo yanakuja hayaepukiki mfano serikali inatakiwa iondoe mabomba ya maji kabla ya barabara au *bulldozer* kupita, iondowe nyaya za umeme na mambo mengine, hatungejenga barabara tukakuta sehemu kubwa ya jamii haina umeme kwa sababu ya barabara au tukakuta sehemu kubwa haina maji kwa sababu ya barabara, kwa hivyo kwanza kinachofanywa ni serikali kupata fedha zakuondoa vile vikwazo kabla ya *bulldozer* kuingia kwenye barabara, hivyo ndivyo tunavyofanya.

Sasa kama *contractor* mmetia saini aanze kesho kutwa au unampa *site* keshokutwa lakini unakuta kwamba kuna nyumba pengine haijalipwa, kuna bomba za maji hazijaondolewa, kuna waya za umeme hazijaondolewa, *contractor* yule atabaki na atakuwa anasubiri kama mwezi mmoja au miwili au mitatu mpaka ahakikishe kwamba kila kitu hakipo ndio atiye *bulldozer*, mfano mzuri ni *terminal building*. Hiyo imechukua karibu miezi minne *contractor* yupo lakini kuna majumba hayawezi kuvunjwa bila ya kulipa na serikali uwezo wake ni huo, mpaka tulipopata pesa 1.6 bilioni shilingi tukawalipa na ndipo *contractor* mchina alipoanza kujenga na anakwenda kwa spidi kubwa sana. Pamoja na kwama sasa hivi ni miezi minne lakini amefanya mpaka sasa hivi iwe amechelewa miezi miwili, naamini kwamba jengo hili litamalizika hata kabla ya wakati ishaalla.

Mhe. Spika, suala la *ZANTEL* matatizo yaliyopo limeelezwa vizuri hukuwepo lakini aliyekuwepo ni kama wewe, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alipata ufafanuzi na naomba wajumbe kama ambavyo juzi tulikuwa na kazi kubwa sana hapa na kwa Baraza hili ilikuwa ni historia haijawahi kutokea lakini limetokea, naamini kwamba maamuzi tuliyofanya siku ile ndio maamuzi ya baraza hili. Kwa hivyo namuomba Mjumbe kwamba maamuzi yaliyotolewa hapa ndio hayo hayo, serikali itakaa itaangalia mimi nasema ni matatizi sio mgogoro baina ya *ZANTEL*, *TIGO* na Manispaa hakuna lisilowezekana tutalitatua na kila mtu atapata haki yake.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wanaridhika na yale ambayo tayari umeyajibu kwa hivyo mengine yapokee tu kwamba utayafanyia kazi ndio wanachosema hao.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe kabla sijamwita Mwenyekiti nichukue nafasi hii kuwashukuru Mawaziri wetu wawili ambao wanahusiana na kamati hii, ule muda wa kunisaidia kuendesha kikao umefika sasa tuna ripoti mbili bado lakini naamini zitachukua muda mfupi tu kumaliza, ripoti ambazo tuzimalize halafu tena tumuombe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aje atufungie mkutano wetu huu.

Sasa muda wetu ni saa saba kasoro dakika tano na tunahitaji jioni ili tusije tukatoka wakati dhiki tuwe na ripoti moja halafu tumuombe Mhe. Makamo wa pili wa Rais, niwaombe basi waheshimiwa wajumbe kwa utaratibu tuliojiwekea kwa kumuomba Mhe. Waziri, Mhe. Mwanasheria Mkuu ili kutoa hoja ya kuongeza muda ya kumaliza ripoti hii na kwenda ripoti ijayo ambayo naamini sio ndefu kama hizi nyengine ili tuweze kumaliza jioni tuwe na ripoti ya mdhibiti peke yake kwa sababu ile ni pana, ile inagusa karibu wizara zote.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja ya kwamba kwa sababu ya shughuli ambazo zimepangwa kwa ajili ya kikao hiki hazijakamilika na kwa sababu muda wa kikao unakaribia kumalizika, naomba baraza hili tukufu liweke kando kanuni ya muda ili tupate kumaliza ripoti iliyobakia ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Nihoji basi wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi (Mhe. Makame Mshimba Mbarouk): Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya haraka haraka kama ulivyonisifu na mimi nitakwenda na sifa ile ile.

Mhe. Spika, kwanza nawashukuru wachangiaji wametusaidia sana, wamechangia vizuri sana na majina ya waheshimiwa waliochangia niseme kwa haraka ni;-

1) Mhe. Subeit Khamis Faki
2) Mhe. Rashid Seif Suleiman
3) Mhe. Ali Abdalla Ali
4) Mhe. Nassor Salim Ali
5) Mhe. Mussa Ali Hassan
6) Mhe. Mahammoud Moh'd Mussa
7) Mhe. Hija Hassan Hija
8) Mhe. Salmin Awadh Salmin

Mhe. Spika, kwanza nimsifu Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu huyu tunampa jina la Magufuli kwa sababu ni hodari sana ukimwambia jambo basi ameshafahamu na kukupa utaalam mzuri hongera sana Mheshimiwa.

Lakini kwa kumalizia la mwisho tunasisitiza sana Kamati katika suala la Pwani Mchangani Mhe. Waziri alikokuwa akitaka kutoa hati akipenda atatwida kama Mwenyekiti, hakupenda ana hiyari yake mwenyewe. Lakini suala hili bado nalisisitiza kwamba wapewe wale wahusika na waliokubalika kwenye ile tume ndio ambao wapewe hati zao, vyenginevyo vyovyote tutakuja kupigishana kelele.

Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wanaokubali kipokea ripoti hii wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwwa na kukubaliwa)

Mhe. Spika: ripoti ifanyiwe kazi na serikali ili kutekeleza yale yaliyomo.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: (Mhe. Ali Abdalla Ali): Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana tena katika shughuli hii ya kawaida ya kila mwaka ya kuripoti utendaji wa Serikali mbele ya Baraza lako tukufu kwa mujibu wa Kanuni ya 106 (14) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar, Toleo la 2011.

Aidha, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuniruhusu kuwasilisha ripoti hii kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipompongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa kufuatilia na kusimamia vyema utendaji wa Serikali. Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imefarajika sana kwa Kiongozi huyu alipotembelea jengo la Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali baada ya kuombwa na Kamati hii kufanya hivyo. Kitendo hicho kinadhihirisha wazi kuwa Serikali inazithamini juhudi na maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili.

Mhe. Spika, napenda vile vile niwashukuru Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wao wote ambao kwa namna moja au nyengine walishirikiana na Kamati yetu tulipokuwa tukitekeleza wajibu wetu kama ilivyo katika kifungu cha 111 cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar, Toleo la mwaka 2011.

Mhe. Spika, kwa kweli nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonesha katika kufuatilia na kuhoji kwa kina utendaji wa shughuli za Serikali na kutoa maoni yao yaliyokuwa na shabaha ya kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji katika Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati yetu kwa kuwataja kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mussa Khamis Silima	-	Mjumbe
6.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
8.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
9.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
10.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	-	Katibu

Mhe. Spika, kabla ya kuwasilisha ripoti yetu naomba kufanya marekebisho kwenye ukurasa wa 140 wa kitabu cha Ripoti za Kamati katika kipengele namba 3 kinachohusiana na changamoto za Chuo cha Utumishi wa Umma. Mhe. Spika, tunaomba kipengele hicho kisomeke kama ifuatavyo: Kwa kuwa watumishi wengi wa Serikali hawana sifa za kujiunga na vyuo, na kwa kuwa Chuo cha Utawala wa Umma kimeanzishwa kutoa taaluma zaidi kwa watumishi wa umma, na kwa kuwa Serikali hutoa nyongeza kwa watumishi

wanaohitimu mafunzo ya kuanzia miezi tisa. Kamati inaishauri Serikali kutoa nyongeza kwa watumishi wanaohitimu kozi kuanzia miezi sita, ili kuwashajihisha watumishi hawa kujiunga na chuo hicho, sambamba na kupata taaluma zaidi.

Mhe. Spika, kama inavyofahamika, Kamati hii imepewa mamlaka ya kuwa msimamizi wa jumla ya Wizara mbili za Serikali zikihusisha pamoja na Vitengo na Idara zao zote. Wizara hizo ni kama zifuatavyo:

- Wizara ya Katiba na Sheria.

- Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kimsingi, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imeridhika kwa kiasi na utendaji wa Serikali. Hata hivyo, inahisi bado jitihada zinahitajika kuchukuliwa na Serikali ili kukuza ufanisi wa kiutendaji, kuongeza ustawi wa wananchi na kuimarisha kasi ya maendeleo endelevu katika nchi kwa ujumla.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Mhe. Spika, Wizara hii kwa kupitia Taasisi na Vitengo vyake mbalimbali imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:

MAHKAMA

Mhe. Spika, Kamati yetu inaipongeza Mahkama kwa kuendelea kuzifanyia matengenezo makubwa na madogo Mahkama mbali mbali za Unguja na Pemba. Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo kwa huzuni napenda kutamka kuwa bado baadhi ya majengo ya Mahkama ni mabovu sana, ijapokuwa Serikali inayafanyia matengenezo majengo hayo mara kwa mara. Mhe. Spika, unapoyaona majengo hayo na ukizingatia uzito wa majukumu yanayotekelezwa humo basi machozi yatakutoka. Kutokana na kadhia hiyo, Kamati inaishauri Serikali izidishe bidii katika kutekeleza hili ikiwa ni pamoja na kuiongezea fedha Mahkama kwenye eneo la matengenezo ya majengo.

Mhe. Spika, Kamati yetu imebaini kuwa Msimamizi Mkuu wa Mahkama ambaye ni Jaji Mkuu hazitembelei Taasisi zake hizo, jambo ambalo ni kinyume na misingi ya uongozi. Ili kuleta ufanisi mzuri unaotakiwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inamuomba Kiongozi huyo kutekeleza hili, kwani linaweza kusaidia kujua mafanikio na changamoto mbali mbali zinazozikabili Taasisi husika. Sambamba na hilo suala hili litawatia moyo na hamasa watendaji na kujiona kuwa wana kiongozi ambaye anathamini juhudi zao wanazozichukua. Aidha, litasaidia kutatua na kuchukuliwa hatua changamoto zinazojitokeza

mapema iwezekanavyo kabla athari haijawa kubwa. Kamati inashauri hili ili kuheshimu na kuyafanyia kazi maneno ya Wahenga yasemayo "Usipoziba ufa utajenga ukuta".

Mhe. Spika, tunawaomba Wasimamizi Wakuu wa Mahkama wathamini juhudi za Serikali kwa kusimamia vyema masuala ya usafi wa majengo haya. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya majengo ya Mahkama ni machafu ingawa yalijengwa au yalifanyiwa matengenezo makubwa. Sambamba na hilo Kamati inaishauri Mahkama kuwa makini inapopitisha michoro ya ramani ya majengo yao, kwani imegundulika kuwa takribani majengo mengi ya Mahkama hayana ghala (stoo) la kuhifadhia vielelezo na kama lipo ni ndogo sana. Kamati inashauri hili baada ya kuona uhifadhi mbaya wa vielelezo katika Mahkama zetu kitu ambacho ni muhimu katika kuendesha kesi.

Mhe. Spika, Kamati yetu pia, inaishauri Mahkama kutofautisha fani ya Sheria na Utawala kwa kuwa kila fani ina misingi yake. Tunashauri hili baada ya kugundua kuwa Hakimu Dhamana "*Magistrate Incharge*" hufanya pia kazi za utawala, kitendo ambacho kinamuongezea mzigo, kwani tumebaini kuwa hushindwa kusimamia vyema majukumu mawili haya ipasavyo. Hivyo, ili kupata ufanisi unaotakiwa Kamati inashauri kuajiriwa mtu mwenye fani ya utawala katika Mahakama zetu na kutomshirikisha Hakimu Dhamana kwenye masuala mawili.

AFISI YA MWANASHERIA MKUU

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Afisi hii kwa kuendelea kuandika Miswada ya Sheria na hatimae kuiwasilisha kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchapisha katika Gazeti Rasmi la Serikali. Hata hivyo, Afisi hii inakabiliwa na changamoto ya kushindwa kuchapisha Miswada hiyo kama ilivyoelezwa na Kanuni ya 78(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar, Toleo la 2011. Katika kufanikisha hili tunaishauri Serikali kuandaa ratiba maalum itakayoonesha ni Miswada ipi itajadiliwa katika mwaka wa fedha husika na katika Mkutano upi wa Baraza la Wawakilishi ili maandalizi ya Miswada hiyo yafanyike mapemaiwezekanavyo. Ama kufuata utaratibu wa Bunge wa Mswada Kusomwa Mara ya Kwanza na kuwasilishwa katika Kikao kijacho.

AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Mhe. Spika, Kamati yetu imeridhishwa sana na utendaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Pamoja na utendaji mzuri huo Afisi hii bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo ni busara zikachukuliwa hatua za haraka, ili Afisi iweze kuendelea vyema kusimamia uendeshaji wa mashtaka

ili haki itendeke. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:- Kutokuwepo maabara yenye vifaa vya kutosha kwa ajili ya uchunguzi wa kikemia. Mhe. Spika, katika kufuatilia hili Kamati yetu ililazimika kuitembelea Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ingawa Afisi hii ipo chini ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, tuliamua kufanya hivyo kwa kuwa Afisi hii ni miongoni mwa Mdau mkubwa wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuhusiana na makosa ya madawa ya kulevya. Hivyo, tukahisi ni vyema kuona jinsi Afisi ya Mkemia inavyotekeleza majukumu yake. Mhe. Spika, kwa ujumla tulisikitishwa sana na hali ngumu ya kiutendaji tuliyoelezwa Afisini hapo. Ili kuiweka Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika mazingira bora na yanayotakiwa Kimataifa, Kamati inaishauri Serikali kuipatia jengo na vifaa vya kisasa Afisi hii muhimu ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya kesi ushahidi wake hupatikana kwa tabu, Kamati inaishauri Mahkama inapofanya uteuzi wa Majaji na Mahakimu izingatie pia uendeshaji wa kesi ili haki itendeke. Kwani imebanika kuwa baadhi ya kesi hufa kutokana na uteuzi huo baada ya kesi hiyo kupangiwa Hakimu mwengine na mshtakiwa anapoamua kesi yake kuanza upya.

Mhe. Spika**,** changamoto nyengine inayoikabili Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni ukosefu wa vitendea kazi vinavyohusiana na makosa ya jinai kama vile Mashine ya *DNA* limekuwa ni tatizo kubwa hususani katika uchunguzi wa kesi zinazohusiana na makosa ya ubakaji na ujauzito kwa watoto wadogo. Kwa sasa ni vigumu sana kuthibitisha makosa ya namna hiyo kama hakuna ushahidi wa moja kwa moja wa kumuhusisha mtuhumiwa. Kutokana na umuhimu wa chombo hiki sambamba na kuona haki inatendeka, Kamati inaishauri Serikali ama kutenga fedha au kutafuta Washirika wa Maendeleo ili kufanikisha hili.
Mhe. Spika, tunashauri hili kwa kuwa hivi sasa makosa ya aina hii yameshamiri nchini kwetu, kwa kuwa washitakiwa wengi hubainika kuwa hawana makosa wala hatia.
Mhe. Spika, imebainika kuwa kuna ongozeko kubwa la kesi za ubakaji hususan katika Mkoa wa Kaskazini – Unguja. Kutokana na ongezeko hilo Kamati yetu inahisi ipo haja kwa Serikali kufanya uchunguzi wa kina ili kujua ni sababu gani zinazopelekea kuongezeka kwa makosa hayo pamoja na kutafuta mbinu bora za kutokomeza makosa haya.

AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, tunaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na Afisi hii ikiwa ni pamoja na usajili wa nyaraka mbali mbali. Hata hivyo, Afisi ya Mrajis Mkuu

wa Serikali inakabiliwa na changamoto mbali mbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo;-

Kwa kuwa nyaraka zinazosajiliwa Afisini hapo zimefanyiwa *"binding"* tangu Mapinduzi na baada ya Mapinduzi nyaraka hazijafanyiwa tena *"binding"* na nyaraka hizo kuanza kuharibika kutokana na sababu mbali mbali. Kamati yetu inaishauri Serikali kwa mara nyengine tena kutenga fedha maalum kwa ajili ya kazi hiyo. Sambamba na kukiweka chumba kinachohifadhiwa nyaraka hizi katika hali au mazingira yanayotakiwa, ikiwa ni pamoja na kuweka vipoza hewa vya kutosha ili kulinda uhalisia wa nyaraka hizo, kwani chumba kinachotumika hivi sasa hakipo kwenye hali nzuri wala hakina kipozahewa.

Mhe. Spika, kwa kuwa imebainika kuwa baadhi ya wananchi hughushi nyaraka mbali mbali, Kamati inaishauri Serikali kuziingiza nyaraka zote kwenye mfumo wa *"digital"* ili kuondosha kabisa tatizo hili. Aidha, Kamati inashauri kuchukuliwa hatua zinazostahili kwa wale wote wanaobainika kushiriki kwa namna moja au nyengine katika kughushi nyaraka za serikali.

Mhe. Spika, ingawa Afisi ya Mrajis imehamia kwenye jengo lililokuwa Benki ya Watu wa Zanzibar – *PBZ* hapo Forodhani, bado Afisi hii inakabiliwa na uhaba wa nafasi. Kamati iligundua baadhi ya Watendaji wa Afisi wanafanya kazi kwenye njia za kupita (*corridors*). Kwa kuwa Afisi hii imepatiwa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa jengo huko Mazizini, na kwa kuwa fedha za kodi za eneo lililokuwa jengo la Afisi hii zitatumika pia kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la Afisi ya Mrajis, Kamati inaishauri Serikali kuwaingizia fedha mapema iwezekanavyo ili lengo lililokusudiwa litekelezwe huo uende vyema.

Mhe. Spika, pamoja na hayo Kamati inaishauri Serikali kuteua Maafisa maalum Mikoani na Wilayani watakaosimamia moja kwa moja masuala ya usajili. Kamati inashauri hili baada ya kugundua kuwa katika maeneo haya hakuna maafisa wanaosimamia masuala hayo na badala yake kazi hii hufanywa na Watumishi wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya, jambo ambalo hupelekea usumbufu mkubwa kwa wananchi.

AFISI YA HAKIMILIKI

Mhe. Spika, Kamati yetu inaipongeza Afisi ya Hakimiliki kwa kusimamia vyema haki za Wasanii wetu hapa nchini. Pamoja na juhudi hizo zinazochukuliwa na Afisi hii inakabiliwa na baadhi ya changamoto kama zifuatazo;-

Ufinyu wa nafasi katika jengo; Afisi haina nafasi ya kutosha, jambo ambalo hupunguza ufanisi na utendaji bora wa kazi. Kutokana na hilo tunashauri

kutafutwa sehemu mbadala ili Watendaji wa Afisi hii watekeleze majukumu yao bila usumbufu wowote.

Uhaba wa Watendaji; Mhe. Spika, Afisi ina Watendaji saba tu, kati yao Maafisa ni watano na wawili ni Watendaji wa kazi za chini. Ili kuimarisha utendaji wa Afisi hii Kamati inaishauri Serikali kuiruhusu Wizara husika kuajiri Watendaji zaidi hususan kwa upande wa Pemba. Tunashauri hili kwa kuwa hivi sasa hakuna Mtendaji hata mmoja katika Afisi ya Pemba. Hili ni kutokana na kuwa Afisa aliyekuwepo ni mmoja tu na kwa kipindi hiki yupo masomoni, na Afisi haina matumaini ya kufanya kazi tena na Mtendaji huyu kwa kuwa kozi anayosomea haihusiani na shughuli huzo kwa hivyo hatutegemei kumpata tena.

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

Mhe. Spika, tumepokea taarifa kuhusiana shughuli zilizotekelezwa na Kamisheni kwa kipindi cha Julai, 2010 hadi Februari, 2011. Mhe. Spika, Kamisheni hii imetekeleza malengo yake iliyojipangia kwa ufanisi mkubwa. Hata hivyo, inakabiliwa na changamoto mbali mbali, baadhi ya chanagamoto hizo ni kama zifuatazo;- Mhe. Spika, ingawa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imehamia kwenye jengo moja na Afisi ya Mrajis bado jengo hilo linakabiliwa na matatizo kadhaa. Miongoni mwa matatizo hayo ni kama yafuatayo;-

- Chumba cha kuhifadhia nyaraka za Wakfu hakina vipoza hewa jambo ambalo linaweza kusababisha nyaraka hizo kuharibika.

- Jengo halina maji, hivyo, Kamisheni hulazimika kununua maji ambayo kwa wiki hugharimu Tsh. 70,000/-. Kutokana na ufinyu wa Ruzuku inayopatiwa na ufinyu wa mapato inayokusanya gharama hizi ni mzigo mkubwa kwa Kamisheni. Aidha, Kamati imewashauri Wahusika kulitafutia ufumbuzi tatizo la kumwagika maji ovyo Afisini hapo kwani yanaweza kuathiri nyaraka zetu kuingia kwenye uharibifu.

- Uhaba wa nafasi. Kamati iligundua baadhi ya Watendaji wa Afisi wanafanya kazi kwenye njia za kupita *(corridors).* Mhe. Spika, kwa kuwa Afisi hii ilitakiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* kutafuta eneo la biashara kwa ajili ya ujenzi wa Afisi, Kamati inaishauri Serikali kuitafutia Kamisheni eneo hilo ili iweze kupata msaada huo kwa lengo la kutatua tatizo hilo.

- Kwa kuwa baadhi ya vifaa kama vile meza za kuandikia zimeshindwa kuingia kwenye vyumba vya jengo hilo kutokana na udogo wa

vyumba hivyo, na kupelekea baadhi ya Watendaji kulazimika kukaa na kufanya shughuli zao kwenye mabusati. Tunaishauri Serikali kuipatia fedha Kamisheni haraka iwezekanavyo ili inunue vifaa hivyo, na fedha zitakazopatikana baada ya mauzo ya meza hizo ziwasilishwe Serikalini ikiwa ni marejesho ya matumizi yaliyofanyika.

Mhe. Spika, changamoto nyengine inayoikabili Kamisheni ni Wapangaji wake kutokulipa kodi. Kutokana na kadhia hiyo, Kamati inawaomba Wapangaji wa Mali za Wakfu wakiwemo Watu Binafsi na Taasisi za Serikali kulipa viwango vya kodi kwa mujibu wa Sheria Nam. 2/2007. Aidha, tunaomba jamii na taasisi mbali mbali kuondokana na dhana kuwa mali ya wakfu ni mali ya serikali, ili kuepusha dhima mbele ya Mwenyezi Mungu huko twendako.

Mhe. Spika, sambamba na hayo Kamisheni pia inakabiliwa na tatizo sugu la usafiri kwa Unguja na Pemba. Kamati inaishauri serikali ulipatia usafiri kamisheni ili iweze kutekeleza kamisheni yake ipasavyo.

Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora

Mhe. Spika, Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ni miongoni mwa taasisi mpya zilizoundwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010.

Lengo la kuanzishwa wizara hii ni pamoja na mambo mengine, kuratibu na kusimamia utendaji wa utumishi wa serikali katika kuhudumia wananchi, sambamba na kuimarisha utawala bora Zanzibar.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba ya Sheria na Utawala, inapongeza kwa dhati serikali ya awamu ya saba kwa kuanzisha wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na kupongeza pongezi hizo tunaomba watumishi wa wizara kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na serikali. Wizara hii katika kipindi cha mwezi Julai 2010, February 2011, kwa kupitia Idara na Vitengo vyake mbali mbali imetekeleza mambo yafuatayo.

Idara ya Utumishi wa Umma

Kamati yetu inaipongeza Idara hii pamoja na mambo mengine kwa kusimamia vyema utendaji warasimu ya Mswada wa Sheria ya Utumishi wa Umma ambao hivi sasa ishapitishwa na Baraza lako tukufu la Wawakilishi Zanzibar katika mkutano wa pili.

Mhe. Spika, tunatoa pongezi hizi kwani kutakuwa na sheria inayosimamia utumishi wa Umma Zanzibar. Jambo ambalo litawajengea watumishi hao kutekeleza wajibu wao kwea moyo mkunjufu na uwadilifu mkubwa.

Aidha Idara ya Utumishi Serikali imekamilisha zoezi la utayarishaji wa miundo ya Utumishi *(Scheme of Service)* Serikali ambapo jumla ya miundo 50 yenye jumla ya kada 138 imetayarishwa. Miundo hiyo inazingatia majukumu yanayotekelezwa na watumishi kwa kila Wizara na tayari yamewasilishwa katika Wizara na serikali kwa ajili ya kupata maoni ya wadau.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada hizo kubwa zilizochukuliwa na Idara hii kukamilisha utayarishaji wa miundo ya utumishi, baadhi ya wizara zimeshindwa kuzithamini juhudi hizo kwani hadi hivi sasa hazijatoa maoni kutoa mapendekezo katika rasimu ya muundo wa utumishi katika Wizara zao.

Kamati inaiyomba kila wizara kuwasilisha maoni hayo ya Idara husika ili kuepuka malalamiko yasiyo ya lazima. Pamoja na uendelezaji wa kazi za wananchi walio chini ya wizara hiyo. Kamati inashauri hili kwa kuwa wizara ndio inayojua mahitaji halisi ya watumishi wake.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka kabla ya Wizara hii mpya hivyo inakabiliwa na ukosefu wa majengo ya Afisi, vitendea kazi vya kisasa na uhaba wa wataalamu wa fani mbali mbali. Kadhalika na upande wa Pemba ndio hiyo hivyo. Ili wizara hii iweze kutekeleza vyema malengo yake iliyojiwekea sambamba na kuwa na uwiyano wa watendaji baina ya Unguja na Pemba pamoja na kuheshimu malengo yaliyoanzishwa na wizara husika. Kamati yetu inaomba serikali kupitia wizara hii mambo yafuatayo yatakelezwe.

Chuo cha Utawala wa Umma

Kamati ya Sheria na Utawala inapongeza Chuo hiki kwa hatua inazochukua kupatia taaluma mbali mbali watumishi wa umma na wananchi kwa jumla. Pamoja na pongezi hizo Chuo kinakabiliwa na changamoto zifuatazo. Idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga chuo hicho hapo si watumishi wa umma. Jambo ambalo ni kinyume na malengo na uanzishwaji wa chuo hicho. Hivyo tunaomba serikali kufuatilia kwa kina suala hili ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, ingawa serikali inajitahidi kukipatia Chuo fedha zinazokadiriwa kwa mwaka. Kamati inashauri serikali kutenga fedha za kutosha katika mwaka wa fedha ujao ili chuo kiweze kukamilisha ujenzi wa jengo lao jipya kwa haraka iwezekanavyo. Tunashauri hili kwa kuwa jengo wanalotumia hivi sasa ni dogo na halipo katika mazingira mazuri. Jambo ambalo huwakwamisha

watendaji wa chuo. Kutokana hilo chuo kimelazimika kukodi jengo katika eneo la Mbweni ili kuweza kutekeleza malengo yake waliyojipangia ipasavyo, kitendo ambacho kinagharimu fedha nyingi.

Idara ya Nyaraka

Pamoja na mazingira magumu inayokabiliwa Idara ya Nyaraka, hata hivyo imeweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia. Miongoni mwa malengo hayo ni kuhifadhi ukaguzi na kufanyia thamani nyaraka mbali mbali za Serikali. Kamati inaunga mkono juhudi hizo. Hata hivyo pamoja na kuunga mkono kwake kamati yetu inaiomba serikali itekeleze yafuatayo ili iweze kufanikiwa ipasavyo idara hiyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa Idara hii hutoa huduma ya utafiti kwa watu mbali mbali na huduma hizo muhusika hulipa ada ya huduma hiyo. Basi Kamati inaiyomba serikali fedha hizo zilipwe moja kwa moja kwenye Idara kwa ajili ya shughuli hiyo, sio kama inavyofanyika hivi sasa.

Tunashauri ili kuwa na huduma hizo hutolewa na Idara za Nyaraka. Hivyo ni busara fedha hizo zikalipwa Idara hapo. Pamoja na hayo Idara ina mambo mengi ya kushughulikia na hasa ukizingatia kuwa bajeti ya mwaka inayopangwa huwa haikamiliki na haikidhi haja. Fedha hizo zisaidie katika ufanikishaji wa malengo ya Idara hiyo.

Aidha jengo la Afisi ni dogo sana ukilinganisha na majukumu ya Idara. Sambamba na hilo Idara hiyo imo ndani ya ukuta mmoja na nyumba ya raia. Jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa kiofisii hasa ofisi muhimu ya kutunza udhibiti wa Taifa kama hiyo. Kutokana na hilo, Kamati imeshauri kununuliwa nyumba hiyo ili watendaji wa idara waweze kutekeleza majukumu yao bila ya usumbufu wowote. Aidha tunashauri ijengwe ghara ambalo litakuwa ni kituo cha kumbukumbu.

Mhe. Spika, kwa kuwa Idara hii pamoja na mambo mengine hutoa huduma ya kuhifadhi nyaraka. Kamati inashauri kupatiwa vitendea kazi vya kutosha idara, zikiwemo kompyuta za kutosha ili kuingia hatua za kuhifadhi nyaraka zote kwa njia ya *electronic*. Hivi sasa kuna komyuta moja tu ya kuhifadhia taarifa ambayo haitoshi.

Sambamba na hilo Kamati inaishauri serikali kuipatia vifaa vya kisasa vya kutengenezea nyaraka, Afisi ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Pia Kamati inaziomba taasisi mbali mbali zinazochukuliwa Idara ya Nyaraka ili kama ghala za kuifadhia nyaraka. Halkadhalika Kamati inaziomba taasisi zinazohitaji huduma kutoka nyaraka walipwe watendaji wake posho. Hii

inatokana na kuwa shughuli wanazofanya watendaji hao ni kubwa na inahitaji umakini zaidi.

Mhe. Spika, tunashauri serikali kuzihifadhi vyema nyaraka za Serikali kwani imebainika takriban taasisi na vitengo vingi vya serikali hazihifadhi nyaraka hizo ipasavyo. Ingawa Idara na Nyaraka hudoa taaluma mara kwa mara kwa watumishi juu ya kuhifadhi nyaraka hizo.

Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mhe. Spika, pamoja na utendaji bora wa Afisi hii bado imekabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo ni muhimu serikali ikachukua hatua kwa haraka. Ili Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iweze kuendelea vyema kutekeleza majukumu. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kutokuwa na wafanyakazi wenye taaluma mbali mbali zinazowawezesha kufanya kazi kwa kisasa, ukiwemo ukaguzi. yakinifu *(Value of money audit)*, ukaguzi wa kompyuta *(Computer rise audit)* na ukaguzi wa mazingira *(Environmental audit)*, hawa wataalamu wote hawapo. Kwa hivyo nayomba serikali ifanye jitihada kuweza kuwaajiri wataalamu hao.

Mhe. Spika, ingawa ofisi hii imekamilisha jengo lake hapo Maisara bado inakabiliwa na ufinyu wa ofisi za kufanyia kazi. Kwani jengo hilo jipya halikidhi mahitaji ya wafanyakazi wote. Kutokana hilo pamoja na umuhimu wa afisi hii, Kamati inaiyomba serikali kununua nyumba iliyopo pembezeno mwa afisi hiyo, ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Aidha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imekabiliwa na changamoto ya maslahi madogo ya wafanyakazi. Hivyo Mhe. Spika, kwa kuzingatia jukumu zito na unyeti wa afisi hii. Kamati inaomba serikali kuwaongeza maslahi watendaji wa afisi hizi ili kuepusha vishawishi visivyo vya lazima. Aidha jambo hilo litawafanya watendaji hawa watekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mwisho

Mhe. Spika, sina dhamira ya kutumia muda wako mwingi zaidi ya hapo. Kwa vile najua wajumbe wangine wanataka kupata nafasi ya kuchangia. Hivyo kwa heshima na taadhima naomba uniruhusu nikushukuru wewe pamoja na Wajumbe kwa kunisikiliza kwa makini.

Aidha nataka kukushukuru wewe kwa mara ya pili kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha ripoti ya Kamati yetu na naomba kuwasilisha.

(Hoja imetolewa ijadiliwe)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kwanza na mimi kuchangia katika ripoti ya Katiba ya Sheria na Utawala ambayo na mimi ni mjumbe wake.

Nianze kwa kumpongeza na kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Ali Abdalla Ali Mwenyekiti wa Kamati yetu hii kwa jinsi anavyoonesha uwezo mkubwa katika kuiongoza kamati yetu na kutupa mashirikiano ya kutosha sisi wajumbe wake kuweza kutekeleza kazi zake.

Mhe. Spika, mengi yameelezwa katika ripoti ya Kamati yetu, lakini pia katika huu muhtasari ambao Mwenyekiti ameusoma. Nilikuwa naomba kulizungumzia jambo moja ambalo tumeona tusiliweke katika maandishi, lakini lilijitokeza tulipokuwa tukifanya ukaguzi wa shughuli mbali mbali ambazo zipo chini ya wizara hizi mbili hasa kule kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, tulipokuwepo Pemba, kama inavyojulikana kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi moja katika kazi zetu ni kuangalia thamani ya fedha zinazotumika katika miradi mbali mbali. Tulipata nafasi ya kutembelea afisi ambayo inatumika kama ni Afisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali kwa Upande wa Kisiwa cha Pemba pale Wete. Tulipotembelea jengo lile mimi binafsi nilipata nafasi ya kuuliza nani. alikuwa *contracture* ambaye alifanya kazi ile.

Kilichoshangaza, kwanza kulikuwa kuna khofu kubwa miongoni mwa watendaji wa Afisi ile kulijibu hilo suala. Lakini baada ya kukazania sana, nilishangazwa na wenzangu pamoja, sio peke yangu. Tuliambiwa kwamba zamana ya ujenzi wa jengo lile kwanza ilikuwa chini ya ndugu Msoma ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara iliyokuwa ikiitwa ya Katiba na Utawala Bora sasa ni Wizara ya Katiba na Sheria. Binafsi nilijiuliza sana kwanza sina taarifa kama ndugu Msoma anamiliki Kampuni ya Ujenzi.

Pili nilikuwa najiuliza hivi kanuni za fedha za serikali zinaruhusu kiongozi katika Wizara husika kuchukua dhima ya ujenzi katika shughuli ambayo iko chini ya Wizara ile? Tuliulizia kuhusu thamani halisi pale, lakini watendaji ndio kabisa walipata kigugumizi na wakatwambia hayo mtayapata huko huko kwenye Makao Makuu ya Wizara Unguja. Tuliambiwa hatua ya awali ilikwama na hatimaye ilibidi atafutwe mkandarasi mwengine amalizie kazi ile.

Hoja yangu kama nilivyosema ni ndogo tu, nilikuwa naomba Mhe. Waziri atakapokuja kututolea ufafanuzi atusaidie na suala hili. Kwa sababu tulizungumza mapema tulipokuwatana naye kwamba lilifikia wapi, tupewa maelezo kidogo. Moja katika kazi yetu katika Kamati ni kuona kwamba serikali inawajibika na watendaji wa serikali wanawajibika katika dhamana zao na hawajiingizi katika vitendo kama hivi ambavyo vinapelekea wananchi wetu kupitia sisi wawakilishi wao kuona mambo ambayo yanatia mashaka juu ya uwadilifu wa watendaji wetu. Nilikuwa naomba hili tupewe maelezo. Ikibidi kama maelezo yatakuwa hayaridhishi, basi si vibaya Baraza lako kuiomba ikiwa Kamati ya PAC ama hata kuagiza baadaye kupitia Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali kulifanyia uchunguzi suala hili na kutuletea ripoti hapa.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Kamati hii ya Utawala Bora. Kwanza nimsifu sana Mhe. Mwenyekiti kwa kuwasilisha ripoti yake kwa umahiri kabisa na ustadi wake wa aina yake kuwa yeye ni Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa sana lakini kidogo naomba nichangie katika maeneo hasa ya Mahakama zetu za Wilaya. Naanza na Mfenesini. Kwa kweli mazingira sio mazuri sana na hususan katika sehemu ya choo. Haihalisi hasa kuwa Mahakama ile ina level ya kuambiwa Mahakama ya Wilaya mpaka Mkoa. Ningemuomba Mhe. Waziri kidogo aweze kusaidia ujenzi uendane na ile *strategy* yenyewe ya ile Mahakama yenyewe.

Nikija kwenye Mahakama ya Mwera niseme pale kidogo panastahili sifa, kutokana na jengo lake zuri, vile ndio inavyotakiwa Mahakama kama ile. Kwa kuendelea hebu Mhe. Waziri anisaidie hili suala la Mahakimu wa Mahakama ambao tunawapigia kelele waingie katika suala la ardhi. Sijui kama limo miongoni mwake na kama limo katika Wizara yake basi ningemuomba Mhe. Waziri aweze kusaidiana na wizara ya ardhi kutokana na hali ambayo ni nzito sana.

Nimesema hivyo kuwa ni nzito kwa sababu sasa hivi kesi nyingi sana tena ni za kusikitisha hasa kabisa kutokana na hali ambayo wazee wetu wanaopeleka kesi kule kwa kudhulumiwa ardhi zao, wanakuwa wanashindwa kupata haki kutokana na kurundikwa zile kesi na kuwa zinakuwa nyingi. Kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri hili suala ajaribu kukaa pamoja na wizara hii ya ardhi ili kuweza kulitafutia ufumbuzi wa kina na kuweza kuwasaidia watu kuondokana na suala kama hilo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema sitakua na mchango mwingi na hasa ulivyotwambia tukusaidie wakati. Kwa hayo hayo naunga mkono asilimia mia kwa mia na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante sana. Inaonesha wajumbe wako wameshachoka, ndio maana wanataka shughuli imalizike. Mimi nitatoa mchango wangu mdogo sana ili kuiyunga mkono hii Kamati.

Mhe. Spika: Mhe. Salmini samahani, nataka niwaombe Waheshimiwa Wajumbe waliokuwepo nnje, warudi ndani ili tumalize kazi hii ya Ripoti ya Sheria na Utawala.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, kwanza niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe wake kwa kuwasilisha ripoti hii muhimu katika Baraza letu hili la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mimi kwa haraka haraka nimeweza kuipitia hii ripoti. Inaonekana changamoto nyingi zilizomo katika kamati hizi au katika wizara ambazo zinasimamia kamati hii ni ukosefu wa majengo. Ukiangalia katika idara zake zote isipokuwa labda ile ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Zote zinakabiliwa na matatizo ya majengo. Kwa kweli hii sio hali nzuri ya utendaji wa kazi. Kwa sababu vyombo vyetu hivi vinahitaji kuwa na ofisi zenye hadhi zinazolingana na majukumu yao. Niiyombe serikali kwa makusudi kabisa itoe kipaumbele katika bajeti zake ili tuone angalau kwamba tunapunguza baadhi ya matatizo ya majengo yetu au katika afisi zetu. Mengine hapa yameambiwa hayana hewa za kutosha.

Mhe. Spika juzi sisi tumeahirisha Baraza kutokana na ukosefu wa hewa. Sasa kama wenzetu hawa wanakosa hewa katika maofisi yao ya kutenda kazi na ndio kazi zao za kila siku, jambo hili haliwezi kuleta uwajibikaji ule unaostahiki. Mimi niombe serikali sana iweze kutoa kipaumbele ili wenzetu hawa waweze kupata afisi nzuri za kufanyia kazi. Naamini ufanisi utaweza kupatikana.

Mhe. Spika, moja kati ya shughuli ambazo wenzetu Afisi ya Mwanasheria Mkuu wameifanya kwa mujibu wa ripoti ni kuchapisha sheria pamoja na sheria ndogo ndogo, pamoja na Katiba. Tumekuwa wananchi wetu hawana uelewa wa sheria zetu. Pamoja na kwamba sheria hizi zinahitaji au wanahitaji wazielewe. Pengine lugha ambazo zinatumika wakati wa uandikaji wa sheria hizi zinaweza zikawa zinatupiga chenga. Nashukuru kwamba Katiba yetu inaeleza wazi kwamba lugha sahihi ya taifa ni Kiswahili. Lakini sheria zetu zinaandikwa kwa lugha ya kiingereza, isipokuwa Katiba tu ndio imeandikwa kwa Kiswahili na kiingereza.

Tunakumbuka kwamba hapa tuliwahi kupitisha ushauri wa serikali, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wakati wanapoandaa sheria waandae sheria zenye lugha mbili ya kiingereza na Kiswahili. Sijui utekelezaji wake ukowapi. Hii itatoa nafasi kwa wananchi wetu kuelewa mambo na kuelewa sheria zikoje kwa wale wanaohitaji kuzisoma. Kama tunavyojua sasa hivi tupo kwenye marekebisho ya Katiba, hata wananchi hawaelewi Katiba ni kitu gani, inasemaje. Kwa hivyo hili linaweza likasaidia wananchi wetu kuweza kuelewa. Tuanzie kwenye lugha, kuwe na sheria ambazo zinaandikwa kwa lugha ya kitaifa ambazo zinafahamika. Hatukatai kuandikwa Sheria kwa lugha ya kiingereza lakini na ya Kiswahili nayo ni muhimu iwepo na kwa sababu ndio lugha ya taifa.

Mhe. Spika, jengine ripoti hii imezungumzia juu ya ukosefu wa vitendea kazi kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Wakaeleza kwamba kuna ukosefu wa chombo muhimu kinachoitwa DNA ambacho kinawapa tabu kwamba chombo hiki hakipo hapa kwetu. Kwa hivyo inawawia shida au inawawia vigumu kuweza kupata ushahidi juu ya mambo yanayohusiana na mambo ya ubakaji na mambo mengine.

Mhe. Spika, juzi tumepitisha sheria ya Mtoto ambapo chombo hiki ni muhimu kuwepo katika nchi yetu ili kiweze kusaidia, kumsaidia Mkurugenzi wa Mashtaka kuweka kesi zake vizuri. Lakini pia kisaidie kupata uhakika juu ya mambo ambayo yanalalamikiwa. Jambo hili bado linaonekana ni tatizo kwetu. Sasa tuiombe serikali iweke umuhimu wa kitu hiki, kitaweza kutusaidia katika utekelezaji wa sheria zetu mbali mbali ambazo tunazitunga.

Jengine Mhe. Spika, ripoti inazungumzia juu ya kutokuwepo kwa vifaa vya kutosha kwa Mkemia. Hili nalo ni tatizo kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashataka kwamba Mkemia Mkuu wa Serikali bado hajapewa nafasi inayostahiki. Serikali itoe umuhimu wa kuwapatia jengo linalostahiki na kitengo chenyewe lakini na kupatiwa vifaa vya kisasa.

Mhe. Spika, hivi karibuni unakumbuka tulipitisha sheria ambayo imesimamiwa na Wizara ya Biashara ya Chakula inayohusiana na viwango vya chakula. Afisi ya Mkemia Mkuu itakuwa ni sehemu ya rufaa na hapa leo imejirejea tena. Inaonesha dhahiri kwamba jambo hili ni muhimu, afisi hii ni muhimu kuiweka katika hali ambayo inaweza ikafanya kazi. Kuwapatia vitendea kazi vinavyostahili Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuweza kutekeleza majukumu yake vizuri.

Mhe. Spika, mimi maoni yangu yalikuwa ni hayo machache sana. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni tunaiyunga mkono ripoti hii ya Kamati ya Sheria na Katiba mia juu ya mia.

Lakini niiyombe serikali izichukulie changamoto hizi kwamba zinahitaji kutekelezwa, zisibakie kwenye ripoti tu. Serikali ichukue kila linalowezekana ili kuona ushauri pamoja na mapendekezo na hizi changamoto ambazo zimeelezwa katika wizara zinazohusika ziweze kutekelezwa, isije ikawa mwakani inaeleza mambo yale kwa yale, hakuna utekelezaji wowote. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kwanza nimpongeze Mhe. Mwenyekiti, kwa kuleta ripoti yake hapa mbele yetu. Mimi niongelee suala alilolizungumza kuhusu Idara ya Nyaraka.

Nisiwe mwizi wa fadhila, katika kufika hapa mimi niliondokea pale. Kwa hivyo najua yale matatizo ambayo yanaikabili idara ile. Idara ilikuwa sehemu mbali mbali na punde tu Idara hii ilikuwa chini ya Wizara ya Elimu. Idara hii kulingana na wizara majukumu wizara ilikuwa bajeti yake ni finyu sana na kuna mambo ya muhimu. Kuna vifungu ambavyo vilikuwa ni lazima vipate pesa na hasa kifungu cha matumizi ya umeme. Kwa kuwa pale kunahifadhiwa nyaraka nyingi na nyingi zinakuwa za muhimu na za serikali. ili kuweka ule ubora wa nyaraka ni lazima pawe na umeme. Ukisema kwamba umeme unakatika kwa muda mfupi tu basi nyaraka zile zinakatika katika kwa sababu ya hali ya hewa ilikwisha izowea ya ubaridi.

Kuiweka idara hii katika Wizara ambayo ina mambo mengi na ya muhimu kwa kweli ni kikwazo. Nishukuru kwamba safari hii imeingia katika Wizara ya Utumishi wa Umma. Ningemuomba waziri aitizame sana idara hii ili iweze kuhimili vile vifungu vilivyokuwa ni muhimu zaidi. Kwa kuwa ni idara muhimu inabidi wafanyakazi wake wawe na utaalamu wa kutosha.

Mhe. Spika, nisipoteze muda mwingi kwa sababu muda hauturuhusu basi niseme nimechangia kwa niaba ya wananchi wangu walionichagua wa Jimbo la Amani, naunga mkono ripoti hii. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, napenda niwashukuru wajumbe wote ambao walichangia nao nio watano na nashukuru kwamba michango yao yote ni mizuri na tutaifanyia kazi.

Mhe. Spika, kuna mambo matatu ambayo napenda niyatolee ufafanuzi. La kwanza ni suala ambalo aliliuliza Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusu ujenzi wa Afisi ya Wakfu Pemba, na kwamba Naibu Katibu Mkuu wangu ndiye aliyekuwa Mjenzi. Naibu Katibu Mkuu hakuwa Mjenzi kama ni Naibu Katibu Mkuu, lakini baada ya suala hili kuliuliza katika kamati mimi nilifuatilia na ni kwamba, Ndugu Msoma ana kampuni yake ya ujenzi ambayo ilikuwa

registered. Kampuni hiyo ili-*tender* pamoja na kampunmi nyengine tatu. Sasa kwa bahati nzuri kampuni yake ndio iliyoshinda ujenzi huu. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, kwa sababu hakuna *restrictions*, hapa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na anajenga ofisi za serikali na vitu vyengine, kwa utaratibu ambao umewekwa basi na yeye akapewa *contract* hii ya kujenga ofisi hiyo.

Suala la kusema kwamba jengo lile ana wasiwasi nalo kwa sababu ya *value for money* mimi nina wasiwasi kidogo. Kwa sababu kampuni au kitu ambacho kinatizama ile *value for money* ni watu watatu, ni *PAC* ya Kamati yako Mhe. Spika, wanaweza wakenda wakatizama *value for money* au kuna *internal auditors* au *external auditors* kwa kutizama hasa. Lakini ninavyojua pahala ambapo imejengwa ile ofisi iko Wete karibu na uwanja wa mpira, ardhi ya pale siku zote inakatika katika. Kwa hivyo, ujenzi wake unataka msingi ulio madhubuti sana. Sasa mimi sina uhakika kiasi gani cha fedha kilichotumika katika msingi na kuja juu, lakini suala hilo tumewaambia watu wa *audit* kwenda kuliangalia na kutizama hasa suala hilo, lakini hio actually ndivyo ilivyotokea.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amezungumzia suala la mahkama. Mahkama zetu nakubali kwamba zote si nzuri sana, hazina *facilities*, hii tumeiona na tunajitahidi kama tulivyoripoti katika kamati kwamba tunajitahidi ku-s*olve* baadhi ya mambo ambayo ni muhimu. Kwa mfano, zile mahkama ambazo hazina vyoo tunajitahidi na hasa kuanzia kipindi cha bajeti *Inshaallah* tutaendelea kuzishughulikia.

Lakini pia alizungumzia suala la Mahkama ya Ardhi. Kweli kuna matatizo ya Mahkama ya Ardhi, kuna Mahkama za Ardhi mbili, moja ni Pemba na moja Unguja. Bahati mbaya Mahkama hizi ziko katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, lakini ni sisi tunaotoa Mahakimu. Sasa Mahkama hizi za Ardhi hapa Unguja kwa kweli kuna kesi nyingi sana na Pemba kuna kesi nyingi sana.

Sasa tulichofanya ni kwamba tumeshajaribu kuomba Mahakimu ambao tutawaongeza kwa Unguja na Pemba, tunachofanya ni kwamba, tutafungua Mahkama nyengine ya Ardhi Kaskazini Unguja, Gamba. Pale jengo lipo na kesi nyingi za sehemu ya Kaskazini zitapungua kwa upande huo na kwa Pemba tutafungua Mahkama moja Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kwa sababu iliyoko hivi sasa ni Mkoa wa Kusini Pemba. Kwa hivyo, angalau tukipata Mahkama mbili Unguja na mbili Pemba tatizo hili kidogo linawea kupunguka na hapo baadae tutatizama uwezekano wa kuongeza.

Mhe. Salmin Awadh Salmin alizungumzia kuhusu miswada ya sheria na kweli nakubaliana naye kwamba lugha yetu ni Lugha ya Kiswahili na kama alivyosema kuwa tuliwahi kulizungumza suala hili kwamba miswada hii nayo iandikwe kwa Lugha ya Kiswahili. Napenda niseme tu kwamba, shughuli ya kuandika sheria kwa Kiswahili ni shughuli ngumu kidogo, suala hili lipo katika ofisi zetu za Mwanasheria Mkuu, tunatizama uwezekano kwa sababu unapoandika kile kitu ni lazima kiwe ni kizuri na tusifanye *rash*. Kwa hivyo, kwa hivi sasa tutaanzia hii hii kwa Kiingereza ingwa tunatafsiri *bills* hizi kwa Kiswahili, lakini pale ambapo tutakuwa tumeshapata watu wa uhakika ambao wanaweza wakatafsiri hasa basi hilo tutalifanya.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la Ofisi ya Wakfu na Ofisi ya Mrajis Mkuu. Tatizo ni kwamba ofisi ile ni ndogo, ni kweli kwa sababu mwanzo tulikuwa Mambomsige lakini baadae tukahama na tukahamia *PBZ* ya zamani nayo ile ni ndogo sana. Sasa ile kwa kweli hatuwezi kufanya *development* yoyote kwa sababu mbili. Kwanza lile jengo ni dogo, lakini pili lile jengo ni la zamani. Sasa kwa mujibu wa utaratibu wa siku hizi hayo mambo ambayo yalizungumzwa ya *IT* ya utaratibu wa siku hizi huwezi ukayaweka katika majengo kama yale.

Lakini bahati nzuri, fedha tulizopata baada ya kukodishwa lile Jumba la Mambomsiige fedha hizo sasa tumeshakabidhiwa sisi na tumeshapata kiwanja, tumeshaanza kutoa *tender* kwa kujenga ofisi hiyo ambayo tuta-*accommodate* Ofisi ya Mrajis Mkuu, Ofisi ya ya Wakfu pamoja na Ofisi ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa hivyo, jengo hilo litakuwa ni kubwa litachukua mazingira yote ambayo yanatakiwa kwa kufanya ofisi ya kisasa, *tender* zimeshatolewa na ninaamini kwamba si muda mkubwa ujenzi utaanza rasmi karibu na Ofisi ya Vitambulisho. Eneo lote lile pale ni letu na tumeshapata kila kitu hivyo hatutokuwa na matatizo mengine tunasubiri ile *process* ya *tender* tukishamaliza ujenzi utaanza rasmi.

Mhe. Spika, la mwisho ambalo nataka kulisema ni kwamba, katika Ofisi ya *DPP* walizungumzia kuhusu ukosefu wa *DNA* na kwamba kesi nyingi zinarundikana kwa sababu hakuna majaji. Ni kweli Mahakimu wetu ni kidogo, lakini tumeshafanya *process* ya kupata Mahakimu wengine lakini tunasubiri katika bajeti inayokuja ili tuweze kupata fedha hizo na Mahakimu *Inshaallah* tutawapata wengi na tutapunguza, sisemi kwamba tutamaliza yote, lakini kwa kiwango kikubwa tutapunguza.

Suala la *DNA* kweli ni suala ambalo *DPP* analihitajia sana, lakini hili liko kwa Mkemia Mkuu ambako ni Wizara ya Afya. Sisi tutashirikiana na Wizara ya Afya ili kuhakikisha kwamba suala hili la *DNA* linapatikana ingawa mashine yenyewe ni ghali sana na naamini kwamba serikali iliwahi kutoa maelezo

kusema kuwa inajitahidi kutafuta kifaa hiki kwa ajili ya shughuli zetu za Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo napenda niseme na nihakikishe kwamba, yote yale mengine ambayo wameyaona kamati tumeyachukua na tunayafanyia kazi. Mengine kama unavyojua Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba tumeshaanza kuyafanyia kazi na *Inshaallah* wakati wa bajeti tutaripoti wapi tumefika katika shughuli hizi. Nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nikushukuru na mimi kunipa nafasi kutoa maoni au ufafanuzi juu ya maeneo machache ambayo yameguswa katika ripoti hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi.

Kwanza napenda sana nichukue nafasi kumshukuru Mhe. Mwenyekiti wa kamati hiyo na wajumbe wake kwa kuwasilisha ripoti hii ambayo imeeleza mambo muhimu, sisi kama wizara tunatakiwa tuweze kuyafanyia kazi.

Kwa ujumla nataka nitangulie kusema kwamba, mengi waliyoyatoa Mhe. Spika, kwenye ripoti hii ni ushauri kwa wizara, kwa msingi huo nasema kwamba, mimi pamoja na watendaji wangu tutahakikisha tunayafanyia kazi na wakati wa kuwasilisha bajeti ya mwaka 2011/2012 Baraza hili litashuhudia ni kwa jinsi gani tutakuwa tumeyachukulia hatua.

Lakini naomba nitoe ufafanuzi kwa maeneo machache hasa lile suala la Chuo cha Utawala wa Umma ambalo mwenyekiti amelizungumza sana. Hata katika maswali na majibu yaliyopita niliulizwa swali hili juu ya suala la kuwasomesha wafanyakazi wa serikali kupitia chuo kile na raia ambao si wafanyakazi wa serikali. Ikaelezwa kwamba, malengo ya chuo hiki hasa ni kuwasomesha wafanyakazi.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme malengo makuu ya taasisi yoyote yanakuwa kwanza ni sera na sheria iliyoanzisha ile taasisi. Sera ya Chuo cha Utawala wa Umma ni kukifanya chuo kiwe kina uwezo wa kujiendesha na kujitegemea, na sera yetu ni kutoa taaluma kwa Wazanzibari wote na wengine ambao watahisi kwamba wana haja ya kuja kupata taaluma kwenye chuo chetu. Kwa hivyo, sera yetu sio kuwasomesha tu wafanyakazi watupu peke yake, hapana, lakini kuwasomesha Wazanzibari wote ambao watakuwa wana haja ya kupata taaluma tulizonazo pale chuoni kwetu.

Kwa hivyo, mkakati utakaosisitiza ni ule wa kuzingatia sera yetu na sheria ya chuo chetu. Hata hivyo, wizara yangu kwa kuelewa umuhimu wa kuwapa taaluma wafanyakazi wa serikali ndio maana Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar imeanzisha hii wizara na miongoni mwa idara zilizomo ndani ya wizara hii, tumeanzisha Idara ya Mafunzo ya Rasilimali Watu (wafanyakazi). Kwa maana hiyo, mipango mikakati ya kuwafundisha wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunayo na tunaiandaa pale kupitia idara hii.

Tutatoa muongozo kwamba kila wizara kupitia idara yake ya utumishi na uendeshaji lazima iwe na hicho kitengo cha mafunzo ya wafanyakazi. Hata sheria yetu tuliyoipitisha tumehakikisha miongoni mwa mambo ambayo yamezingatiwa watu wengi walidhani kwamba sheria ile itazingatia maslahi tu kwa maana ya mishahara na maposho, lakini inazingatia pia kumuendeleza mfanyakazi ili asibaki pale alipo. Kwa hiyo napenda nimhakikishie mwenyekiti wa kamati na Baraza lako tukufu, kwamba eneo hilo tunalizingatia la kuweza kuwasomesha wafanyakazi wa serikali.

Tuna njia nyingi tu pale za kuweza kutoa haya mafunzo, hata kama mtu hana sifa tunatoa mafunzo ya miezi mitatu kuangalia uwezekano wa kuona kwamba tunaweza tukamnyanyua angalau akaanza na cheti kabla hajaanza yale mafunzo ya cheti ya mwaka mmoja au miezi tisa. Kwa hivyo, juhudi zitaendelea. Lakini kwa wale ambao tunahisi hawa sasa hawawezi kusomesheka hapo tena tutakuwa hatuna namna, lakini serikali kupitia wizara yangu hilo tunalizingatia.

Mhe. Spika, lililozungumzwa kwenye ripoti hii pia ni ufinyu wa bajeti jambo ambalo linaeleweka. Lakini kama tunavyoelewa kwamba taasisi zote zilizomo kwenye wizara hii, zilikuwa ni taasisi zilizotoka kwenye wizara nyengine huko nyuma. Kwa hivyo, tupewe nafasi basi, kwa sababu wizara hii ni mpya na kwa mara ya kwanza ndio tutaanza kupanga bajeti yetu kupitia wizara hii basi nadhani tunaweza tukaona ni kwa jinsi gani bajeti yetu tunaiweka kwa mujibu wa matakwa ya shughuli zetu zitakavyokuwa.

Jengine ambalo limejitokeza kwenye ripoti hii na mwenyekiti amelizungumza kwa nguvu zake zote na mimi nakubaliana naye Mhe. Mwenyekiti na nimpongeze sana kwa kuliona hili. Juu ya suala zima la utawala bora. Ukweli ni kwamba, huwezi kuwa na kitu kama huna sera inayokuongoza katika kuendesha hiyo shughuli. Sasa nishukuru viongozi waliopita kwa kuanza angalau na mkakati wa suala hili la utawala bora. Lakini hivi sasa wizara yangu tuko katika hatua za mwisho za kukamilisha sera ya utawala bora ambayo tunatarajia si muda mrefu itakwenda kwenye kikao cha Makatibu Wakuu na hatimaye itakwenda kwenye *cabinet* na baadae serikali itaipitisha sera hiyo. Hapo sasa tukiw ana sera tutaweza kufanya kazi vizuri inayohusiana na *good governance*.

Ni kweli huko nyuma kuna kamati katika kila wizara lakini hakuna wizara ambayo imeweza kulifanyia kazi hili jambo. Na kwa sababu hakuna namna ya

kuweza kuwakamata kwamba bwana wewe hujatekeleza hili unafanyaje, kwa sababu hakuna sera. Sasa kwa kuwa tuko katika hatua za mwisho za kumalizia sera ni imani yangu kwamba sera ikikamilika na taratibu nyengine zikikamilika basi tutaweza kusimamia vizuri suala hili la utawala bora.

Mhe. Spika, kuna jengine ambalo limezungumziwa suala la nyaraka namna tunavyozihifadhi. Kama tunavyojua kwamba muda mwingi taasisi hii imekuwa ikiwa kama ni kijisehemu cha idara, lakini Serikali hii ya Mapinduzi chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar, imelitilia mkazo hili jambo na kuweka mkakati wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na nafasi nzuri au njia ya kuweza kuhifadhi nyaraka zetu. Ndio maana sasa idara hii sio kitengo bali inaitwa ni Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa. *(Makofi)*

Nia ya wazo hili ni kufanya kwamba lazima tuwe na utaratibu mzuri wa kuweza kuhifadhi nyaraka zetu. Mwenyekiti wa Kamati amesema angalau tuwe na ghala la kuhifadhi, lakini mimi siiti ghala ni *strong room*, lazima tuongeze *strong* kwa ajili ya kuhifadhi nyaraka zetu za taifa. Lazima tuseme kweli, utaratibu unaotumika hata kwa wizara na taasisi nyengine za serikali, nyaraka za serikali zina muda wake, naomba wanivumilie Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu ni mambo ambayo yameelezwa na naomba nitoe ufafanuzi juu ya hili suala la nyaraka.

Suala la nyaraka ni kitu muhimu, lakini sote ni mashahidi tukienda katika taasisi za serikali kule kwenye mipira ya zamani ya magari, kule kunakowekwa mandoo ya *oil* chafu ndiko nyaraka zinakowekwa. Matokeo yake tunawapa kazi watu wetu wa Idara ya Nyaraka wakati wanapotaka kuzichambua sasa kujua zipi za kuziteketeza kwa maana ya kuzi *destroy* na zipi ambazo zinahitaji kuwekwa kama ni kumbukumbu ya taifa. Sasa nadhani kuanzishwa kwa idara hii kwanza tutanyanyua hadhi ya wafanyakazi watakaoshughulikia nyaraka. Tumezowea tu kwamba watu wanaoshughulikia masjala ni watu wa chini, lakini kumbe sivyo. Hii ni taaluma au ni kada ambayo inahitaji watu wake wawe na ujuzi wa kuweza kufanya hizi kazi.

Kwa hivyo, napenda nisema kwamba, watakaokuwa wanashughulikia nyaraka sasa napale kwenye Chuo cha Utawala wa Umma tunayo kada hii tunatoa mafunzo, kuna watu wanachukua *certificate* na wanachukua diploma ya *record management*. Watu hawa sasa watajulikana, kwa mfano yule mkuu wa masjala atajulikana kama *record manager* ili aweze kuwa na hadhi watu wasimdharau, wakimdharau yeye na zile nyaraka zenyewe zinadharaulika. Lakini pia tutatoa muongozo kwa taasisi zote za serikali, kwamba sehemu ya masjala isiwe ni sehemu ya ovyo ovyo tu, kila taasisi ni lazima ijenge *strong room* kwa ajili ya kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu zao. Kwa hivyo, napenda niseme kwamba eneo hili nalo tutalifanyia kazi.

Eneo la mwisho ambalo nataka nilitolee ufafanuzi ni suala zima la maslahi madogo ambayo yamezungumziwa juu ya suala la Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Lakini maslahi madogo Waheshimiwa Wajumbe na Mhe. Spika, si kwa ofisi hii tu ya Mdhibiti kama nilivyosema kwenye jibu langu nililolitoa wiki moja iliyopita, ni kwa serikali nzima. Nataka niwahakikishie kwamba, nia ya serikali kupitia wizara yangu ni kuhakikisha kwamba tunanyanyua maslahi ya wafanyakazi kwa nguvu zetu zote.

Jana nilipokuwepo Pemba nilikuwa naarifiwa na hii nini athari yake? Athari yake ni kwamba kweli kabisa kuwa baadhi ya wataalamu tunawakosa kwa sababu ya maslahi madogo. Jana niliarifiwa Pemba kwamba hivi karibuni karibu wataalamu 20 wa kilimo wametukimbia kwa sababu ya maslahi madogo. Sasa napenda nimshukuru mwenyekiti kwa kuliona hili, lakini serikali kupitia wizara yangu kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012 kama alivyotangaza siku ile Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba tutakja na bango kitita kwa ajili ya maslahi ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wawe wastahamilivu tutakapokuja kwenye bajeti yetu basi tutakuja na taarifa inayohusiana na kuwapa maslahi mazuri wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naomba sasa na mimi niunge mkono taarifa hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsane Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuja kufanya majumuisho, lakini kabla sijafanya majumuisho naomba niweke *hansard* sawa. Kwenye hotuba niliyosoma Kamisheni ya Wakfu inanunua maji shilingi 70 elfu kwa wiki moja, sio siku moja. naomba ieleweke hivyo.

Baada ya hapo nichukue nafasi hii kuwashukuru wajumbe wangu wanne waliochangia katika kamati yetu hii tukianza na Mhe. Ismail Jussa Ladhu (Mjumbe wa kamati), Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Fatma Mbarouk Said. Nawashukuru wote kwa michango yao lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa kujibu hoja vizuri na kutupa ahadi kwamba matatizo yote, changamoto watatekeleza kwa hali na mali. Kwa hivyo, tutawashukuru na sisi tutafuatilia utekelezaji huo ili twende sambamba katika kutekeleza mambo yetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaoikubali na kuipokea ripoti hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Ripoti hiyo sasa ifanyiwe kazi ili kutekeleza yale maelekezo na mapendekezo ya kamati hiyo. Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukue nafasi hii kukushukuruni katika hatua hii ya kwanza kwa kumudu kupitisha ripoti zote tatu kazi ambayo kidogo ilikuwa ni nzito, lakini kwa msaada wenu mkubwa tumemudu kufanya hivyo. Nakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na mawaziri kwa kazi hiyo nzuri.

(Saa 8:20 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika *(PAC)*

Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika *(PAC)* (Mhe. Omar Ali Shehe): Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na tukaweza kukutana ili kuendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, napenda kukushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa niaba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika kwa kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa kazi za Kamati kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi zinavyoelekeza kupitia kifungu cha 106(14) toleo la mwaka 2011.

Mhe. Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati ya *PAC* kutoa shukurani zetu za dhati kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati hii kwa muda wote wa kazi ikiwa ni pamoja na kutoa muongozo thabiti katika kutekeleza kazi za Kamati hii, ikieleweka kwamba Afisi hii ndio mdau mkubwa wa Kamati ya *PAC* katika kutekeleza majukumu yake iliyopangiwa kisheria. Aidha, napenda kuzishukuru Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali kutokana na mashirikiano makubwa waliyoyaonesha wakati wote Kamati ilipokuwa ikifanya kazi za kufuatilia maagizo kwa Taasisi hizo.

Mhe. Spika, nitakuwa mpungufu wa fadhila iwapo sitowashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya *PAC* kwa mashirikiano makubwa waliyoyatoa wakati wa kufanya kazi na hatimae tukaweza kuwasilisha ripoti ya Kamati mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, Kamati ya *PAC* imeundwa na Wajumbe wafuatao:-

1. Mhe. Omar Ali Shehe - Mwenyekiti
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Juma Abdalla - Mjumbe
4. Mhe. Farida Amour Moh'd - Mjumbe
5. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Mjumbe
6. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad - Mjumbe
7. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman - Mjumbe
8. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Mjumbe
9. Ndg. Abdalla Ali Shauri - Katibu
10. Ndg. Othman Ali Haji - Katibu

Mhe. Spika, Kamati ya *PAC* imeundwa kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi kifungu cha 115 toleo la 2011 na kupewa majukumu yake chini ya kifungu cha 115(2) cha Kanuni hizo ambayo ni:-

a) Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya hesabu za mwaka za matumizi ya fedha za Serikali na Mashirika yake na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

b) Kuchambua na kutafakari ripoti yoyote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pale ambapo Rais ataagiza ukaguzi huo ufanywe.

c) Kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali na asasi zake.

d) Kutoa ripoti yake baada ya kufanya uchunguzi kuhusuiana na matumizi ya ziada ya fedha iliyotolewa kwa mwaka wa fedha unaohusika.

Aidha, ifahamike wazi kwamba katika kufanya kazi zake Kamati ya *PAC* itakuwa na wajibu wa kuchunguza kama:

Fedha zilizooneshwa katika Makadirio ya Matumizi ya Serikali na Mashirika yake zimetumika kama ilivyokubaliwa; na matumizi yalikuwa chini ya mamlaka inayohusika na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa majukumu haya ya Kamati kama yalivyoainishwa na Kanuni za Baraza la Wawakilishi ni dhahiri kwamba Kamati ya *PAC* ina jukumu zito la kuchunguza na kuhakikisha kuwepo kwa nidhamu nzuri za matumizi ya fedha na rasilimali za umma, suala ambalo ni muhimu sana kutokana na ukweli kwamba kwa kipindi kirefu kumekuwa na matumizi mabaya ya rasilimali pamoja na wizi wa fedha za Umma.

Mhe. Spika, naomba niipongeze Serikali kwa juhudi za kuimarisha misingi ya utawala bora nchini kwa kuanzisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yenye jukumu la kuhakiksha kwamba:

- Fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

- Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo, na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

- Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, Hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Kamati ya *PAC* katika kufanya kazi zake, mbali ya muongozo wa Katiba ya Zanzibar na Kanuni za Baraza la Wawakilishi, pia inaongozwa na Sheria zifuatazo:

1. Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni *zake (Public Finance Act No. 12 of 2005 and The Public Finance Regulations, 2005);*

2. Sheria ya Ununuzi na Ugavi wa Mali za Umma na Kanuni zake *(Public Procurement and Disposal of Public Assets Act No. 9 of 2005 and Its Regulations).*
3. Sheria ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(Public Investment Act No.4 /2002)*
4. Sheria ya Baraza la Manispaa *(The Zanzibar Municipal Council Act No. 3 of 1995)*
5. Sheria ya Kuanzisha Halmashauri na Mabaraza ya Miji *(The Districts and Town Councils Act No. 4 of 1995).*
6. Sheria ya Pencheni (Kwa Watumishi wa Kisiasa) - *Pensions (Political Appointees) Act No. 1 of 1990.*
7. Sheria ya Kuanzishwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(The Establishment of the Office of The Controller and Auditor General Act No 11 of 2003).*
8. Sheria ya Kinga na Fursa za Wajumbe *(The House of Representatives (Immunities, Powers and Privileges) Act No. 4 of 2007)*

Pamoja na Kanuni nyengine zinazohusiana na makusanyo, matumizi na malipo katika taasisi mbali mbali za umma kama zilivyoidhinishwa na mamlaka husika.

Mhe. Spika, Serikali imejitahidi kuweka misingi madhubuti ya udhibiti wa rasilimali za umma kwa kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hatimae kuwasilisha katika Baraza hili Sheria nilizotangulia kuzieleza kwa lengo la utekelezaji wa utawala bora katika udhibiti na kuchunga nidhamu ya matumizi ya fedha na rasilimali za umma. Pamoja na juhudi hizo za Serikali, Ripoti za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali bado zinaonesha mapungufu makubwa ya kiutendaji ambayo yanarejesha nyuma juhudi na ari ya washirika wa maendeleo pamoja na azma ya Serikali ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa wananchi wake.

Mhe. Spika, kama tulivyoshuhudia katika wiki iliyopita, Mhe. Waziri wa Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora aliwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2008/2009. Hii ina maana kwamba Kamati ya *PAC* haikuweza kuifanyia kazi ripoti hiyo kwa mwaka uliopita na badala yake katika mzunguko wa awali wa kazi za Kamati, Kamati ilipata mafunzo ya kuijengea uwezo kupitia mada mbali mbali zikiwemo:- Sheria ya Fedha na Manunuzi, Utaratibu wa Mzunguko wa Fedha Zanzibar, Maadili ya Ukaguzi na Wakaguzi, Aina za Ukaguzi, Uzoefu wa Kamati ya *PAC* katika Ushirikiano wa Kimataifa na Uhusiano wa Ukaguzi na Utawala Bora kwa lengo la kuijengea uwezo wa kuanzia kazi. Aidha, mafunzo hayo tuliyapata kupitia Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za

Serikali kwa kushirikiana na Afisi ya Baraza la Wawakilishi. Tunazipongeza sana Taasisi hizi kwa kutambua umuhimu wa kuipatia Kamati mafunzo hayo hasa tukizingatia kwamba wengi kati ya Wajumbe wa Kamati yetu ni wapya katika shughuli za Kamati na shughuli za Baraza kwa ujumla.

Mhe. Spika, katika mzunguko wa pili wa kazi za Kamati zilizoanza tarehe 28/02/2011 na kumalizika tarehe 11/03/2011, Kamati ilifuatilia maagizo yaliyotolewa na Kamati ya *PAC* kuanzia mwaka wa 2006/2007; 2007/2008; 2008/2009 na 2009/2010. Lengo kuu la kazi hii ilikuwa ni kuikumbusha Serikali wajibu wake wa kuzifanyia kazi Ripoti za Kamati na kujiridhisha kwa kiasi gani Serikali inayatekeleza maagizo mbali mbali yanayotolewa na Kamati kupitia ripoti hizo. Katika ufuatiliaji wa maagizo hayo kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na Ripoti za Kamati ya *PAC* zimeonesha sura zifuatazo:

1. SURA YA UPOTEVU WA FEDHA ZA UMMA KUPITIA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MANUNUZI

Mhe. Spika, hoja nyingi zilizojitokeza katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni upotevu wa fedha za umma zilizoidhinishwa na Baraza hili kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya shughuli za Serikali pamoja na manunuzi ya vifaa mbali mbali katika taasisi za Serikali. Ripoti za Mdhibiti zinaonesha kwamba katika Wizara, Mashirika na Taasisi za Serikali huwa kuna upotevu mkubwa wa fedha za umma unaofanyika ambapo wakati wa ukaguzi hutolewa maelezo tu bila kuwa na vielelezo *(Supporting Documents)* vinavyothibitisha uhalali wa malipo hayo, uhalisia wa matumizi ama utoaji wa fedha zilizotumika.

Kwa mfano, katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2005/06 iliripotiwa kuwa jumla ya Tsh. 1,721,401,530.35 na U$378,844.92 zimepotea. Aidha, ripoti ya mwaka 2006/07 imeripotiwa jumla ya Tsh. 1,273,364,649 na U$ 72,893 zimepotea na katika ripoti ya mwaka 2007/208 imeripotiwa kuwa jumla ya Tsh. 269,757,772 na U$ 145,480 zimepotea. Upotevu huu umetokana na malipo ya masurufu *(imprest)*, malipo yasiyo na vielelezo vya uthibitisho na idhini ya malipo, hati za malipo ambazo zilikosekana wakati wa ukaguzi *(missing vouchers)*, vifaa ambavyo havikuingizwa katika daftari la vifaa, mikataba ya ujenzi pamoja na malipo yasiyo na stakabadhi (risiti).

2. SURA YA KUPOTEA KWA MALI ZA UMMA KUTOKANA NA KUTOKUWEPO KWA DAFTARI LA KUHIFADHIA MALI ZA KUDUMU *(FIXED ASSET REGISTER)*

Mhe. Spika, mbali ya rasilimali fedha, mtaji mkubwa wa Serikali ni mali mbali mbali zinazomilikiwa na Serikali kwa niaba ya wananchi ziwe ni zenye kuhamishika na zisizohamishika. Sote tunafahamu namna ambavyo Serikali inavyoweza kuzitumia rasilimali hizi katika kujiendesha kiuchumi.

Ni kitu cha kusikitisha sana kuona hadi leo, ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinavyoonesha udhaifu wa jinsi ambavyo taasisi nyingi za Serikali na Mashirika ya Umma yanavyoshindwa kuwa na daftari ama mfumo unaoonesha orodha ya mali zinazomilikiwa na taasisi husika pamoja na thamani halisi ya mali hizo. Aidha, inasikitisha pia kuona kuwa baadhi ya majengo ya Serikali hayana hatimiliki, hata sehemu muhimu zinazotumika kwa ajili ya vitega uchumi nyeti vya Serikali kama vile Bandari hawana hatimiliki.

Mhe. Spika, mapungufu haya mbali mbali hupelekea Serikali kutokujua uhalisia wa mali zake na mtaji wake wa uchumi. Aidha, hali hii inaweza kupelekea wajanja kujitwalia mali za umma kwa njia ya udanganyifu. Katika kukabiliana na hili, Kamati yangu ilitoa agizo kwa taasisi zote pamoja na Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia Idara ya Uhakiki Mali kuhakikisha kuwa Taasisi zote za Serikali na Mashirika ya Umma yanakuwa na daftari la kuhifadhia mali za kudumu pamoja na kuweka thamani za mali hizo. Kamati yetu inaipongeza Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kuandaa muongozo huo na kuusambaza kwa Taasisi zote za Serikali.

Aidha, mbali ya kasoro ya kutosajiliwa, Kamati yetu imebaini kuwa baadhi ya mali za umma zimekodishwa kwa bei ya kutupa na kwa thamani isiyolingana kabisa na thamani halisi pamoja na mikataba yenye utata. Ni matarajio ya Kamati kuwa Taasisi zote za Serikali zitawajibika na utekelezaji wa kusajili mali za Serikali zinazomilikiwa na taasisi zao pamoja na kuziwekea thamani. Kamati ya *PAC* haitokubali tena kuivumilia hali hii ya kuzifanya mali za Serikali kama "Shamba la Bibi". Aidha, Kamati ya *PAC* inaishauri Serikali kufanya mapitio ya mali zote za umma zilizo mikononi mwa watu binafsi na ambazo umiliki wake haukufuata sheria kwamba mali hizo zirejeshwe Serikalini. *(Makofi)*

3. SURA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

Mhe. Spika, moja kati ya jukumu la Kamati ya *PAC* ni kuchunguza kama "fedha zilizoidhinishwa katika makadirio ya matumizi ya Serikali na Mashirika yake zimetumika kama ilivyokubaliwa na matumizi yalikuwa chini ya mamlaka husika na kama matumizi yalizingatia thamani halisi ya fedha".

Kwa mnasaba wa jukumu hili, Kamati imebaini kuwepo kwa uhaulishwaji mkubwa *(reallocation)* unaofanywa na baadhi ya taasisi, uhaulishwaji huu unachafua sura ya bajeti kama ilivyoidhinishwa na Baraza hili tukufu. Mbali na uhaulishwaji wa matumizi ya vifungu, pia Kamati imebaini kufanyika kwa matumizi yaliyo kinyume na yalivyoidhinishwa na Baraza hili.

Mhe. Spika, napenda nizikumbushe Wizara na Taasisi za Umma kuwa kufanya kinyume na kile kilichoamuliwa na Baraza hili, ni kwenda kinyume na taratibu na ni chanzo kikubwa cha UFISADI wa fedha za Umma. Pamoja na ufinyu wa bajeti kama hoja inavyotolewa, watendaji hawana budi kupanga bajeti kwa kuangalia vipaumbele vilivyo muhimu zaidi kwani "KUPANGA NI KUCHAGUA"

Mhe. Spika, Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya Taasisi aghlabu humalizia vifungu vya bajeti kabla ya kumalizika kwa miezi sita ya bajeti (Vifungu vya Safari), na miezi sita mingine hujaliziwa kwa kuuliwa vifungu vyengine vikiwemo vifungu vya mafunzo ya Ukimwi, malipo ya umeme, maji, mafunzo ya ndani na mengineyo.

Katika sura hii, iwapo bajeti ya miaka mitatu kwa taasisi husika imetumia mtindo huu ni dhahiri kwamba katika taasisi hiyo linalopewa kipaumbele ni safari, hivyo vifungu vinavyouliwa kila mwaka huwa havina maana, kwa msingi huu havipaswi kutengewa fedha na kuidhinishwa katika Baraza hili.

Mhe. Spika, Kamati inaomba suala hili lizingatiwe na kutafutiwa ufumbuzi.

4. SURA YA KUSUASUA KWA MASHIRIKA YA UMMA

Mhe. Spika, ripoti zote za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinaonesha hali ya kusuasua kwa Mashirika yetu ya Umma kutokana na tatizo la mitaji, hali ya madeni, mzigo mkubwa wa wingi wa wafanyakazi, tatizo la ushindani na Sekta binafsi na kadhalika. Ni ukweli usiopingika kwamba Mashirika yetu yamepata changamoto kubwa baada ya Serikali kuruhusu mageuzi na kuipa nafasi Sekta binafsi kuendesha Shughuli zinazofanywa na Mashirika hayo, pamoja na ukweli kwamba Mashirika hayo yalibeba jukumu zito la kugharamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika miaka ya nyuma.

Mhe. Spika, katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu, kuna umuhimu kwa Serikali kutafuta na kuharakisha mchakato wa mageuzi yatakayopelekea kufufuka na kuimarika kwa Mashirika yetu, kama vile.

- Shirika la Meli na Uwakala
- Shirika la Biashara la Taifa *(ZSTC)*

- Shirika la Umeme

Pia Kamati inazipongeza Serikali, Uongozi na Bodi za Mashirika ya Bandari, Shirika la Bima, Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)* na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa namna walivyoweza kuimarisha Mashirika hayo na hatimae yakaweza kupata faida na hata kulipa kodi Serikalini. Kamati pia inaishauri Serikali kutafuta namna ya kuangalia hatma ya Shirika la Magari na Shirika la Utalii.

5. SURA YA MADENI KWA TAASISI ZA SERIKALI

Mhe. Spika, sehemu kubwa ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huainisha madeni mbali mbali baina ya Taasisi moja ya Serikali na Taasisi nyengine ya Serikali na baina ya Serikali na Taasisi binafsi. Hali ya kuwepo kwa mlolongo wa hesabu za madeni katika vitabu vya Mdhibiti kati ya taasisi za Umma, sio tu huathiri sura ya Taasisi katika ufungaji wa mahesabu ya Serikali kwa mwaka, lakini pia huathiri utekelezaji wa bajeti ya taasisi husika.

Kamati yetu imeona kuwa msingi wa taasisi kudaiwa licha ya tatizo la athari ya ufinyu wa bajeti lakini pia ni tatizo lililosababishwa na kudharau kuona umuhimu wa matumizi ya baadhi ya vifungu kama vilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

Kamati yetu imelifanyia kazi tatizo hili la mrundikano wa madeni ya muda mrefu kwa kuziagiza Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukaa pamoja ili waangalie namna ya kuyatafutia ufumbuzi madeni ya taasisi ambayo hayana mwelekeo wa kuyalipa (hayalipiki).

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba kazi hiyo imeshafanyika na mchanganuo wa kiwango cha fedha kinachodaiwa, kilicholipwa na kilichobaki na kuonesha anayedai na kudaiwa, umeshakabidhiwa kwa Kamati ya *PAC* kwa hatua ya kufanya mapitio ili baadae Kamati imtaarifu Waziri anayeshughulikia masuala ya Fedha, ili na yeye awasilishe azimio la kutaka ridhaa ya kufutwa kwa madeni hayo yanayofikia Tsh. 444,919,278.67/- mbele ya Baraza hili.

Naomba niipongeze Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya. Pia naomba kutoa wito kwa taasisi za Umma kuwa kufutwa kwa madeni hayo ni sawa na kupiga mstari mwekundu kwa taasisi kuendelea kukopeshana HUDUMA.

Mhe. Spika, Kamati ya *PAC* inasisitiza kuwa madeni yaliyokuwa hayakuingizwa katika orodha hii maana yake hayo yanalipika hivyo Taasisi zitafute namna ya kuyalipa madeni hayo. Aidha, katika namna nyengine ya kuzuia kurudia mtindo wa kulimbikiza madeni, Kamati inapiga marufuku mtindo wa taasisi KUKOPESHANA.

6. UMUHIMU WA KUFANYIKA KWA UKAGUZI YAKINIFU *(VALUE FOR MONEY AUDITING)*

Mhe. Spika, kwa muda mrefu tangu kuanzishwa kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hadi ukaguzi wa mwaka 2008/09, aina ya ukaguzi uliokuwa ukifanywa ni ule wa kuchunguza uhalali wa malipo na matumizi katika taasisi za umma, upungufu wa aina hiyo ya ukaguzi tumeuona.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa bado watendaji wa taasisi zetu hawajaweza kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma licha ya kuwepo kwa ukaguzi, pia kuna umuhimu mkubwa kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuanza aina hii mpya ya ukaguzi kutokana na ukweli kwamba.

- Tasisi nyingi za Ukaguzi wa Fedha za Umma za Kimataifa *(SAIs)* katika nchi mbali mbali zilizoendelea na zinazoendelea zimeshaanzisha kutumia aina hii ya ukaguzi, ukaguzi ambao umeleta faida kubwa na kuokoa fedha nyingi sana za wananchi.

- Fedha nyingi za wananchi hupotea kwa kufanya malipo yasiyolingana na kitu kilichonunuliwa ama ujenzi uliohusika.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nieleze mfano mmoja mdogo sana wa jinsi ambavyo mchwa waliokosa imani wanavyoendelea kumung'unya uchumi wetu dhaifu.

> *"Kuna fundi mjenzi mmoja aliripoti kwangu kwa njia isiyo rasmi kwamba alibahatika kupata kazi ya kufanya marekebisho ya matengenezo ya jiko katika moja ya Mashirika yetu tuliyonayo. Fundi alidai kulipwa jumla ya Tsh 2,000,000/= kama malipo ya kazi yake, kilichomshtusha fundi wakati wa malipo alitakiwa kusaini vocha ya Tsh. milioni 20,000,000/=. Kwa kitendo hicho fundi aligoma kusaini, lakini baada ya majadiliano marefu fundi aliongezwa shilingi laki tano naye akakubali kusaini.*

Mhe. Spika, nimeamua kutoa mfano wa hadithi hii kwa nia ya kuchora picha kwa Waheshimiwa Wajumbe ili wajiulize kwamba ikiwa matengenezo ya jiko yamepelekea wajanja kuramba jumla ya shilingi milioni kumi na nane kwa kazi yenye thamani ya Tsh 2,000,000. Je, kwenye miradi mikubwa ya ujenzi wa majengo, barabara na miradi mingine ya maendeleo ambayo hutumia mamilioni na mabilioni ya shilingi, Taifa letu linapoteza kiasi gani cha pesa kupitia mbinu kama hizi za wajanja?

Mhe. Spika, Zanzibar kama sehemu ya dunia na katika namna ya kufufua uchumi wetu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali lazima aanzishe aina hii ya ukaguzi. Serikali inapaswa kufanya kadri inavyoweza kuiwezesha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutekeleza jukumu hili. Aidha, ili kwenda sambamba na mageuzi haya ya ukaguzi, Serikali na Baraza la Wawakilishi halina budi kuijengea uwezo Kamati ya *PAC* ili iweze kuzitafsiri na kuzifanyia kazi Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa aina ya ukaguzi unaofanywa.

7. MAPITIO YA SHERIA YA FEDHA ZA UMMA, NAMBA 12 YA MWAKA 2005 NA KANUNI ZAKE *(PUBLIC FINANCE ACT. NO. 12, 2005 AND ITS REGULATIONS)*

Mhe. Spika, Kamati yetu inafanya kazi zake kwa kufuata Sheria nyingi ikiwa ni pamoja na Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2005 na Kanuni zake za mwaka 2005. Ni muhimu katika utekelezaji wa kazi kufanya mapitio ya Sheria ili kufahamu mapungufu yanayojitokeza katika utekelezaji wake. Baadhi ya maeneo ambayo Kamati imeona yanahitaji kufanyiwa marekebisho ni haya yafuatayo:

Mhe. Spika, kuna haja ya kuangaliwa upya kifungu cha 25(1) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2005 kinachozungumzia uwezo wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kukagua taasisi zote za umma ambazo fedha zake zinakusanywa na kutumika kwa ajili ya Zanzibar. Utata wa utekelezaji wa kifungu hichi ni kwamba kuna Taasisi za Muungano zenye kukusanya mapato ndani ya nchi yetu ya Zanzibar, lakini Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina mamlaka ya kufanya ukaguzi katika Taasisi hizo, kama vile Uhamiaji Zanzibar na Ofisi za Kibalozi zinazotoa viza kwa ajili ya wageni wanaokuja moja kwa moja Zanzibar. Baya zaidi suala la udhibiti wa ukaguzi wa mahesabu ya Serikali sio suala la Muungano kwani halimo katika orodha ya mambo ya Muungano katika nyongeza ya kwanza wala nyongeza ya pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, suala la ukaguzi kwa vile si suala la Muungano tulitarajia kuwa lingelipewa idhini na Katiba ya Zanzibar kama

vilivyopewa mamlaka vyombo nyengine ambavyo si vya Kimuungano kufanya shughuli zake Zanzibar kama ilivyo katika ibara ya 124(1)(2) ya Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Fedha za Umma kinapingana na kifungu cha 112 (5) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Labda nianze kuonesha kupingana huko. Kwa mujibu wa kifungu cha 112 (5) cha Katiba, baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahakama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi, atatayarisha ripoti na kuiwasilisha kwa Rais.

Mhe. Spika, baada ya Rais kukabidhiwa ripoti hiyo, yeye ndie atakayewaagiza watu wanaohusika (bila ya shaka ni Waziri anayehusika na Ukaguzi na Udhibiti wa Hesabu kama inavyofanyika) waiwasilishe ripoti hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Baraza la Wawakilishi kitakachofanyika baada ya Rais kukabidhiwa ripoti hiyo ambapo itamlazimu aiwasilishe ndani ya siku saba ya kuanza kwa kikao hicho. Tatizo lililopo ni kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2005, kinachomuagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuiwasilisha ripoti hiyo kwa Waziri anayeshughulikia masuala ya Fedha, kwa ufupi tuseme Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo naye kwa haraka aiwasilishe katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mgongano kama huu pia unajitokeza katika kifungu cha 29 (1) (b) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2005, kinachoelekeza kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya ukaguzi aiwasilishe ripoti yake kwa watu watatu, kwanza kwa Rais; pili kwa Waziri anayehusika na masuala ya Ukaguzi na mtu wa tatu ni Waziri anayeshughulikia masuala ya Fedha. Kifungu hichi kwa mara nyengine kinapingana na maelekezo ya Katiba, kifungu cha 112 (5) kinachomtaka Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuiwasilisha ripoti yake ya ukaguzi kwa Mhe. Rais pekee.

Mhe. Spika, aidha, kifungu cha 30 (2) cha Sheria ya Fedha za Umma kinaelekeza kwamba baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuiwasilisha ripoti yake kwa Waziri anayehusika na masula ya Udhibiti na Ukaguzi ambaye kwa mujibu wa kifungu cha 29 (1) (b) cha sheria hiyo, anapaswa (kinyume na maelekezo ya kifungu cha 112 (5) cha Katiba) kuiwasilisha Barazani. Iwapo Waziri huyo atakataa kuiwasilisha ripoti hiyo Barazani, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyo katika muongozo wa kifungu cha 112 (5) cha Katiba, ataiwasilisha ripoti hiyo kwa Spika ambaye yeye ndio ataiwasilisha Barazani.

Mhe. Spika, tatizo lililopo ni kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hapaswi kuiwasilisha ripoti hiyo kwa Waziri, isipokuwa anapaswa aiwasilishe kwa Rais, na kama Rais atakataa kufuata muongozo wa kifungu cha 112 (5) cha Katiba, ndipo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataiwasilisha kwa Spika kwa ajili ya yeye kuiwasilisha Barazani.

Mhe. Spika, hizi ni baadhi tu ya kasoro zinazohusiana na Sheria yetu ya Fedha na Kanuni zake. Kamati yetu inachokitaka hapa ni kwamba Serikali ikae tena kuzipitia Sheria za Fedha kwa makini ili kwanza ziendane na mabadiliko ya Katiba na ziendane na wakati tulionao. Si vizuri kabisa kwa Sheria ama Kanuni kupingana na Katiba, na hili linapotokezea sio tu kuipa Mahakama kazi nzito ya kutangaza ubatili wa Sheria ama Kanuni hiyo ama vifungu vyake vinavyopingana na Katiba, lakini pia Wajumbe wa Baraza lako tunajibebesha mzigo mzito wa lawama kutoka kwa wananchi wetu wa kutuona hatuwajibiki ipasavyo kwa kutunga Sheria zilizo batili kwa kiasi ya kupingana na Katiba yetu.

9. MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA SHERIA YA KUANZISHWA AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

Mhe. Spika, tutakumbuka kwamba mnamo mwaka 2003 tulipitisha Sheria Nam. 11 ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar ambapo tunaipongeza Serikali kwa hatua hii. Hata hivyo, kuna haja kubwa ya kuipitia tena ili tuangalie namna gani Sheria hii inavyokidhi mabadiliko ya kiutendaji na kiteknolojia katika kazi za ukaguzi duniani.

Mhe. Spika, Sheria hii imekosa kutoa maelezo ni kwa namna gani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anavyoweza kuyadhibiti Mashirika, Makampuni na Taasisi za ukaguzi za nje zinazokagua Taasisi za Serikali na hivyo kuikosesha Serikali usimamizi wa uwazi wa mali za umma. (Hapa tusisahau kuwa anayemlipa KABILI ndie anayechagua wimbo). *(Makofi)*

Mhe. Spika, Sheria hii pia kwa mujibu wa Sheria ya Kimataifa imekosa kuainisha moja kwa moja uhuru wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika uajiri, upangaji na ulipaji wa mishahara, mambo ambayo kwa sasa yanafanywa na taasisi nyengine, kitendo kinachokwenda kinyume na Sheria za Ukaguzi Duniani *(LIMA DECLARATION).*

Mhe. Spika, eneo jengine la msingi lililokosekana katika Sheria ni kutokuwepo vifungu vyengine vyenye kutoa maelekezo na ufafanuzi wa kina juu ya uwezo

wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar wa kushirikiana bega kwa bega na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Tanzania Bara katika kukagua Taasisi za Muungano. Hii inatokana na hoja ile ile kwamba suala la ukaguzi si suala la Muungano yaliyotajwa katika nyongeza ya kwanza ya mambo ya Muungano yaliyotajwa katika ibara ya 4(3) Katiba ya Jamuhuri ya Tanzania ya mwaka 1977. Hali ambayo inakosesha Kamati ya *P.A.C* fursa ya kupata taarifa za Ukaguzi zinazohusu taasisi za Muungano kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu Zanzibar kwa vile *P.A.C* inafanya kazi zake kupitia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Zanzibar.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo linakasoro kubwa ni baadhi ya masuala ya msingi ambayo yanayohusiana na kazi za udhibiti kuingizwa katika sheria ya fedha badala ya kuingizwa katika Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar, Sheria Namba 11 ya mwaka 2003 kama Sheria nyengine za Ukaguzi (*Public Audit Act*) zinavyoonekana duniani kote.

HITIMISHO

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kwa kusema kuwa wananchi wenzetu tunao wawakilisha katika chombo hichi kutoka majimboni mwetu ni maskini na wanaelekea kukata tamaa. Tegemeo pekee lililobakia kwao mbali ya kusubiri kudra ya Mwenyezi Mungu, ni uwepo wa serikali makini na inayowajibika kufuatia mageuzi ya kisiasa yaliyotokea nchini ambayo yalipelekea kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Tegemeo jengine, sambamba na hilo ni kwa chombo hiki cha kutunga sheria na kuisimamia serikali. Chombo ambacho kina wawakilishi makini, wenye nia ya kuisimamia ipasavyo serikali kwa faida ya wananchi.

Mhe. Spika, kwa mnasaba wa matumaini waliyonayo wananchi wetu kwa serikali yao, ni wajibu wa serikali sasa kujidhatiti kujenga uchumi kwa kukusanya kodi, kuongeza vyanzo vya mapato na kutafuta mikopo na misaada. Hata hivyo, haitakuwa na maana hata kidogo kama hakutakuwa na matumizi mazuri ya fedha na raslimali za nchi kwa faida ya wananchi. Hii ndio maana ya Utawala Bora.

Mhe. Spika, katika kutekeleza dhana hiyo ya Utawala Bora, serikali haina budi kuiongezea nguvu Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Kamati ya *PAC,* ili ziweze kwenda na wakati kwa kufanya ukaguzi wa kisasa unaozingatia mwenendo wa kimataifa wa ukaguzi wa mahesabu kama vile ukaguzi yakinifu (*value for money audit*) ukaguzi kwa kutumia computa (*Computer Auditing*), Ukaguzi wa Mazingira (*Environmental Auditing*). Ni vyema tukafahamu kwamba dunia ya ukaguzi sasa iko huko na hata wenzetu na ndugu zetu wa Tanzania Bara wameshafika huko.

Narudia tena kuiopongeza Serikali kwa kutandika misingi ya Utawala Bora kwa kuazisha taasisi za kudhibiti na kuchunguza hesabu za serikali, kuweka sheria zinazosimamia mwenendo wa fedha pamoja na kuwepo kwa Kamati za Baraza, zinazofanya kazi za kusimamia mwenendo wa shughuli za serikali.

Mhe. Spika, kwa vile serikali imeonesha nia na dhamira, kilichobaki ni kuwa na UTHUBUTU wa kufanya maboresho ya sheria, kuzipa nguvu na uwezo taasisi husika pamoja na kuwachukuwa hatua za dhati na zilizo wazi, wale wote wanaokiuka maadili na Sheria zetu. Ingawa adhabu zilizomo hazitoshi na zinahitaji kupitiwa upya ili ziendane na wakati na mahitaji, kamati inaitaka serikali izitilie nguvu kanuni hizi ili kupunguza makosa madogo madogo ili yasiweze kujirejea katika ripoti za kila mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Mhe. Spika, naamini kama wanavyoamini wengine kuwa serikali ya awamu ya saba chini ya uongozi shupavu wa Jamedari Dr. Ali Moh'd Shein, kwa upande wa muhimili wa serikali, na Alhaji Pandu Ameir Kificho kwa upande wa muhimili wa Baraza la Wawakilishi watayafanyiakazi yale yote yaliyoshauriwa na kupendekezwa na Kamati ya *PAC*, kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kudhibiti mapato yetu na hivyo kujenga uchumi wetu kwa faida ya nchi na wananchi wetu. Itakuwa si vyema kumalizia bila ya kuupongeza kwa dhati uongozi wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Spika pamoja na katibu, kwa mashirikiano yao yanayoifanya kamati iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Naomba nimalizie kwa kumnukuu mwanafalsafa mmoja aliyesema *"If you don't want to pull a trigger, don't point the gun*"

Mhe. Spika, naomba kutoa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mchangiaji wa mwanzo kwenye kamati hii. Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa nafasi hii.
Kwanza nimshukuru Mwenyekiti, kwa kutoa ripoti hii nzuri kabisa na yenye mwelekeo wa kuisaidia serikali yetu ili tuweze kudhibiti mapato yetu. Mhe. Spika, hii ripoti aliyoisoma Mwenyekiti imemaliza kila kitu. Mimi baada ya kusikiliza basi nimekosa mengi ya kuchangia, maana keshayaeleza yote Mwenyekiti.

Kwa hivyo, mimi nichukuwe nafasi hii kuipongeza Kamati hii ya *PAC* kwa kazi nzuri iliyofanya ya kuyaona hayo na kuyaleta mbele ya wajumbe hapa ili waweze kuyachangia. Niishukuru Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa

Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutuonesha yale mapungufu ambayo yamejitokeza katika matumizi yanayofanywa na watendaji wetu.

Mhe. Spika, niingie kwenye Kamati ya *PAC* kwa kuwashukuru wajumbe wenzangu wa kamati hii kwa mashirikiano tuliyoyafanya mpaka kuweza kuwasilisha ripoti hii leo. Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa yote keshayamaliza Mwenyekiti, mimi nichukuwe nafasi ya kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, nasema naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia kwa mia, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mkwajuni, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kutoa baraka zangu japo kidogo, katika hotuba ya kamati hii muhimu sana ya *PAC*. Mhe. Spika, mimi nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti wa kamati hii kwa namna alivyowasilisha hotuba hii ya kamati ya *PAC*, ambayo ndani yake ina mambo muhimu sana kwa ajili ya nchi yetu.

Mhe. Spika, ninavyoamini mimi na nina hakika kila mmoja wetu ndivyo anavyoamini kwamba moja katika misingi muhimu sana ya utawala bora, basi ni matumizi mazuri ya fedha za umma. Kama hivyo ndivyo, basi taasisi zinazoshughulikia upangaji wa matumizi ya umma na udhibiti wa matumizi ya umma, basi ni taasisi muhimu sana. Nafikiri katika nchi yetu ni taasisi mbili tu zinazofanya kazi hiyo.

Moja ni Baraza la Wawakilishi, ambalo linahusika kupanga na hatimaye kufuatilia. Lakini kuna Afisi ya Mdhibiti Mkuu wa Serikali, yeye kazi yake ni kudhibiti matumizi. Kuhakikisha kama Baraza la Wawakilishi tulivyopanga, ndivyo matumizi yalivyotekelezwa.

Mhe. Spika, kama hivyo ndivyo, basi nadhani ni lazima tukubali kwamba Afisi ya Mdhibiti ni afisi muhimu sana, kwa sababu ndio inayobaini yale mapungufu ya kiutendaji katika matumizi ya fedha za umma.

Mhe. Spika, nilipokuwa naangalia mtiririko wa ripoti za Mdhibiti Mkuu, basi niligundua hilo lipo kweli, kwa sababu katika ripoti yake ya mwaka 2005/2006 aliainisha mule kiasi cha fedha zilizopotea, ambazo kwa kweli ni kiwango ambacho kinatisha kidogo. Katika ripoti ile alieleza kuwa kuna fedha bilioni 1,721,401,530.35/= zimepotea kwa mwaka ule. Pia sambamba na hilo USD 378,844.92 zimepotea mwaka huo huo.

Nilipoangalia ripoti ya mwaka 2006/2007, Mhe. Spika, Shs. 1,273,364,649/= zimepotea na USD 72,893 zimepotea. Ripoti ya mwaka 2007/2008, milioni

269,757,772 zimepotea na mwaka huo huo dolla za Kimarekani 145,480 zimepotea. Sasa Mhe. Spika, hali hii kwa kweli inatisha.

Mhe. Spika, pesa hizi zimepokea kizembe, kwa sababu ukiangalia sababu za kupotea kwake ni kwa sababu ya matumizi yasiyokuwa na stakabadhi, au matumizi yasiyokuwa na vielelezo muhimu ndio humu zinamopotea. Kwa kweli hii hali inatisha, ndio nikasema Afisi ya Mdhibiti Mkuu na ripoti yake ni kitu muhimu sana, kwa sababu serikali inapata kujiangalia wanakosea wapi.

Mambo kama haya Mhe. Spika, yanavunja moyo sana. Mimi nilikuwa naomba haya wananchi wasije wakaambiwa. Maana wakiambiwa kwa kweli watapoteza imani na serikali yao Mhe. Spika. Mimi nafikiri Afisi ya Mdhibiti ni muhimu sana, kama ni hivyo basi hii afisi inahitaji kutunzwa sana.

Mhe. Spika, Mdhibiti Mkuu akishamaliza ripoti yake hatimaye huileta hapa Baraza la Wawakilishi na hatimaye sisi ndio tunaidhinisha yale matumizi. Baraza sasa limekasimu madaraka yake kwa Kamati ya *PAC*. Kwa hivyo, Kamati ya *PAC* nayo inahusika kikamilifu katika udhibiti sasa kwa kupitia ile ripoti ya Mkaguzi Mkuu, kuiangalia mapungufu yaliomo na hatimaye kuiambia serikali kama kazi ambayo kaifanya Mwenyekiti hivi punde.

Mhe. Spika, ripoti ya Kamati ya *PAC* nayo ni muhimu sana kwa sababu nina hakikia kuwa wafadhili wale wanaotufadhili, basi wanaangalia utendaji wa serikali kwa kupitia zile fedha zao walizotusaidia kwa kuangalia hii ripoti ya Kamati ya *PAC*. Nchi nyingi ndivyo wanavyofanya. Wafadhili wakitaka kuona pesa zao zinatumika vizuri au laa, basi ni ripoti ya Kamati ya *PAC*.

Vile vile sio wafadhili tu hata wananchi nao wanataka kujua fedha zao, kwa sababu fedha ni zao si ndio wanaochanga. Kwa hivyo na wao wanataka kujua fedha zao zinatumika vipi ni ripoti ya Kamati ya *PAC* ndio inayotoa kiyoo cha kuangalia mambo hayo. Kwa hivyo, *PAC* nayo ni muhimu sana.

Mhe. Spika, mimi sina mengi ya kusema, lakini nilikuwa nahisi kuna mambo serikali ni lazima iyaangalie kwa upeo wake na iyaangalie kwa nia njema kabisa. Moja ni kumuenzi *CAG* na watendaji wake. Nafikiri wiki iliyopita maswali yalikuwa mengi kuhusu maslahi na kadhalika, mimi nadhani hili ni muhimu sana, pamoja na maelezo ambayo waziri alikuwa akijibu mara kwa mara. Lakini maslahi ya watendaji wa *CAG* ni muhimu sana. Kwa sababu ukitaka kuwadhibiti na wao wasipokee rushwa, basi nina hakika hawapokei, lakini ukitaka kuwadhibiti basi maslahi yao yawe bora zaidi. Kwa sababu siku nyengine wanaweza kwenda kugundua *scandal* kubwa kweli kweli, lakini mtu akataka kuficha mambo yake kwa kumrubuni yule mkaguzi. Lakini ikiwa

maslahi yake ni mazuri na yanamtosha basi sio rahisi kurubunika. Kwa hivyo, nilikuwa nahisi hawa ni watu nyeti na kuna haja ya kuboreshewa maslahi yao.

Jambo jengine muhimu sana Mhe. Spika, ni kwamba Kamati ya *PAC* mara nyengine hulazimika kufanya kazi ngumu sana. Kwa bahati wajumbe wa *PAC* mara nyingi wanakuwa ni wataalamu wa siasa, sio wataalamu wa mambo ya mahesabu nakadhalika. Kwa hivyo, nafikiri kuna umuhimu sana Kamati ya *PAC* kupatiwa mafunzo katika kipindi hiki ambacho wao wapo. Nilikuwa napendekeza Mhe. Spika, kwamba pamoja na *rotation* ya wajumbe kuingia katika kamati hii na hii.

Mhe. Spika, lakini kwa umuhimu wa kamati ya *PAC* nadhani ni vyema wajumbe wa Kamati ya *PAC* wakishachaguliwa wapewe mafunzo, tayari hapo itakuwa ni hatua kubwa sana ambayo serikali imechukua, pengine kwa gharama kubwa, basi ni vyema kamati ile ikabakishwa na kuendelea na miaka mitano mizima, kwa sababu wanakuwa na uzoefu wa kutosha na wanakuwa na taaluma ambayo tayari wameshaipata. Lakini baada ya miaka miwili ukiwaondoa na kuweka wengine, inabidi lazima ufanye kazi tena upya ya kuwaelimisha, kutokana na ule unyeti wa kamati hii. Kwa hivyo, nilikuwa nahisi nitowe hili penginezo na kama litakuwa linafaa, basi lizingatiwe.

Mhe. Spika, suala jengine muhimu sana ni kwamba kamati zako za Baraza kila moja inashughulikia wizara mbili au tatu au kamati ina wizara nyingi basi ni wizara nne. Lakini Kamati ya *PAC* inatakiwa itembelee wizara 16 zote za serikali na mashirika yake, kuna mashirika sijui manane, ni lazima mashirika yote yapitiwe.

Kwa hivyo, hii kamati ina kazi kubwa ya kufanya, nafikiri pia inahitaji muda zaidi. Hivyo, naomba kusema kwamba wiki mbili wanazopewa kamati hii sawa sawa na kamati nyengine, yaani wanazopewa kamati ya hii ya *PAC* kwa kweli Mhe. Spika, hawafanyi hata robo ya kazi ambayo hasa wanatakiwa wafanye. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana kamati hii iongezewe muda.

Mhe. Spika, katika kubadilishana mawazo kamati ya *PAC* na kamati nyengine za *PAC* katika nchi nyengine. Kwa mfano, Kamati ya *PAC* ya Uganda basi iko kazini mwaka mzima haipumziki. Kamati ya *PAC* inakuwa na bajeti yake maalum. Kwa sababu mara nyengine inabidi ikodi au iajiri wataalamu katika fani fulani.

Kwa mfano, sasa hivi dunia nzima kama hotuba ya Mhe. Mwenyekiti, ilivyosema kuwa inaelekea kwenye ukaguzi wa *value for money*. *Value for money* niwe kama Abdalla Juma mjumbe wa *PAC* basi siwezi kwenda kukagua jumba lililojengwa na wataalamu na ma-*engineer*. Kwa sababu sifa ni yangu,

lakini ili kupata kujua thamani halisi ya lile jengo, basi ni lazima nitafute mtu nimkodi mimi. Sasa huwezi kumkodi *engineer* bure ni lazima umlipe. Kwa hivyo, kama kamati ya *PAC* itahitaji kumpata mtu wa aina hiyo ni lazima imlipe na kwa hivyo ni lazima iwe na fungu maalum. Kwa hivyo, nilikuwa naomba katika kazi za *PAC* basi kuwe na mfuko maalum wa kazi hizo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, labda sasa nigusie kidogo mambo mengine katika utendaji wa kamati ya *PAC* ambayo tuliyoyaona kwa kiwango kikubwa ni mapungufu. Moja ni kwamba taasisi nyingi za serikali Mhe. Spika, hazina daftari la kuhifadhia mali za serikali na kutokana na ukosefu huu sasa serikali inawezekana sana haijui mali zake. Kama ni hivyo, basi haiwezi hata kujitathmini na mtaji wa kiasi gani, hilo moja.

La pili, ikiwa *register* kama hili halipo, kuna hatari ya wajanja kujichukulia mali za serikali bila kujulikana na mifano hai ninayo Mhe. Spika. Kule kwetu kuna Sheha mmoja alikuwa na shamba la serikali halipungui heka 10 kaliuza lote, na nina hakika serikali haijui, kwa sababu ile mali haipo ndani ya *register*. Kwa hivyo, hili ni tatizo na katika kufuatilia tuliambiwa kwamba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tayari imeshatoa muongozi wa kutayarisha hilo daftari, lakini ukenda kwa wahasibu wanakuambia wao bado hawajapata huo muongozo. Sasa nilikuwa nasema hili ni tatizo serikali lazima ilione na ilifuatilie kwa karibu sana, mali za serikali Mhe. Spika, zinapotea ovyo ovyo.

Jambo jengine muhimu Mhe. Spika, nafikiri liwe la mwisho hili, ili niwapatie na wenzangu nafasi. Mhe. Spika, ukenda ndani kwenye serikali unakuta serikali iko katika kipindi cha mpito cha kufanyia *reform* taasisi zake nyingi. Sasa *reform* kila taasisi unayokwenda kuna reform. Lakini *reform* hizi Mhe. Spika, zinachelewa sana kutekelezwa. Kwa mfano, hapa tuna nyimbo tunaimba sijui ni mwaka wa ngapi huu tena, kuna *reform* serikali za mitaa mpaka leo bado haijaja juu tukaiona, kila siku *reform*. Pia kuna *reform* ya Shirika la Meli, tumesema sana na bado mpaka leo haijatokea. Kuna *reform* ya *ZSTC* nayo pia haijaja juu mpaka leo na haya mashirika ni muhimu sana, kwa sababu yanasaidia sana uchumi wa nchi.

Kwa mfano, tunaona faida ambayo tunaipata kubwa sana katika ule mfuko wa *ZSSF*. Mfuko ule unasaidia sana serikali kwa sababu uko mzuri. Kuna Shirika la Bandari pia linasaidia sana serikali, pamoja na mapungufu yake lakini linakusanya kwa ufanisi mkubwa. Kwa hivyo, ingekuwa na *ZSTC* inafanya kazi kama hiyo, Shirika la Meli wakafanya hivyo na mashirika mengine basi nafikiri uchumi wetu ungezidi kuimarika. Sasa naiomba sana serikali kwa kupitia taasisi zake zinazohusika au kama ni Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, waharakishe zile fomu ili tuone utendaji unakwenda vizuri.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi fursa hii leo kwa mara ya pili kuzichangia ripoti za kamati mbali mbali. Mhe. Spika, ripoti tunayoijadili sasa, naweza kusema ndio ripoti muhimu kuliko zote katika makati zetu na ni muhimu kwa sababu ndio roho ya shughuli za Bunge popote duniani. Historia ya kuanzishwa mabunge kule Uingereza, basi ilianzia na walipa kodi kutaka wawakilishwe ili wajuwe msingi wa matumizi ya kodi zao, ndio msingi wa ule usemi kwamba "*no taxation without representation"*. Kwa hivyo, nasema kwa sababu ya msingi huo ndio maana nasema, ripoti hii ya *PAC* ni muhimu kuliko zote kwa sababu ndio inayochunga matumizi ya fedha za walipa kodi katika nchi.

Mhe. Spika, baada ya kueleza umuhimu wake huo, naomba na mimi nisisitize kitu ambacho kipo katika ukurasa wa mwanzo wa ripoti hii, juu ya umuhimu na haja ya serikali kupitia wizara mbali mbali, kuzichukulia kwa umakini mkubwa ripoti za kamati zote zinazowasilishwa katika Baraza hili. Kwa sababu kama nilivyosema kuwa hii ni sehemu muhimu sana ya utekelezaji wa kazi za Baraza. Kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar katika mamlaka tatu za dola, Baraza la Wawakilishi ndio mamlaka ya kutunga sheria na usimamizi wa shughuli za serikali. Kamati zao hizo Mhe. Spika, zinapofanya kazi yake ndio zinatekeleza ile moja katika majukumu yake muhimu kabisa ya kusimamia shughuli za serikali.

Mhe. Spika, tumesikitika humu katika baadhi ya sehemu, nilikuwa sikusema kule mwanzo, lakini sasa namalizia naomba niseme kwamba inaonekana serikali mara nyengine katika wizara mbali mbali, haizipi umuhimu wake kiasi ambacho kamati zinapokwenda kufanya kazi yake, idara au ikiwa Katibu Mkuu au mtu mwengine yeyote wa serikali katika wizara ile anayetakiwa kutoa maelezo, basi hata ile ripoti ya kamati yeye hana. Anachukulia kwamba tumeshazungumza ndio tumeshafanya kazi zetu yamekwisha tu. Kwa hivyo, ndio naseme kwanza kuna haja ya kuzipa umuhimu wake.

Katika hilo Mhe. Spika, niseme nimesikitishwa na jambo moja hapa leo. Tangu wiki iliyopita tunajadili ripoti za kamati tumeshuhudia kitendo kimoja kizuri kabisa, kwamba tunapojadili zile kamati za kudumu ripoti zake, basi ile wizara inayohusika mbali ya kwamba kuna waziri wake humu ndani ambaye ndiye anawajibika kwa Baraza, lakini pia wale watendaji wakuu wa wizara tulikuwa tukiwaona kule juu, kwamba walikuwa wanafuatilia umuhimu wa yale yanayoelezwa na kamati ili kwenda kuyafanyia kazi.

Nasikitika Mhe. Spika, kwamba hivi sasa wakati Baraza lako linajadili kamati muhimu kuliko zote, hata wale Makatibu Wakuu basi hatuwaoni kule juu. Najua tutaambiwa kuwa mawaziri wapo wanayachukua, lakini kama ni hivyo, kwa nini wakati wa kupitisha matumizi tunawaona kule juu. Tukipitisha matumizi hawaridhiki kuwa mawaziri wao wapo ndani. Leo tunapohoji matumizi ambapo wao ndio wasimamizi wa matumizi yale hao Makatibu Wakuu basi hatuwaoni kule juu Mhe. Spika. Hili linatusikitisha sana, tunaona ni kiasi gani mawaziri wanaohusika na wizara zao hawazipi uzito unaostahili ripoti za kamati kama hii. Kwa hivyo, naomba suala hili litazamwe kwa umakini sana.

Mhe. Spika, *PAC* ripoti yake imeelezea haja ya kuimarisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa sababu afisi hii na Kamati ya *PAC* ni watoto pacha, wanafanyakazi kwa ukaribu, ni ripoti ya mkaguzi ndio inayowapa nguvu *PAC* kwenda kufuatilia yale mambo ambayo yamekuwa yakijitokeza katika ripoti hii. Sasa nilikuwa namuomba sana waziri anayehusika kwamba hili pendekezo la haja ya kufanya mapitio ya sheria iliyoanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aipe umuhimu wake, juu ya kufanya mapitio ili kwanza kuondosha ule mgongano uliopo baina ya sheria hiyo nambari 11 ya mwaka 2003 na kifungu cha 12 cha Katiba ya Zanzibar. Lakini hata ule mgongano uliopo pia baina ya sheria ya fedha nambari 8 ya mwaka 2005.

Mhe. Spika, sikusudii kutoa maelezo, kwa sababu tayari Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* ameelezea kwa ufasaha na kwa kina kabisa. Namuomba waziri husika na serikali kwa jumla yake ilitazame hili juu ya umuhimu wake wa kuleta mswada wa kuweka sawa mgongano huu ambao unaonekana katika sheria hizi na katiba.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nije katika baadhi ya mambo ambayo yameelezwa humu.

Mhe. Spika, miongoni mwa haya ambalo nataka kulitilia mkazo ni kuhusu suala zima alilolizungumzia Mhe. Mjumbe mwenzangu hapa ni *reform* ambayo hatuioni. Kwa kweli Kamati ya *PAC* imeeleza humu kwenye ripoti yake kwamba yapo mashirika mengi ya serikali ambayo yanaonekana imekuwa ni mzigo, kwa sababu yanashindwa kujiendesha kibiashara.

Mhe. Spika, sasa nadhani wakati umefika kwamba tusiendelee kuziteketeza fedha chache za wananchi wetu ambao ni masikini, kwa kuendesha mashirika ambayo hayana faida kwa nchi. *(Makofi)*

Kwa kweli ninafurahi sana kumsikia Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo anapoyaambia mashirika haya kwamba hatayavumilia ikiwa yanaendelea kuipatia hasara serikali. Lakini tunahitaji kuona na wala isiishie ni kauli tu, isipokuwa tuone na vitendo.

Kwa maana hiyo, hii *reform* tuone kama kuna haja ya kutafutwa *consultant* kwa ajili ya kuyapitia hapa na baadaye tukaletwa ripoti juu ya mashirika yepi yanayojiendesha vizuri yaendelee na yale yanayoitia hasara serikali. Kwa hivyo, yale yanawatia hasara wananchi walipakodi ambao ni masikini wa nchi hii, basi haya yatafutiwe njia ya kubinafsishwa au kama yanafungwa yafungwe.

Mhe. Spika, ulimwengu wa siku hizi kuna *Public Private Partnership*, lakini unaposhindwa kuna *Private Sector* ambayo inaweza kutoa huduma katika maeneo mengi ambayo yanatolewa. Katika suala hili yametajwa baadhi ya mashirika kama vile Shirika la Biashara la Magari, Shirika la Meli na vile vile shirika lililoelezwa kwa maelezo makubwa ni Shirika la Utalii.

Kwanza nadhani kwa umuhimu wa Sekta ya Utalii ilivyo hivi sasa, sioni sababu ya kuwa na Shirika la Utalii katika nchi yetu. Kwa hivyo, ni vyema tungeiachia Sekta Binafsi ikafanyakazi hii na serikali ikakusanya kodi, lakini Shirika la Utalii kwa hasara inayotajwa humu ndani na kwamba inashindwa kukusanya mapato yake ni kuendelea kuiongezea mzigo serikali tu.

Mhe. Spika, kwa ujumla kuna haja Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo haya Mashirika ya Serikali na kutuletea ripoti hapa kwamba yepi yanayofaa kubakishwa nay ale yanayofaa kubinafsishwa.

Vile vile kwenye hayo naomba nizungumzie kuhusu vitu viwili ambayo vinaonekana vinaikosesha mapato serikali pamoja na nchi yetu. Mhe. Spika, kila siku tunalia kwamba nchi yetu ni masikini na serikali yetu ni changa, mpaka wakati mwengine wananchi hufanya mas-hara na kusema hii imekuwa mtoto aliyedumaa itakua lini.

Sasa hapa kuna mambo yaliyotajwa yanayotiliwa mashaka na moja lilizungumzwa asubuhi hapa kuhusu Hoteli ya Bwawani na kwenye Ripoti ya Kamati ya *PAC* limekuja tena Mhe. Spika, nadhani katika sehemu ya kuangalia basi ni hapa.

Miongoni mwa mambo yaliyotajwa ni kwamba Hoteli ya Bwawani imekuwa chaka la kufichia matumizi mabovu ya serikali, wizara, idara, yaani taasisi za serikali zimetajwa humu kuwa zinakwenda kutumia huduma za Hoteli ya Bwawani na baadaye hazifanyi malipo na matokeo yake ni mlimbikizo wa madeni ambayo yanaonekana yapo pale. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba suala ambalo liko kwenye ukurasa wa 150 kwa mujibu wa Kitabu cha Ripoti za Kamati tulizopewa sisi Wajumbe, basi ni vyema kuangaliwa kwa undani jambo hili.

Pamoja na hayo, baadhi ya mifano imetajwa hapa asubuhi katika Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Katika majibu ya Mhe. Waziri kwa mfano katika kumchagua yule ambaye amepewa tenda ya kuendesha *Disco Take*, tumeambiwa ni uzoefu mbali ya kutizama kiwango cha fedha kwamba kuna kampuni ambayo imetoa shilingi milioni 35 kwa ajili ya kulipia na akapewa yule aliyetoa shilingi milioni 15. Lakini Mhe. Spika tunasema uzoefu, sasa huyu aliyepewa miaka 10 iliyopita alikuwa na uzoefu gani, nadhani uzoefu ameujenga pale Bwawani.

Mhe. Spika, sasa kama upo mwengine ambaye anaweza kutupa zaidi kwa nini tusimpe nafasi na yeye, ili serikali yetu ikapata fedha, sasa nalisema hili Mhe. Spika, kwa sababu kuna haja ya kuliangalia kwa undani sana, yaani tuambiwe kuna nini hapa Bwawani hata mambo haya yanafanyika katika hali kama hiyo.

Vile vile mfano mwengine ulitajwa kwenye ripoti ya kamati ile kwamba imekubaliwa hizo shilingi milioni 15, lakini hivi sasa halipi hizo shilingi milioni 15 huyu mwekezaji na analipa shilingi milioni 10 na milioni 5 kila mwezi tunaambiwa zinachangia kufanyia matengenezo.

Kwa upande wa mkataba haukusema hivyo, kwamba serikali au mkodishaji atakuwa yeye mwenyewe anachangia kwenye gharama za matengenezo ya sehemu ile inayohusika. Kwa hivyo, mambo haya kuna haja ya kuyatizama kwa karibu zaidi.

Mhe. Spika, pia kuna suala la Kisiwa cha Changuu limetajwa. Kwa kweli kisiwa hiki wakati kilipokuwa chini ya Shirika la Utalii kilikuwa kinaingiza kwa mwezi Dola elfu 8,000/=, lakini serikali imekikodisha kwa Dola elfu 3500/=. Sasa unajiuliza hapo tunatafuta faida au tunanunua hasara. Kwa hivyo, Mhe. Spika tunaomba maelezo ambalo pia limetajwa kwenye ripoti kwenye ukurasa wa 154. *(Makofi)*

Katika Sekta ya Utalii nimalizie, kuna suala zima la mahoteli haya kuwaajiri wahasibu ambao wanashirika kwenye michezo michafu ya kucheza na mahesabu kiasi cha kuikosesha serikali mapato. Mhe. Spika, nadhani suala hili Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aliangalie kwa ukaribu sana, ili tuone kwamba wawekezaji hawa hawaji kutengeneza fedha hapa na kuondoka na kutuachia mashimo, bali wawe kweli ni wachangiaji

kutokana na uwekezaji wao na kuchangia mapato ya nchi yetu ambayo yatakayosaidia kuimarisha huduma tunazozitoa kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, pia ningeomba nipatiwe maelezo kuhusu suala ambalo limetajwa kwenye ukurasa wa 149 juu ya ununuzi wa gari ambayo ilikuwa itumike kwa Afisa Mdhamini wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko Kisiwani Pemba. Kwa kweli ripoti imeelezwa kuwa gari hii ilikuwa ya serikali na halafu ikauzwa kwa mtu binafsi na baadaye serikali ikanunua kwa mtu binafsi na kupelekwa Pemba kwa ajili kutumika kwa Afisa Mdhamini. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kamati imesema inafuatilia na bado haijakamilisha kwa sababu haijapewa maelezo ya kutosha, lakini nadhani kuna haja ya kulifuatilia isijekuwa kama yale ya *bens* iliyonunuliwa Afisi ya Rais Ikulu na halafu ikajaikaharibika njiani. Kwa maana hiyo, naomba Mhe. Spika, tupatiwe maelezo mazuri kuhusu suala hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 157 pia kuna suala ambalo limenigusa sana linalohusu Idara ya Anga. Kwa kweli idara hii tumeambiwa kuna malimbikizo ya madeni yanayotokana na gharama za utuaji wa ndege pamoja na huduma zinazopewa jumla yake ni shilingi 241,141,778/= na fedha hizi Shirika la *ATC* hilo linalodaiwa, lakini hizi zilikuwa ni jumla katika ya fedha zilizokuwa zikidaiwa mwanzo shilingi milioni 290,799,944/=. Kwa hivyo, kwenye milioni 290 nyengine zimelipwa kwa hesabu za haraka ni kama shilingi milioni 50/= hivi, lakini shilingi milioni 241 zilizobakia kwenye milioni 290 hizi zinadaiwa Shirika la *ATC*.

Sasa sijui kwa nini tunasuasua katika kudai fedha hizi na kuzipata Mhe. Spika, kwa sababu wenzetu hawa wanakuwa wepesi sana kututukana kupitia vyombo vya habari kwamba sisi wanatufadhili umeme unalipiwa na wala hatulipi madeni. Lakini sisi tunayo madeni ambayo tunayadai mashirika yao tunashindwa kuyadai na kuzileta fedha hizi kwenye Mfuko wa Serikali, kwa ajili ya kusaidia kuboresha huduma za watu wetu.

Kwa hivyo, katika hili naiomba Idara ya Anga pamoja na serikali kupitia pia kwako Mhe. Spika, kwamba deni hili shilingi milioni 241 za Wazanzibari tuhakikishe zinapatikana, ili zisaidie kuboresha huduma au kwa lugha ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kuzifanya huduma zetu ziwe bora katika Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la mwisho kabisa kwenye ukurasa wa 169 wa Ripoti hii ya Kamati ya *PAC* umezungumzia suala moja ambalo ni muhimu sana ambalo ni kuhusu utitiri wa ukusanyaji wa kodi. Sasa kwenye maelezo yake imesema

kwamba tayari imeshazungumza na uongozi unaohusika wa wizara, *ZRB*, *TRA* pamoja na wengine wote.

Kwa kweli suala hili ni muhimu likaangaliwa vizuri sana, kwa sababu Zanzibar kimsingi ni nchi ya biashara na kama ni nchi ya kibiashara ambayo inataka kuvutia wawekezaji, basi inahitaji kuwa na mazingira mazuri ya kufanyiabiashara, yaani *Business Friendly Environment* iwepo hapa.

Sasa unapokuwa na utitiri kama ilivyosema mwa na Kamati ya *PAC*, wakusanyaji wakodi inaonekana hata hizo mamlaka zimekiri hilo na kuelezea juu ya haja ya kuangalia upya. Kwa hiyo, tukiwepo kwenye hali kama hiyo hatuwezi kuvutia watu kuja hapa na hasa katika mazingira ya ushindani ambayo tunayokwenda nayo hivi sasa, yaani kila nchi inatafuta kuvutia biashara pamoja na uwekezaji katika nchi yetu.

Kwa hivyo, na hili naiomba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo chini ya Waziri *the most able* Mhe. Omar Yussuf Mzee kupitia kwako Mhe. Spika, basi alitizame kwa umakini kabisa, ili atakapotuletea bajeti yake tukijaaliwa mwezi wa Juni izingatie haja ya kuweka mazingira mazuri ya kuikuza *Private Sector*, ambayo yeye mwenyewe alituambia, kwamba miongoni mwa sababu zilizopelekea mishahara kuwa duni Zanzibar ni kuwa bado wananchi wengi wanategemea ajira kutoka serikali, kwa sababu *Private Sector* haijakua.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema kuwajenga hayo mazingira mazuri *Private Sector*, ili wakue na waweze kutoa ajira na serikali ipate nafuu kuwa ndio mwajiri pekee katika nchi hii, pia iweze kupata kile kichache kiwalipe wengi na tuweze kupata tija kwa wafanyakazi pamoja na wananchi wetu kwa jumla.

Baada ya kutoa maelezo hayo Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema naipongeza tena Kamati ya *PAC*, nawapongeza sana wajumbe wake wote na pia naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Kwanza nimshukuru Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*) kwa kuwasilisha ripoti yake hii.

Vile vile nisiwe mwizi wa fadhila niwapongeze Makatibu wetu wa Kamati hii kwa kutusaidia, wakati tulipokuwa kwenye maeneo mbali mbali ya mawizara tofauti katika kufuatilia kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, *CAG* anayokazi kubwa tena ya lawama. Kwa hivyo, kama walivyokwisha kusema wenzangu kwamba *CAG* apewe uwezo mkubwa wa kuweza kuendesha mambo yake na kwa sababu ni mwanamke mwengangu tena anaonesha uwezo mkubwa.

Kwa kweli siku zote wanawake siku zote tunakuwa ni waaminifu, kwamba mimi mwenyewe kwenye kamati hii ni mzoefu kidogo, kwa sababu kabla ya hapo na mimi yalikuwa yakinikuta haya, kwani mwanzo nilikuwa ni Mshika Fedha karibu muda wa miaka 20 na upande huu wa watu wa *CAG* mara kwa mara tunaonana na wakati mwengine kwa ajili ya kunikagua. Vile vile niseme kwamba wanawake ni waaminifu kwa sababu haikutokea hata siku moja ripoti yangu ikafika hapa ikiwa na matatizo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, niseme kwamba *CAG* nao uwezo mkubwa na pia anahitaji kupewa uwezo zaidi. Kwa mfano, *CAG* anawalea wafanyakazi wake kama ni watoto wake, yaani kusema kweli anajitolea sana, ukienda kwenye ile afisi na katika matembezi yangu ya afisi sijaona afisi ambayo ni nzuri na yenye maendeleo, kwa sababu ndani ya afisi ile kuna utangawazi na kwa kuzingatia ile *value for money*. Kwa hivyo, nimpongeze sana mama huyu kwa kazi zake nzito tena za lawama, lakini anafanyakazi kwa ushupavu sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Afisi ya *CAG* ni *catalyst* ambayo inatu-*speedup* Kamati ya *PAC*. Kwa maana hiyo, hii Kamati ya PAC kwa kuwa tunafuatilia matumizi ya Bajeti ya Serikali, basi ni lazima twende *deep* na tujue fedha za serikali zinatumika vipi kwenye mawizara ama ndivyo au sivyo.

Kwa hivyo, ninaomba kupitia kwako Mhe. Spika, Kamati hii ya *PAC* kwa kuwa si kamati ya kufanyakazi zake katika kuripua tu, basi tunaomba tuongezewe muda, ingawa kila mtu analia mama yangu hapa, lakini na sisi tunasema kamati hii ni nzito na inahitaji kupewa uwezo wa kitaalamu, kwa kuwa kamati hii ina-*deal* na sheria basi tunaomba iongezewe muda wa kutosha, ili iweze kufanyakazi vizuri.

Mhe. Spika, katika kupita kwenye maeneo mbali mbali tumekuta matatizo na hasa ya *reallocation*, yaani unafanya uhaulishaji wa kifungu kimoja na chengine. Kwa kweli niseme na mimi kupitia Ripoti yetu ya Kamati ya *PAC*, kwamba taasisi wakati zinapoleta maombi yao ya vifungu vile basi ni vyema vitizamwe vile vifungu ambavyo ni muhimu visipunguzwe, ili tuondokane na tatizo hili la *reallocation*.

Kwa maana hiyo, kama walivyoelezea wenzangu kwamba tumekuta tatizo la *Fix Asset Register* na wengi walisema kuwa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo haijawapa *format*. Sasa wakati tulipopita mara ya pili

tuliambiwa hiyo *format* tayari imeshatolewa. Kwa hivyo, hivi sasa tunasema wakati tutakapopita tena kwa kesi kama hii, basi Kamati ya *PAC* haitovumilia kuona kwamba mali za serikali zipo tu na wala hazina udhibiti au *register* ya vitu hivi vya serikali.

Mhe. Spika, pia naomba kutoa shukurani zangu ambapo nilikuwa nimesahau. Kwanza kwa kuniteua kuwa kwenye kamati hii nasema nikushukuru sana kwa hilo.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kwa sababu wenzangu mengi wameshayazungumza, basi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii jioni ya leo kuchangia kwa ufupi Ripoti ya Kamati ya *PAC*.

Mhe. Spika, kabla ya kuchangia kidogo naomba niseme mambo yafuatayo. Kutokana na kwamba hivi sasa dunia ni kama kijiji, taarifa ambayo tunaizungumza hapa, basi tujue kwamba haibakii katika jengo hili, yaani inasambaa Zanzibar pamoja na uso wa dunia nzima. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika kamwe tusidhani kwamba Zanzibar kwa sababu ni visiwa yale ambayo tunafanya hapa ndio yatakayobakia kwenye mikoba yetu, kwa kweli yanasambaa na watu wenye macho wanayaona.

Mhe. Spika, yale ambayo Wazanzibari kwa kuwakilishwa na Wawakilishi wao tunayafanya, basi Wazanzibari wanayafuatilia kwa upeo wake. Lakini Wazanzibari ambao wamo ndani na nje ya nchi pia wanaangalia nini Wawakilishi wao wanafanya.

Mhe. Spika, ushahidi wa hayo yale matokeo ambayo juzi tumeyafanya hapa, basi nawaomba wenzangu wakafungue tovuti ya *Mzalendonet* waangalie jinsi ya wenzetu walioko nje walivyotusifu au kutudharau kutokana na matokeo ya juzi.

Kutokana na hali hiyo, natahadharisha kwamba yale ambayo tunayafanya hapa kamwe hayabakii kwenye jengo hili. Kwa kweli Wazanzibari ambao wako nje wanafuatilia nini serikali yao chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohammed Shein inafanya na nini wawakilishi wao wanawafanyia Wazanzibari ambao ni masikini. Kwa hiyo, wakati tunapochangia, tukihoji pamoja na kutetea tujue kwamba Wazanzibari wanaangalia nini wawakilishi wao wanafanya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sisi ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kama utakavyotafsiri sisi ndio wasimamizi wa serikali kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar, sisi ndio ambao tunaidhinisha mipango ya serikali pamoja na kukosoa. Kwa hivyo, lazima serikali itambue kwamba kuna umuhimu wa kusikiliza na kufuatilia maagizo ya Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Kwa kweli nasikitika sana watendaji wa serikali siku za bajeti wako tayari kukufuata Mwera, ili uwasaidie bajeti yao ipite, lakini siku ya ripoti wanasahau na hii ni jeuri, kwa sababu hawana shida tena. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kadri tunavyokaribia mwezi wa Juni, basi watendaji wa serikali watakuwa karibu na sisi, kwa sababu wanataka tuwapitishie fedha zao na wakafanye wanavyotaka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kupitia kwako Mhe. Spika kwamba dawa ya jeuri ni jeuri au mtu akikudharau basi na wewe mdharau na wala usimtukane. Kwa maana hiyo, kama watendaji wanatudharau basi na sisi tuwadharau na tuangalie nani mwenye dharau kubwa baina ya sisi na wao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya utangulizi wangu huo sasa niende kwenye ufutaji wa madeni. Kwa kweli kuna haja kwa serikali kuangalia taratibu za ufutaji wa madeni, Sheria ya Fedha imeweka taratibu za jinsi ya kufuta madeni ya serikali, lakini tumegundua kwamba baadhi ya taasisi hukaa tu kwenye meza na kufuta madeni, jambo ambalo linakwenda kinyume kabisa na taratibu za Sheria ya Fedha ya ufutaji wa madeni. *(Makofi)*

Mhe. Spika, athari ya jambo hili ni kwamba zinaendelea kuua Taasisi na Mashirika ya Umma. Tabia ya mashirika na taasisi za serikali kukaa kwenye meza na kufuta madeni ni tabia ambayo kwa kweli inaumiza nchi yetu na zaidi inaumiza wananchi wetu.

Kutokana na hali hiyo, naomba kupata majibu Mhe. Spika, kwa sababu tumekuwa tukihoji muda mrefu kwamba Shirika la *ZSTC* inaidai serikali zaidi ya shilingi bilioni 4, lakini kwa mujibu wa Ripoti ya *PAC* eti wamelipwa bilioni 1 na nusu na nyengine wameombwa zifutwe.

Sasa tabia hii ya serikali kuu inakopa kwa mtoto wake na baadaye wakeshakuona deni ni kubwa waambiwa futeni, nadhani hatuna lengo la kuyaendeleza mashirika haya. Kwa maana hiyo, Mhe. Spika mashirika haya maisha hayataleta tija kwa wananchi wetu na zaidi yanatia hasara na kuwalipa watu misha hara ambayo haina kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani kama serikali iko tayari kubaki na mashirika haya, basi lazima nidhamu ya ukopaji na urejeshaji wa madeni itumike, vyenginevyo mashirika haya naungana na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba yafutwe na wala yasiongezee mzigo serikali pamoja na kuongeza mashaka kwa wananchi wetu wanyonge ambao hali zao si nzuri sana.

Vile vile kuhusu suala la Afisi ya *CAG* ni muhimu sana na lazima tukubali kwamba tuongeze uwezo wa vitendeakazi pamoja na utaalamu. Mhe. Spika, ikiwa kweli tunahitaji kupatiwa usalama wa nchi yetu kifedha, basi lazima afisi hii iongezewe utaalamu pamoja na vitendeakazi, vyenginevyo itakuwa ni nadharia zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaomba Kamati ya *PAC* ipatiwe mafunzo zaidi pamoja na kuiongezea muda na mimi niko kwenye Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii na wala sina tatizo. Kwa kweli Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii wiki zangu mbili zinanitosha, lakini Kamati ya *PAC* nakuomba sana uiongezee muda, ili waweze kuchunguza jinsi gani serikali inafanya.

Kamati ya *PAC* ni wajumbe wake ni wanasiasa na hawana wataalamu wa fedha, sasa wanakwenda kuwachunguza watu wenye utaalamu wa fedha, yaani wanajua kila mbinu ya kutafuta fedha kwa njia halali au si halali, kwa hiyo wiki moja au mbili hazitoshi kwa ajili ya kufanya kazi zao. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ni vyema kuiongeza muda kamati hii Mhe. Spika, vyenginevyo tutakuwa tunafanya mambo ambayo si sahihi, kwa sababu wataalamu ambao tunakwenda kuwachunguza ni wataalamu wa fedha. Kwa mfano, Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yussuf Mzee wanaijua fedha *A to Z*, sasa unampeleka Mhe. Abdalla Juma Abdalla Mwalimu wa Dini hawezi siku moja kumchunguza. Kwa hivyo, lazima muda uongezwe Mhe. Spika pamoja na utaalamu na ikiwezekana basi ni vyema tuwape na Askari Polisi wafuatane nao. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, Baraza lililopita nilikuwa kwenye Kamati ya *PAC* tulikwenda Afisi ya Baraza la Manispaa, basi mtendaji baada ya kujibu hoja anacheka tu, inamaana tayari ameharibu kwa sababu hajibu hoja yeye alikuwa akicheka tu na matokeo yake watu wote walicheka. Kwa hiyo, nadhani ni vyema Kamati ya *PAC* ipewe Askari Polisi na kwa yule mwenye kuharibu basi achukuliwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna msemo wa Kiswahili unaosema hivi “Ukimuonea haya mke ndugu basi huzai”. Kwa hivyo, kama Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohammed Shein anataka nchi hii kuwaokoa Wazanzibari, basi lazima akubali

pamoja na serikali yake kufanya haki na lazima tufuatwe sheria na wala huruma haiji kwenye kutafuta haki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakuomba pamoja na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi, kwa sababu yeye ndiye msimamizi wa serikali hii humu ndani, basi aangalie maagizo hayo ya kamati pamoja na wajumbe kwamba lazima watendaji wetu tuwashughulikie kwa mujibu wa sheria na kanuni, ikiwa tunaoneana haya basi nafikiri itatuulia nchi na wananchi wetu maisha wateendelea kuwa masikini.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa 146 kwamba Kamati ya *PAC* imebaini kwamba pale inapokwenda kukagua mahesabu, basi vielelezo hakuna, lakini wanapohoji *PAC*, siku ya pili vielelezo hupatikana. Sasa unajiuliza mwaka mzima idara imeshindwa kupata risiti na kesho asubuhi risiti inapatikana maana yake nini, hapa kuna wizi, maana yake kuna duka ambalo risiti ambazo si sahihi zinachukuliwa. *(Makofi)*

Kwa kweli haiwezekani kama watu wako makini mwaka mzima wanakosa risiti lakini Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*) anapata risiti mpya, yaani ukiinusa ni mpya kabisa. Kwa hivyo, lazima tuwe makini sana, ikiwa hoja imekosekana mwaka mmoja basi hoja hiyo imekuwa ni hoja, yaani huyo mtu ameharibu na lazima ashughulikiwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine kwenye ukurasa 170 na hoja hii niliikuta mwaka 2009, kwamba kulikuwa na mgongano baina ya Afisi ya *CAG* na *ZRB* kuhusu mapato yaliyopotea kwenye Hoteli ya *Vera Club*. Mhe. Spika, nakumbuka wakati nilipokuwa Kamati ya *PAC* kipindi hicho, kwamba *CAG* walidai kuwa mapato yalivuja na *ZRB* ambao tunawategemea ambao ndio wasimamizi wa kodi wao bado walikuwa wakitetea na kuona kwamba *CAG* ni muongo.

Mhe. Spika, kwa asilimia 90 na zaidi *CAG* haandiki mambo ya kubahatisha, yaani ni wataalamu yenye uwezo hata akisema kuwa Mhe. Hija Hassan Hija amepoteza, basi amepoteza na wala hawamuoneni mtu *CAG*. Kwa hivyo, lazima tuseme kuwa mapato haya Mhe. Spika, *ZRB* walieleze yamekwenda wapi tokea mwaka 2006/2007 mpaka leo hoja hii inaendelea, basi watueleze *ZRB* mapato haya yamekwenda wapi na sio wakae na kujenga hoja kwamba pengine *CAG* ulikosea na ulisahau, hakuna kusahau katika majukumu ya watu. Kwa maana hiyo, Mhe. Spika watueleze *ZRB* mapoto hayo yamekwenda wapi, ili Wazanzibari waridhike kwamba mapato haya yalikuwa halali au yamepotea.

Mhe. Spika, baada ya hayo, niseme kwamba serikali lazima itufanyie haki kwa niaba ya wananchi na wakubali pale tunapohitaji kuchunguzwa, kwa sababu

mtu kama hana kosa asiogope kuchunguzwa atasafika tu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya *PAC*. Mhe. Spika, kwa kweli kila mjumbe anayesimama hapa anaelezea kuhusu jinsi gani ya kuweza kuimarisha hii kamati kwa ajili ya kuleta ufanisi za kazi zake nzuri.

Kwa kweli Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*) wakati alipokuwa akiwasilisha alisema kwamba kuna upotevu wa fedha ambazo ni nyingi tu. Lakini kinachosikitisha ni kuwa mpaka leo hao watu bado hawajakamatwa, upotezaji wa fedha umeonekana, yaani Kamati ya *PAC* imeona, lakini waliopoteza mpaka leo bado hawajakamatwa Mhe. Spika jambo hili linasikitisha sana, kwa nini wasikamatwe. *(Makofi)*

Kwa mfano, wenzetu Bara juzi Mhe. Spika, nilikuwa nikimsikiliza Mhe. Augustine Liatonga Mrema ambaye ni Mwenyekiti, basi walitoa amri pale pale na Mkurugenzi wa Halmashauri akamatwe na mshahara wake ukatwe na sisi tunaogopa nini. Mhe. Spika, ndio maana tukasema kwamba Kamati ya *PAC* lazima ipewe Askari Polisi, kwa sababu ikigundua basi pale pale anatiwa pingu kwa sababu ni mwizi, tena fedha za wajuja jasho nasikitika sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wazee wetu wanajikakamua, wanapoteza muda pamoja na mambo mengine mbali mbali, hatimaye zile fedha tunakwenda kumpa mtu ambaye amevaa suti na kuzitumia bure bure na sisi hapa tumekaa viongozi na wala hilo haliwezekani. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, ni vyema kuiangalia Sheria ya Kamati ya *PAC* nafikiri ina mapungufu, kwa sababu kama tutaifanyia marekebisho vizuri pamoja na kuiandaa vizuri na wengine wamesema taaluma, jambo ambalo ni muhimu na wengine wamesema muda, yaani muda wa wiki mbili hautoshi na hili pia tuliangalie.

Kwa mfano, wenzetu nchi za nje wanapewa muda wa mwaka mzima Kamati ya *PAC* na fungu lake lipo chini ya kwapa na mshika fedha wake yupo. Lakini kamati yetu sisi inapewa wiki mbili tu na imetusaidia pahala pakubwa sana, kwa sababu imegundua kuna Afisi ambazo tayari zimeshakopesha zile pesa.

Mhe. Spika, mimi nimesema nianzie hapo kwamba upotevu huu wa pesa kwa kweli inatia huruma kwa sababu ni pesa za wavuja jasho kwa hivyo tuiangalie *PAC* vipi itaweza kusaidia sheria, ili waweze kuwa na nguvu ya kuweko na polisi mtu atiwe pingu pale pale anayegundulikana.

Mhe. Spika, kwa nini *PAC* tusiipeleke nchi za nje kwa muda wa wiki mbili, mwezi mzima au mwaka mmoja ikenda kuviva tu, tunaona kama kitu joki tunapiga mabao lakini ni *serious* lakini hatari yake iko mbele kwa sababu *PAC* haina taaluma kiasi hicho. Lakini Mhe. Spika, fumba macho toa fuko lako hilo wape hawa na kwa kuwa nasema hili sio kwamba na mimi nitakwenda kwenye safari aa? mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Majenzi lakini kwa umuhimu tuwajengee hawa hali halisi ilivyo, lazima tuwapeleke nje kwa muda wa mwezi au mwaka mzima wakirudi watakuwa wameshawiva kitaaluma hiyo japo mishahara tukate lakini tuwapeleke.

Mhe. Spika, kuna deni hili ambalo limezungumzwa la *ZSTC* na wizara ya fedha, nakumbuka huko nyuma walikubaliana kuwa wabadilishane wale walioanguka kwenye mkarafuu watalipwa na wizara ya fedha, sasa Mhe. Waziri nataka anieleze hili suala ni kweli na kama ni kweli mpaka leo wananchi wetu wanaanguka kwenye mikarafuu hawajalipwa hizi fedha na suala hili tayari wameshalibeba wao. Sasa na hili Mhe. Waziri aje kuniambia kuwa ni kweli na muda upo sasa hivi au siku yoyote wataweza kulipwa ili na wale watu walioumia kule waweze kufaidika, kwa sababu kama hatukuwalipa karafuu hazitachumwa tena, Kwa kuwa tumewekeyana tathmini huko nyuma kwamba anayeanguka anapigwa tathmini na kuweza kulipwa jinsi alivyoumia viungo vyake, sasa leo tukisema tuiondoe hiyo itatupa hasara kubwa sana Mhe. Spika.

Lakini katika hizi sheria zetu za wakurugenzi au waziri katika utumiaji wa fedha mimi nafikiria kunakuwa na *limit* ya kiwango cha chini kuliko kiwango cha juu hebu na ii sheria tuitizame, kwa sababu tayari hawa watu wanavuruga mali tu. Utakuta mtu hana uwezo wa kutumia milioni arubaini yeye anatumia bila ya idhini ya aina yoyote nayo sheria hii tuiangalie kama imepitwa na wakati basi mimi naomba waheshimiwa tuiboreshe, au tuitengeneze vizuri ili ilete ufanisi mzuri katika ulindaji wa fedha zisipotee kiholela.

Mhe. Spika, tuna hoteli yetu ile ya *VENTA CLUB.* Kwa kweli ukienda inasikitisha tumeshakosa pesa nyingi pale na tunadai nyingi sana. Lakini hatua mpaka sasa hivi sijasikia nashukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ameunda kamati hiyo na *stage* ya mwisho mpaka sasa hivi hatujasikia imefikia wapi. Lakini ninavyofikiria imo katika harakati za kuweza kulimaliza hili suala kwa sababu pale kuna pesa zetu za kodi. Umeme wanadai, maji wanadai, kodi ya mapato wanadai pale na wananchi wetu wanadai pale. Basi mimi ningeomba tu hili suala tuharakishe ili tuweze kupata kodi zetu zote hizo na wale wafanyakazi wakaweza kulipwa nalo hili naliomba kwa Mheshimiwa mhusika aliangalie hili suala la kuweza kufanya harakati ili wale wananchi wanaodaiwa

wengine na wameshapelekwa Mahakamani. Wengine wanaogopa kuacha deni la mzigo mzito kwa wale waliokuwepo.

Kama leo nilivyosema kwamba sitakuwa na maneno mengi ya kukuchosha wewe, Kwa hivyo kwa kumalizia Mhe. Spika, wale waliopoteza fedha zetu za umma wadhibitiwe mara moja. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikazungumza machache sana, mimi nataka niipongeze kamati ya *PAC* kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ukiangalia ripoti za kamati kwa kweli wamejitahidi sana na wanastahili pongezi.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja kwa *CAG* na mimi kama alivyosema jirani yangu hapa Mhe. Fatma Mbarouk Said nataka nimpongeze sana mama huyu ambaye amekabidhiwa jukumu zito la kuangalia na kusimamia matumizi ya serikali na fedha za umma hazipotei.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana na vifungu vya kamati kwa hivi vifungu vya sheria ambavyo vimetajwa katika ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati upo umuhimu mkubwa sana wa kuweza kuangalia upya na kuweza kufanya marekebisho ili huyu mdhibiti wa fedha za serikali aweze kufanya kazi zake vizuri na kwa uwazi kabisa na bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Spika, hivi karibuni tulizungumzia suala zima la utumishi wa umma na katika sheria ile tulijaribu sana kumlinda Katibu Mkuu Kiongozi kwa kuangalia maslahi yake pale wakati anapostaafu, nadhani kumbe ilikuwa kuna na umuhimu mwengine mkubwa sana wa kumuangalia *CAG* vile vile na yeye maslahi yake pale wakati anapostaafu. Huyu mwenzetu tumemtwika mzigo mkubwa sana wa fitna mzigo ambao wenzako wameshatumia wewe unakwenda kuwaambia umetumia vibaya. Huyu mwenzetu baada ya kustaafu anaweza kukosa hata jirani wa kuzungumza naye, kwa sababu mazingira ya kazi yake huyu anakosa jirani.

Sasa mimi nadhani lazima tujaribu kuangalia upya sheria zetu tumeweke *CAG* katika mazingira ambayo hata akistaafu kazi basi hata kama atazongwa zongwa awe hana ulazima wa kumuangalia jirani. Mhe. Spika, sasa mimi nadhani suala hili tuliangalie kwa upeo katika hayo marekebisho yatakayokuja basi nadhani na umuhimu wa kumlinda *CAG* kwa kweli tuweze kuyatia maanani sana.

Mhe. Spika, nataka nimpongeze *CAG* na afisi yake nzima, Kama Ofisi ya *CAG* haina macho basi wajumbe wa kamati ya *PAC* hawataona chochote. Kwa hivyo katika ripoti hii ubora wake wote unatokana na umahiri, ukweli, uwazi na

uchungu wa *CAG* pamoja na watendaji wake kuonyesha wenzetu Kamati ya *PAC* ni maeneo gani ambayo wanatakiwa kuyafanyia kazi.

Mhe. Spika, suala la mafunzo ni muhimu sana katika kamati au katika eneo ambalo linatakiwa yatoke mafunzo mengi. Katika hii kamati yetu ya *PAC* kuna watu ambao wamebobea katika mambo ya mahisabu, wameshakaa vyuoni zaidi ya miaka kumi, wewe mwanasiasa umetoka darasa lako la saba la mkoloni ukweli utadanganywa na wala huoni kitu. Sasa ndio maana tukasema kwamba kuna umuhimu wa kutoa mafunzo makubwa kwa wajumbe wa Kamati ya *PAC* kwa kweli una umuhimu mkubwa.

Lakini Mhe. Spika, nataka nitofautiane kidogo na rafiki yangu na swahiba wangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu alivyosema kwamba kamati hii ni muhimu kuliko kamati zote si kweli. Mimi ni mwenyekiti wa kamati ya kushughulikia Afisi za viongozi wa kitaifa hii kamati yangu ni muhimu kweli kweli na ina kazi muhimu kweli kweli. *(Makofi)* Mhe. Spika, sio kwamba najitetea lakini tunajaribu kuangalia umuhimu wa kila kamati katika yale maeneo ambayo inayafanyia kazi, vyenginevyo kamati nyengine mnaweza kuja kuzifuta.

Mhe. Spika, mimi nataka vile vile wenzangu wa kamati ya *PAC* wajaribu kuangalia kuna eneo moja ambalo tunahisi mali za serikali zinapotea. Kuna baadhi ya waheshimiwa nadhani walizungumza wakati walipokuwa wakichangia ripoti ya kamati ya Maji, Ujenzi kwamba kuna mashamba mengi ya serikali hayajulikani, watu wanavuna utafikiri mashamba ya baba zao. Hii ni mali ya umme kwa hivyo mimi naomba sana wenzetu wa kamati ya *PAC* hebu tujaribu katika ripoti za kamati zinazokuja tujaribu kuchungulia na huko tuone ni rasilimali gani za serikali ambazo zinapotea. Hili ukijaribu kulifuatilia kwa undani kuna baadhi ya mashamba ya serikali unaambiwa haya ya kilimo, ukienda kilimo wanasema haya ya Ardhi.

Mimi nadhani taasisi mbili hizi kuweza kukaa na kujua haya mashamba ya serikali kwa sababu haya mashamba mengine yana mazao kuna miembe, kuna minazi, kuna mikarafuu utamkuta mtu kaweka majanvi hapo utafikiri karafuu zake kumbe shamba la serikali na hakuna mtu yoyote ambaye anamhoji. Kwa hivyo mimi nadhani bado upo umuhimu wa kuangalia maeneo mengine ambayo serikali inaweza kukusanya kodi.

Mhe. Spika, vile vile katika eneo hili la wawekezaji bado kuna maeneo yamekaa kwa muda mrefu na sijui sheria zetu za ardhi zinasemaje, kuna maeneo yamekaa muda mrefu yamezungurushwa makuta yanaota mwani watu wanataka ardhi kwa ajili ya kuwekeza hawapati kuna makuta mbayo hayaingizi chochote serikalini, mimi nadhani huu ni upotevu wa mali za umma. Makuta haya kama wangelikuwa wawekezaji ambao wako tayari kuwekeza basi

nadhani serikali ingekuwa inakusanya mapato na vile vile kutoa ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, mimi huenda nikajazuia bajeti ya Wizara ya fedha. Mhe. Omar Yussuf Mzee ni rafiki yangu tena nampenda sana na ndio maana huwa natoa indhari kabla mambo hayajaanza kutokea, Shirika la *ZSTC* mimi sikubaliani na wazo kwamba shirika hili pesa wanazodai serikalini wasamehe haiwezekani.

Kama hili ni shirika la serikali basi serikali ilikuwa inatakiwa itafute fedha kwa ajili ya kuliwezesha shirika hili lifanye kazi zake vizuri, leo inakuwaje shirika linadai halafu serikali iseme kwamba hawalipi italipa. Mimi sitapitisha bajeti ya wizara ya fedha kama fedha za *ZSTC* hawajalipa, kabla hamjanipeleka huko mbele mwanzo nilikuwa nyuma na huku nyuma nilikuwa nikicheza vizuri.

Kipindi hicho mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi tulitetea sana shirika la *ZSTC* na tulitetea kwa sababu gani, *ZSTC* wakati wa msimu wa karafuu wanakwenda *PBZ* kukopa na pale ile *deposit* tu peke yake ni milioni hamsini, halafu milioni hamsini yenyewe hairejeshi kumbe wanaidai serikali karibu bilioni tano. Sasa huu sio uonevu hili shirika si tunaliua wenyewe. Mimi bado sikubaliani na mawazo ya serikali kusema Shirika la *ZSTC* fedha zake wasamehe, hata hao wananchi wetu tunawatia unyonge kwa nini, unapofika msimu wa karafuu zinakuwa nyingi shirika halina pesa linakwenda kukopa *PBZ* wakati serikalini kuna pesa inadai.

Sasa utakuta inafika pahala *ZSTC* wameshazinunua karafuu nyingi. Zile fedha zinakuwa zina riba. Ili ile riba isiongezeke, inabidi zile karafuu wauze kwa bei ya hasara, ili kuweza kulipa kwa wakati lile deni. Wakati ule ule karafuu hizi kama wanaweza kustahamili ndani ya miezi sita, bei inapanda kwa ghafla wanauza bei mara mbili. Kwa maana hiyo, hili shirika lina uwezo wa kujiendesha kumbe tunaliua sisi wenyewe. Tusigeuke wanga kuua watoto wetu tuliowazaa. Mheshimiwa, Shirika la *ZSTC* bilioni tatu na nusu zilizobakia muwalipe *(Makofi)*

Mhe. Spika, kidogo mimi nilikuwa nataka nipate ufafanuzi najua umeshakamata maiki yako, leo Mhe. Waziri wa Mawasiliano alipokuwa anazungumza kuhusu barabara kuchelewa, alizungumza kwamba kuna mambo mengi yanayochangia, pengine kuna nyaya za umeme, kuna mabomba ya maji. Sasa mimi najiuliza suala moja kwa sababu serikali inapotia mikataba katika ujenzi wa barabara kama hizi tunajua kuna uchambuzi yakinifu umeshafanywa na mle kutakuwa na mambo kama hayo ya mabomba ya maji na kuweka nyaya za umeme, sasa hii miradi inapochelewa je, serikali inakuwa haingii hasara kwa sababu ina maana mradi unapochelewa hata zile fedha mlizokubaliana pengine zinaweza kuongezeka kitu kama hicho. Sasa hapa nauliza kwa kuangalia hii

value for money. Je, hii miradi kuchelewa chelewa kwa muda mrefu hii *value for money* inapatikana vizuri.

Mhe. Spika, namalizia malizia tuangalie sana haya majengo yetu hasa mapya tunaponunua fanicha, tuangalie sana kamati ya *PAC* katika manunuzi ya fanicha hasa katika majengo yetu mapya. Tunashukuru sasa hivi serikali imeshaanza mpango mzuri wa kuanza kujenga majengo yake tunawapongeza kwa sababu hatutaki tena kuendelea kukaa kwenye yale mejengo ya kurithi. Lakini majengo haya baada ya kumaliza yatahitaji fanicha. Mhe. Spika, mfano mzuri ulitokea humu humu ndani tulililetewa viti hapa kila ukizidi zaidi ya kg. 80 basi utakwenda zako chini, bahati nzuri vikang'olewa tukaletewa vyengine hivi hapa hata ukiwa na tani tatu hapa wewe utazunguruka zunguruka tu.

Mhe. Spika, sasa hili limetokea hapa kwetu kama lingetokea kwa wenzetu ingekuwa ndio imetoka jengo zuri lakin vitu bwagire bwagire maneno ya kikwetu shamba kule.

Mhe. Spika, nikimaliza dakika yangu moja iliyobakia nataka nizungumzie kamati ya *PAC* mimi nilipata taarifa hivi karibuni katika haya majenereta yetu ya umeme. Tumeambiwa majanareta yale kuna karibu sita au saba ni mabovu hebu fuatilieni kama kweli mabovu. Je, hii *Volue for money ina- apply* pale, kwa sababu maeneo kama haya ndio ya kujaribu kuangalia kwa sababu kama sasa hivi umeme unakatika tunategemea zile janareta za akiba zifanye kazi, kumbe tunaambiwa majeneta mabovu. Sasa tujaribu kuangalia huko ndani pengine hiyo *volue for money* labda kuna panya wameingia kwenye majenereta.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache nakushukuru mengine yaliyobakia nitakuja kuzungumza kwenye bajeti kuu ya serikali. Nakushukuru Mhe. Spika. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru sana na mimi kwa kunipatia hii nafasi. Lakini pili nataka niipongeze sana kamati ya *PAC* inayoongozwa na Mhe. Omar somo yangu kwa kazi nzuri anayoifanya, nataka niwahakikishie waheshimiwa wana kamati, kwamba ripoti yao nimeisoma yote na nimeyaelewa yote. Nataka niwaambie tu kwamba nitafanya kazi karibu na kamati yao kwa faida ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na michango miwili midogo sana. Kwanza nataka niwahakikishie na niwaambie waheshimiwa wajumbe kwamba muongozo kwa ajili ya usajili wa mali za serikali tayari tumeshautoa kwa taasisi zote za serikali na tumewapa *dead line* mpaka mwezi wa Juni, iwe taarifa zote tumeshazipata,

kitakachotucheleweshа na hicho tumekubaliana kwamba hatutakifanya baadaye taratibu ukishakuijua mali yako iko wapi na mali yako ipi. Tutafanya taratibu kujua tathmini hasa ya ile mali ina milki kiasi gani hicho tutakifanya taratibu. Lakini muongozi tumeshautoa na Juni tumewaambia ni *dead line*, kama kuna Mhashibu ambaye hana muongozo basi tunamuomba afike pale Hazina ile aje achukue muongozo.

Mhe. Spika, la pili ambalo nilikuwa nataka nilizungumzie kidogo kuhusu habari ya mashirika ya umma. Kwanza nataka nimuombe sana sana Mhe. Hamza Hassan Juma ndugu yangu, mdogo wangu na rafiki yangu itakapokuja bajeti yangu asiizuie anionee huruma na upya wangu. Lakini nataka niseme mashirika haya ya serikali yalikuwa mengi. Sote sisi ni Wazanzibari na tunayakumbuka tumeanza kuyabinafsisha mengine na sasa tumebakiwa na mashirika manane. Lakini haya mashirika manane mengi yao hayafanyi vizuri, hayafanyi vizuri kwanza mengi yao yana matatizo ya mitaji kama ilivyoelezwa. Mengine yana wafanyakazi wengi lakini mengine yameshindwa kushindana na sekta binafsi. Tulichokifanya serikalini tunalipitia shirika moja baada ya moja kuangalia jinsi gani tutakavyoweza kulifanyia marekebisho, kama shirika hilo litakuwa na mwelekeo wa kufanya kazi kama Shirika sio kama Idara ya serikali.

Mhe. Spika, nathubutu kusema tumeanza na *PBZ* tumeifanyia *reform* kubwa sana na serikali imetumia zaidi ya bilioni nne kuifanyia *reform PBZ retrenchment* pamoja na a*utomation* leo *PBZ* ni shirika moja linalopigiwa mfano sasa, lakini vile vile nataka niseme *ZSTC* tayari, maelekezo ya kulifanyia *reform* yameshatolewa na serikali na kazi tumekabidhiwa wizara tatu, Wizara ya Biashara na Viwanda, Wizara ya Utumishi na Wizara ya Fedha, tayari tumeshakabidhiwa kazi na shirika hili linaweza likaitaka serikali ilipie *reform* zao sio chini ya bilioni tatu.

Mhe. Spika, pale ndipo ninapotaka kumwambia ndugu yangu kweli haya mashirika tulipoyaunda Mhe. Spika, lengo lake ni kuchangia bajeti ya serikali haya mashirika hayakuwa yakichangia kabisa. Yamekwenda mwisho akasema hata kodi yalikuwa hayalipi wakiingiza vitu hakuna kodi wanapewa misamaha. Mwaka 2005 Baraza lako tukufu tumefanya marekebisho ya sheria. Tukasema sasa mashirika yasichangie *up grant* kwenye bajeti ya serikali lakini yalipe kodi, wanapoingiza bidhaa kama ni kulipishwa kodi walipishwe kodi mashirika haya hayakuwa yakilipishwa kodi yakiingiza misamaha.

Mhe. Spika, nilipoingia nikawaambia natumia sheria na marekebisho ya sheria ya mwaka 2005 nikayaomba mashirika kuanzia sasa yatakuwa na wajibu wa kulipa kodi pale panapolazimika kulipa kodi. Mtoto anapojituma ndipo unapoona faida yake haya mashirika yalikuwa hayajitumi. Sasa nataka

nimwambie Mhe. Hamza Hassan Juma asizuie bajeti yangu kwa sababu *ZSTC* atahitaji kutoka serikalini si chini ya bilioni tatu, katika *reform* ambazo tayari tumeshakabidhiwa na serikali wizara tatu, kuna *reform* ya wafanyakazi, kuna *reform ya automation*, kuna majukumu mapya ya *ZSTC* ndio maana nikasema kwamba wakati ule walipokuwa wanadai bilioni tano kulikuwa kuna makubaliano kwamba tukiwapa bilioni moja na nusu basi tumemalizana.

Lakini mimi ningemwambia wewe *ZSTC* ni shirika la serikali sasa nipe gawio la serikali na mwenye mali ni serikali gawio langu maana yake ni *hundred percent* sasa umelisaidiaje hilo shirika hujalisaidia. Kwa hivyo nasema kwamba mimi ndio mwenye mali, mimi ndio serikali *ZSTC* nikimwambia nipe gawio langu maana yake ni asilimia mia. Mimi ndio mwenye mali hujalisaidia shirika. Tulipomwambia shirika kwamba gawio lote bakia nalo uendelee kuliendesha shirika ndio maana nikamwambia Mhe. Hamza Hassan Juma asikamate bajeti. Ukikamata bajeti ya Wizara ya Fedha *ZSTC* atakufa kwa sababu nitakuwa sina pahala pa kuisaidia *ZSTC* bajeti umeshaikamata mimi nimsaidie wapi.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema ni kwamba mashirika haya tunayafanyia kazi kesho tunajadili mashirika mawili mengine, Shirika la Umeme tunalijadili kesho na Shirika jengine moja tunalijadili kesho, kwa hivyo tukishakumalizana kuyajadili hayo nani atakwenda katika zile *reform*. Kuna baadhi ya waheshimiwa wawakilishi walikuwa wanasema kwamba wanasikia tu hii *reform* lakini hawazioni, nataka niwaambie sasa wataziona *reform.* Lengo la wizara yangu Mhe. Spika, kwanza shirika lifanye kazi kama shirika. Lakini la pili, shirika lilipe ndani ya serikali kwa mujibu wa marekebisho ya sheria ya mwaka 2005.Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Hamiza Hassan kwamba tufanye kazi kwa pamoja shirika la *ZSTC* bado ni letu sote na tunataka kulipa majukumu.

Mhe. Spika, niliulizwa suala hapa la watu walioanguka mikarafuu hiyo sio kazi ya Wizara ya fedha lakini nataka niseme *ZSTC* tulilibebesha majukumu ambayo siyo ya kwake. *ZSTC* unamwambia akajenge barabara atakupa tu pesa zake yeye badala ya kufanya kazi yeye anatakiwa auze karafuu halafu ainyanyue mikarafuu kwa kutafuta mbegu mpya na kuwasaidia wakulima wa mikarafuu. Kama ukimwambia *ZSTC* akajenge barabara, akanunue karabai, akanunue mabusati ya kulalia hapo shirika unaliua bure. Sasa *restructure* hiyo ndio tunalipeleka shirika hili liweze kufanya kazi sasa hivi kwa uhakika. Nataka niseme kwamba mashirika yatakayokuwa hayawezi kufanya kazi nadhani serikali itaachana nayo ili tupunguze ruzuku.

Hivi sasa ninavyokwambia Mhe. Spika, serikali inatoa zaidi ya bilioni saba kila mwaka kama ni ruzuku kwa tasisi kama hizi ambazo hazijiendeshi. Sasa mimi

nataka tujiendeshe ili na mimi nipate na aliyekuwa hajiendeshi mimi nadhani tutawafungulia mlango tuachane nao.

Mhe. Spika, nikimalizia nataka nikubaliane na wewe kwamba mdhibiti na Mkaguzi Mkuu amefanya kazi nzuri sana, ninalosisistiza twende na *value for money*, ukaguzi wa *value for money* Mhe. Spika, ndio utakaotusaidia nimesoma ripoti ya mwenyekiti wa *PAC* anasema mtu amekwenda kuuza kitu shilingi elfu mbili kapewa risiti atie saini kwenye vocha elfu ishirini ndipo mtu anaposhtuka. Kitu cha elfu mbili naambiwaje nitie saini kwenye vocha ya elfu ishirini, tukenda kwenye *value for money* hilo jambo halipo. Huwezi kumwambia mtu mshumaa huu bei yake laki moja akishakuona *volue for money* haliwezekani.

Kwa hivyo nataka niwambie Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, tujitahidi sana sasa hivi *value for money* ni njia pekee itakayoweza kutusaidia. Ofisi yangu Mhe. Spika, itajitahidi sana kufanya kazi karibu zaidi na Wizara ya Utawala Bora ili tuweze kufanikisha shughuli zetu hizi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kupata wasaa wa kuchangia ripoti hii ya Kamati ya PAC.

Mheshimiwa kubwa kwa upande wangu ni hizi *reforms* tu. Lakini namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha amechangia vizuri. Mimi nataka kusema kwa kweli hizo *reforms* zimeanza na tunaendelea nazo na nyengine tayari matunda yake yameonekana. Kubwa upande watu ni hili suala la Serikali za Mitaa. Kwa kweli tunaendelea nazo na niseme *technical paper* iko tayari inafata ngazi zake. Tukijaaliwa mwaka huu hautakwisha hizi reforms za Serikali za Mitaa tutafika mahala.

Mheshimiwa na mimi nakubaliana na mwenzangu na kamati kwamba tutafanya kazi pamoja. Wao wanatuangalia tunafanya kazi vipi na hasa kwenye matumizi ya fedha. Tutashirikiana kuona kasoro za hapa na pale zinarekebishwa ili tuendelee mbele.

Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, na mimi nishukuru na nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kwa ripoti yake aliyoiwasilisha kwa ufasaha. Naomba nitoe ufafanuzi wa mambo machache sana na niaze na lile la kumtunza *CAG*.

Mhe. Spika, kwa kweli *CAG* anatunzwa. Hivi sasa alivyo akistaafu anatunzwa na serikali kama viongozi wengine kwa mujibu wa Katiba mpaka Mwenyezi Mungu atakapo muhitaji.

Kwa hivyo serikali inamtunza *CAG* baada ya kumaliza muda wake na serikali itaendelea kumtunza. Inafanya hivyo kwa kujua umuhimu wa kazi za *CAG*. Hata katika kumuondoa katika nafasi yake basi ni lazima kuwe na mambo ya msingi ya kuweza kumuondoa. Au awe hawezi kutokana na sababu za maradhi. Mwenyezi Mungu amnusuru kwa hilo. Ama pengine awe na mambo na aundiwe Kamati na hiyo kamati ndio iweze kusema kwamba ana matatizo, ndipo aweze kuondolewa kwenye nafasi ile.

Pili suala la ripoti ya *CAG* au ripoti ya *PAC* kufanyiwa kazi na serikali. nataka niwahakikishie kama juzi nilivyojibu suala langu. Ripoti hizi sasa zitakuwa zinafanyiwa kazi na serikali. Nadhani si muda mrefu serikali itaikalia hii ripoti ya CAG na kila Wizara itaambiwa kwenye wizara yako kuna jambo hili na hili, tunaomba hili jambo ukalifanyie kazi ili hili jambo lisijirejee tena mara nyengine.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo limeguswa na Waheshimiwa Wajumbe ni suala la marekebisho ya Sheria Nam. 11 ya Mwaka 2005. Hivi sasa wizara yangu kupitia Ofisi ya *CAG* inafanya mapitio ya hii sheria. Pengine baada ya vikao vya Bajeti kumalizika usoni, tunatarajia kuleta mswada wa sheria ili kuifanyia marekebisho Sheria hii ya *CAG*.

Uimarishaji wa Ofisi pamoja na kuwajengea uwezo watendaji. Tunajitahidi, hivi sasa kwa kiasi fulani wapo wataalamu kiasi sio wa kutosha. Hali ilivyo sasa sivyo ilivyokuwa zamani.

Mwisho juu ya suala ambalo ndugu yangu amelisema anayemlipa *Kabili* ndiyo anayechagua wimbo. Maana yake anayemlipa mpiga zumari ndiye anayechagua wimbo, ndio maana yake. Katika hili nataka niseme kwamba CAG kwa mujibu wa sheria na taratibu ziliopo hakuna mtu yeyote ambaye anaweza akamuingilia juu ya utendaji wa shughuli zake za kazi.

Nataka niwathibitishie kwamba kazi aliyoifanya ya kuandika ripoti yake ndivyo hivyo hivyo ambavyo mimi nimeiwasilisha kwenye Baraza la Wawakilishi baada ya kuagizwa na Mhe. Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba niunge mkono hoja hii ya Kamati ya PAC.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, mimi naunga mkono tu ripoti. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nakushukuru mimi nina mambo mawili tu.

Kwanza ni ningeliomba Kamati kwa yale mambo ambayo wanahisi yakwenda kinyume na sheria. Wanapoandika ripoti yao basi na sisi watupelekee ili kwa upande wetu tushirikiane na Idara yetu ya DPP kuwapeleka mahakamani watu wanaofanya shughuli kama hizo.

Kwa mfano kulikuwa kuna shutma ya gari kwa mfano iliyouzwa na SMZ. Akanunua mfanyakazi, halafu mfanyakazi huyo huyo kauza tena kwa SMZ. Kwa kweli huu ni ubadhilifu. Lakini ni lazima tuweze kupata ushahidi ili tuweze kuwapeleka mahakamani.

Pili Mhe. Spika, naomba nitoe ufafanuzi zaidi katika suala la *CAG*. Kwa kweli tukisoma Katiba Kifungu cha 111, hichi kinaelezea hasa namna gani *CAG* anatunzwa na serikali. Katiba hiyo hiyo kifungu cha 112 kianzungumzia habari ya *appointment* yake. Kifungu cha 113 kinazungumzia kwamba hatoweza kuondolewa kazini isipokuwa kwa utaratibu maalum ambao utaratibu huo ni sawa sawa na jaji wa Mahakama Kuu. Mwisho kifungu cha 115(5) kinasema *CAG* baada ya kumaliza kazi zake au kustaafu basi hatoajiriwa pahala pengine popote isipokuwa atatunzwa tu na serikali.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ni kweli kabisa katika Wizara 16 ambazo Kamati hii ya PAC wametembelea moja ilikuwa ni wizara yangu na mimi hapa nimeguswa.

Kwanza niipongeze Kamati hii kwa kazi nzuri ambayo wamefanya. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako niende haraka haraka yale mambo ambayo mimi nimeona kwamba wizara yangu inahusika.

Nianze na Mhe. Hamza aliyezungumzia suala la deni ya *ATC*. Ni kweli *ATC* tunadai zaidi ya shilingi milioni 200 na ni deni la zamani tangu mwaka 2008. Lakini juzi hivi ambapo katika ziara hizi za ushirikiano baina ya serikali mbili SMZ na SMT wenzetu wamekubali kwamba watalishughulikia. Kwa taarifa yako ni kwamba tayari Katibu Mkuu ameshawaandikia rasmi barua ya kulikumbusha deni hilo kwa ajili ya malipo.

Jengine kuhusu fidia. Mhe. Hamza vile vile alipokuwa anazungumzia (*value for money)* alizungumzia juu ya ulipaji wa fidia. Nataka nimwambie Mhe. Hamza bahati nzuri na yeye alikuwepo mstari huu wa mbele. Kila bajeti serikali na Wizara yangu inafanya makisio kuhakikisha kwamba fedha zinazotakiwa zinalipwa. Lakini yeye anajua zaidi alikaa muda mrefu hapa. Ni bajeti gani ya maendeleo ambayo ilikamilishwa kwa asilimia 100. Si rahisi, ndio maana serikali inalipa fidia kwa mujibu wa uwezo wake.Serikali inajikuna ijipatapo. Vyenginevyo kama kweli kila kibu tulipe Wizara ya Miundombinu nakuhakikishia hata mishahara watu wasingelipwa. Maana tunazaidi ya shilingi bilioni 24 tunataka tuwalipe fidia wananchi.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba kamati hii katika ukurasa wa 155, wamesikitika kutohudhuria kwangu katika kamati. Mimi nimekuwa katika Kamati kama Makamo Mwenyekiti kwa muda wa miaka miwili na nusu. Tunapomwita waziri asipokuja mimi nilikuwa nachukia sana, nilikuwa sifurahi hata kidogo.

Mhe. Spika, kamati hizi zimeundwa Kikatiba, Kisheria na kuna Kanuni. Nataka niwambie wenzangu tu kwamba kama Waziri hakuja mnapomwita si kwa sababu ya dharau. Kuna vitu ambavyo ni muhimu sana. Sio kama Kamati si muhimu lakini jaalia kuna ujumbe wa *World Bank* unaokukusudia kukupa dola milioni 48 na mlishaahidiana tangu zamani kwamba tarehe fulani, saa fulani mje. Ni wakati huo huo ambapo kamati inakwita. Basi hata Naibu Waziri anaweza akaenda. Mimi nafikiri ni muhimu zaidi si suala la Waziri au Naibu Waziri ni suala la kuwasilisha hoja kama Naibu Waziri yupo, kama waziri yupo. Nasema huu ni mfano. Na kweli siku hii ambayo walinitaka nilikuwa nina dharura hiyo. Nina hakika kwamba nisengekwenda hizo dola milioni 48 tungezisikia tu. Wasione kama nilidharau, ni kwa sababu ya dharura ambazo zina uzito wake katika serikali na katika nchi.

Mhe. Spika, kamati hii vile vile nashukuru kwamba wamelipongeza Shirika la Bandari kwa mafanikio yake makubwa. Naamini kwa sifa hizi hawatakuwa wagema. Wataendelea na mwakani Ishallah mtakapokwenda mtapata sifa nyingi zaidi.

Vile vile waligusia suala la kuorodhesha mali za wizara yetu. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendelea ameeleza kwamba muongozo umeshatolewa na kila wizara itaorodhesha mali zake ziko wapi na zipo vipi. Taarifa hizo zitapelekwa kwa mwenye mali mkuu ambaye ni yeye. Kwa hivyo hili tayari linashughulikiwa.

Jengine kutafuta hati miliki. Hili nimeshalieleza asubuhi kwamba kuna muongozo wa serikali. Wizara zote zinahimizwa kwamba zitafute hati miliki ya

maeneo yao yote ambayo kuna mali zetu au miradi yetu. Hili naamini kwamba kila wizara inajitahidi sasa hivi katika kulishughulikia hilo.

Jengine Mhe. Spika, Shirika la Meli na Uwakala linaonekana linayumba, hii ni kwa mujibu wa PAC. Mimi nasema Shirika la Meli kama lilivyo sasa, basi nalo lingepongezwa kama Shirika la Bandari. Kwa sababu Shirika la Meli lina meli moja tena hiyo meli yenyewe mguu mmoja mzima, mguu mmoja mbovu. Meli ya pili ya mafuta, meli hii inakodishwa kwa *GAPCO*.

Jengine ni Uwakala wa meli, pamoja na kwamba tuna meli mbili ambayo ni Maendeleo, MV. Ukombozi na huu Uwakala. Lakini shirika hili linajitegemea kwa *operation* zake zote kuanzia mishahara hata matengenezo ya meli zake. Kwa hivyo hili nalo lingesifiwa, lakini kwa mujibu wa PAC wameona hivyo, siwalaumu. Lakini mara nyengine waende ndani zaidi waone na walinganishe lilivyokuwa Shirika la lilivyo sasa hivi. Katika hali hii ambayo wana meli mbili na moja ni kongwe sana MV. Maendeleo, meli ya pili ya Ukombozi ambayo inakodishwa kwa ajili ya kuja kuchukua mafuta. Na sehemu kubwa ni Uwakala wa meli za nje.

Mhe. Spika, sitaki nichukue muda mrefu lakini haya nimeona kama Wizara yangu imehusika nayo. Nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ahsante sana mimi naishukuru sana Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika Wizara yangu, hasa walipochukua jitihada wakafika mpaka kule Kengeja na wakaona mambo ambayo wamekuja kuyaeleza kwenye ripoti yao. Itanisaidia sana katika kufuatilia. Sauti yao wao waliyoitoa kwenye Kamati bila shaka itamfanya Waziri wa Fedha aongeze chochote ili ile skuli ya Kengeja iweze kupata bording iliyo nzuri ili waweze kuka watu kwa vizuri sana.

Halafu pia nawapongeza sana kwa kutilia mkazo suala la mafunzo ya sayansi na teknolojia na kunihimiza nitafute walimu wa sayansi. Nitajitahidi na nitashirikiana nao katika hilo.

Naunga mkono Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, na mimi naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa kwazi nzuri waliyoifanya. Kwa mara ya kwanza Wizarani kwangu hakuna matatizo ya msingi waliyoyaona kuhusu shughuli zetu hizi za kihesabu. Isipokuwa kulikuwa na tatizo moja dogo tu ambalo tutalimaliza mwezi huu.

Kuna wakati fulani fedha za wafanyakazi zilichukuliwa ulipopotea mshahara wakati ule wa wafanyakazi hewa. Kukawa na wafanyakazi kama sita (6) waliokatwa mishahara walikuwa hawastahiki. Sasa wamelipwa wanne (4) wakabakia wawili (2). Naomba kulihakikishia Baraza lako kwamba mwisho wa mwezi huu na hao wawili watalipwa. Kwa hivyo suala hilo litakuwa limekwisha.

Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, na mimi naishukuru sana Kamati ya PAC na naitakia kile la kheri. Niseme kwamba maneno ameyamaliza huyu mama hapa. Kwamba katika watu waaminifu wanawake ni waaminifu.

Wizara yangu haina hoja mbaya ni nzuri na tutasimama kidete kuhakikisha kwamba mapato ya serikali yanakwenda vizuri. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi ila tu nitoe shukurani zangu kwanza kwa ripoti ya Kamati. Kama nilivyosema awali kwamba imenipa muelekeo, imeniongoza na naomba mashirikiano na yote ambayo wameyaona yote nayaunga mkono na nitayatekeleza kama walivyonielekeza.

Naomba tuwe na subira ili tuone nini kinachoendelea. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii ili niweze kumpongeza sana Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa kazi nzuri aliyokuwa akiifanya tokea zamani na sasa wanaendelea nayo, Ishallah Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu na hekma na uaminifu ili aendelee kutenda kazi vizuri.

Nililolisikia ni kwamba kutoka kwa Mhe. Hamza kwamba amesikia majenereta sita (6) mabovu katika majenereta yaliyokuja hivi karibuni. Nataka nimuhakikishie kwamba hilo sio kweli. Majenereta yangu yote ni mazima, nashindwa kuyaendesha sasa kwa sababu sina hela ya mafuta basi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko: Ahsante sana Mhe. Spika, kupata nafasi hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa leo tunahitimisha habari zetu kwa kuzungumza habari ya PAC. Mimi nilibahatika katika miezi tisa ya nyuma kuwa ni mwanakamati wa PAC, kwa hivyo naona kila tukenda mbele matatizo yanazidi kupungua kwa kiwango kikubwa sana.

Kwa upande wa Wizara yatu ya Biashara suala la *ZSTC* naona mwenzangu Waziri wa Fedha amelizungumzia kwa uzuri kabisa na kwa upeo mkubwa. Ninachotaka kuwahakikishia kwamba wizara yetu kama ni mdao mkubwa wa suala hili, tumejitayarisha na tumeshaanza mchakato wa kufanya *reform* kubwa kabisa ya *ZCC* na kulifanya shirika lenye uwezo litakalo weza kudhibiti masuala ya upandaji mikarafuu, ukuzaji mikarafuu na ununuzi na uzaji wa karafuu.

Kuanzia sasa hivi zao la karafuu litakuwa sio kama mwana wa kambo au mwana aliyekuwa hana baba. Litakuwa linadhibitiwa vizuri tangu wakati wa upandaji mpaka uvunaji, mpaka uuzaji. Kutatokea *reform* kubwa katika Shirika hili na tunaomba mashirikiano ya sote ili kuona shirika hili tangu lilipoanzishwa mpaka leo ni Shirika la kihistoria na linamtazamo mkubwa na muhimu kabisa katika serikali yetu. *Reform* itafanyika na sio muda mrefu kuanzia sasa hivi.

Suala jengine ilikuwa ni suala la gari ambazo documents hizi tayari wameshakabidhiwa PAC. Naamini kwamba watazichunguza wataziangalia na pale watakapoona kuna dosari au kuna masuala zaidi basi wizara yetu ipo tayari kushirikiana nao na kuweza kuzitolea maelezo zaidi kama yatahitajika.

Maelezo yote na michango pamoja na ushauri ambao umetolewa na Kamati ya PAC tunaithamini sana na tutaifanyia kazi bila ya kigugumizi. Tunaamini kwamba tutawaridhisha kwa kiwango kikubwa sana.

Zaidi nawashukuru sana Mwenyekiti pamoja na Kamati yake kwa kwazi nzuri waliyoifanya na kwa kweli wanastahiki sifa. Sisi Wizara ya Biashara tunawakaribisha wakati wowote karibuni tena karibuni sana mjisikie mkono nyumbani. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuhusiana na ripoti hii ya Kamati ya PAC. Mimi kwanza naomba niwapongeze sana Mwenyeki, Makamo na kikosi chake cha kazi kwa namna ambavyo wanaendelea na kazi ambayo tulikuwa tunaifanya kazi pamoja. Tunawapongeza sana na nawaomba waendelee.

Katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi ripoti ya PAC pamoja na michango inayotokana na ripoti yake tumeichukulia kama ni miongozo na maelekezo ya kazi kwa wizara yetu. Naahidi kwamba yote ambayo wameelekeza kwa jumla tutayafanyia kazi na tutakuwa pamoja katika kuona *accountability* ya mali ya umma iko katika hali nzuri katika nchi yetu. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, mimi niwashukuru Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wake wote. Kwa vile hawakuwa na mashaka na Wizara hii. Hawakupata bahati ya kuja kutukagua, lakini Inshaallah nimewasikia wenzangu kuanzia Julai basi tutajiweka vizuri zaidi. Ahsante sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC)): Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuja kusimama mbele ya Baraza lako kwa nia ya kufanya majumuisho kati ya yale ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe na Waheshimiwa Mawaziri kwa vile walivyopata fursa ya kuchangia na hata wale ambao hawakupata fursa lakini makofi yao yalionyesha kuwa ni ishara ya kukubaliana na hili.

Mhe. Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe waliochangia ripoti yetu ya Kamati nao ni kama hawa wafuatao:-

1) Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
2) Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4) Mhe. Fatma Mbarouk Said
5) Mhe. Hija Hassan Hija
6) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
7) Mhe. Hamza Hassan Juma
8) Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (kwa maandishi)

Kwa upande wa Mawaziri waliopata fursa ya kujibu na kufafanua baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe nao ni:-

9) Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.
10) Mhe. Haji Mwinyi Makame
11) Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
12) Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais
13) Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.
14) Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.
15) Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
16) Mhe. Waziri wa Afya.

17) Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawakae na Watoto.
18) Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.
19) Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.
20) Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.
21) Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi
22) Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Michango yote ya Waheshimiwa Wajumbe imelenga katika kuipa nguvu, uwezo pamoja na kuiombea muda Kamati yetu ya PAC ili iweze kuzifanyia kazi ripoti za CAG ili hatimaye uchumi wa nchi yetu upate kukua na uwe na faida kwa wananchi wetu.

Vile vile Mhe. Spika, michango ya Waheshimiwa Mawaziri pamoja na kulenga kujibu hoja na kufafanua baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe, Michango ya Waheshimiwa Mawaziri imelenga kuelezea utayarifu wao wa kushirikiana na Kamati ya PAC katika kuhakikisha matumizi mazuri ya fedha na hivyo kukomesha ufisadi katika nchi yetu.

Waheshimiwa naomba nichukue fursa hii nimshukuru sana Mhe. Abubakar Khamis Bakar (Waziri wa Katiba na Sheria) kwa kauli yake aliyoitoa kwa kutaka kushirikiana na Kamati ya PAC ili kuwaburuza Mahakamani mafisafi wa fedha. Naomba niseme kwamba tukijaaliwa katika ripoti inayofuata ya mwaka2008/2009 kazi ya kuwapeleka Mahakamani mafisadi itaanza rasmi.*(Makofi).*

Mhe. Spika, kwa ujumla kamati yetu imepata nguvu mpya ya kufanya kazi. Ripoti hii ya mwaka 2008/2009 na ripoti nyengine ambayo tuna taarifa itafika katika Baraza lako tukufu wakati wa kikao cha bajeti, ripoti ya mwaka 2009/2010 ripoti ambayo itakuwa na ukaguzi unaoonyesha *value for money. (Makofi)*

Mhe. Spika, mwisho kabisa kabla sijamaliza naomba maombi mawili. Moja tulitegemea makatibu wakuu watakuwepo hapa kama vile ambavyo wanakuwepo wakati wakiomba fedha na leo watakuwepo wakati ambao tunachambua matumizi yao. Hivyo basi nawaomba mawaziri wazichukue ripoti hizi na wazipeleke kwa watendaji, kwa sababu kamati mara nyingi inapofanya kazi tunapofika kule, huambiwa sisi hoja za mdhibiti hatujazipata, kitu ambacho huleta usumbufu mkubwa kwa kamati yetu.

Lakini ombi la pili naomba kama vile anavyofanya Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete wakati anapopokea ripoti hutoa neno

na lile neno likaonyesha uzito wa kamati za mdhibiti, namuomba Mhe. Rais wa Zanzibar na hapa mara tu wanapokabidhiwa ripoti basi naye atoe neno ambalo litaonyesha uzito wa ripoti za mdhibiti. Naamini kwamba kauli ya Rais katika nchi inakuwa nzito zaidi kulikoni kauli ya Mhe. Haji Omar Kheri, namuomba Mhe. Rais afanye hivyo.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba sisi kamati ya PAC tuna kauli mbiu yetu ambayo inasema kwamba Zanzibar bila ya ufisadi inawezekana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji basi wale wanaoikubali na kuipokea ripoti hii ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika, kabla hatujamuita Mhe. Makamao wa Pili wa Rais kwa sababu ya muda uliobakia ni robo, sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuweka utaratibu.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliobakia hautoshi kuwezesha Makamo wa Pili wa Rais kuweza kutoa hotuba yake, hivyo naliomba Baraza lako tukufu liridhie kuongeza muda ili kumaliza shughuli iliyo mbele yetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji basi wale wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi).*

Niwashukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisaidia kuendesha kikao hiki, kwa kazi kubwa mliyoifanya leo kuanzia asubuhi hadi wakati huu, kiasi cha kuweza kumaliza shughuli zetu vizuri na kwa ufanisi mkubwa. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aje atufungie.

Hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi Katika Ufungaji wa Mkutano wa Tatu wa Baraza la Wawakilishi

Mhe. Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi wa rehma kwa kutujaalia amani na mshikamano katika nchi yetu ya Zanzibar na katika serikali yetu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa. nazidi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutekeleza kwa ufanisi shughuli za mkutano huu wa tatu wa Baraza la Nane la wawakilishi la Zanzibar. Pia, napenda kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuendesha mkutano huu kwa busara, umakini na mafanikio makubwa. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza kwa kuendesha vikao mbali mbali katika mkutano huu wa tatu kwa umakini na ufanisi mkubwa. Kwa kweli baraza hili halikufanya makosa kwa kuwachagua viongozi wetu hawa.

Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda pia kuchukua fursa hii adhimu kuwapongeza kwa dhati kabisa jaji kiongozi wa mahakama kuu ya Zanzibar Mhe. Omar Othman Makungu, na Mwanasheria Mkuu mpya wa serikali Mhe. Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kwao na Mhe. Doctor. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kushika nyadhifa hizo hivi karibuni.

Mhe. Spika, kama tunavyojua Mwanasheria Mkuu wa serikali kwa nafasi yake hiyo huwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na tayari umeshamuapisha rasmi kuwa mjumbe wa baraza hili tukufu. Kuteuliwa kwake huko kunaonesha imani kubwa ambayo Mhe. Rais alinayo juu yake. Ninamtakia kila la kheri na mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yake hayo mapya.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru waheshimiwa wawakilishi wenzangu kwa kuuliza maswali mazuri, kuhusu utendaji wa shughuli za serikali na kutoa maoni yao wakati wa kujadili miswada na hoja mbali mbali zilizowasilishwa hapa barazani. Pia, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri kwa kuyajibu vizuri na kwa ufasaha maswali yaliyoulizwa pamoja na kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali. Ni matumaini yangu kwamba wananchi wamefaidika na mijadala yetu katika baraza hili na majibu yote yaliyotolewa.

Mhe. Spika, katika mkutano huu jumla ya maswali ya msingi 77 kati ya 147 yaliyopangwa yaliulizwa na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri pamoja na maswali mengi ya nyongeza. Baraza pia lilipitisha miswada minne ya sheria ifuatayo:-

(i) Mswada wa sheria ya kufuta sheria ya mfuko wa elimu ya juu nam. 6 ya 2001 na kuweka sheria mpya ya bodi ya mikopo ya elimu ya juu na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

(ii) Mswada wa sheria ya mikataba ya amana na mali zinazohamishika na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

(iii) Mswada wa sheria ya kufuta sheria ya mpango wa taifa wa kujitosheleza kwa chakula *(mtakula)* nam. 3 ya 1988 na kutunga sheria ya uhakika wa chakula na lishe Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

(iv) Mswada wa sheria ya mtoto itakayotoa haki na maslahi bora ya mtoto, itakayorekebisha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai na kusahihisha sheria zinazohusiana na mambo hayo.

Mhe. Spika, baraza lilipokea na kujadili ripoti ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu Zanzibar kwa kipindi cha 2008/2009. Vile vile, baraza lilipokea na kujadili ripoti za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi. Aidha, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu walipata fursa ya kuhudhuria katika warsha, semina na matukio mengine kama ifuatavyo:-

(a) Walihudhuria warsha kuhusu mswada wa sheria ya uhakika wa chakula na lishe Zanzibar iliyofanyika tarehe 22 machi 2011 kwenye ukumbi wa *Zanzibar ocean view.*

(b) Walihudhuria semina kuhusu mswada wa sheria ya watoto ya 2011 iliyofanyika tarehe 26 machi 2011 kwenye afisi ya Baraza la Wawakilishi.

(c) Waheshimiwa Wajumbe pia walihudhuria mkutano wa Asasi za kiraia uliofanyika tarehe 27 machi 2011 kwenye afisi ya Baraza la Wawakilishi.

(d) Halikadhalika, walihudhuria maonyesho ya asasi za kiraia yaliyofanyika tarehe 28 na 29 machi 2011 kwenye viwanja vya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mswada wa kwanza uliojadiliwa katika Baraza lako tukufu unakusudia kufuta sheria ya mfuko wa elimu ya juu nam. 6 ya mwaka 2001 na

kuweka sheria mpya itakayojulikana kama sheria ya kuanzisha bodi ya mikopo ya elimu ya juu, Zanzibar. Pamoja na mambo mengine, sheria mpya ya bodi ya mikopo inafafanua muundo wa bodi hiyo, kazi zake na uteuzi wa mkurugenzi na majukumu yake. Aidha, sheria hii inazungumzia kuanzishwa kwa mfuko wa elimu ya juu pamoja na malengo ya mfuko. Mswada pia unaweka wazi utaratibu na masharti ya kupata mkopo, urudishwaji pamoja na majukumu ya mwajiri na mdhamini wa mkopaji.

Mhe. Spika, chini ya sheria hii mpya ya bodi ya mikopo ya elimu ya juu, mwanafunzi anaweza kufikiriwa kupewa mikopo endapo:-

(a) Atakuwa ni Mzanzibari;
(b) Ameruhusiwa kujiunga na chuo cha elimu ya juu;
(c) Amewasilisha maombi kwa maandishi kwenye fomu iliyowekwa;
(d) Mtu ambaye hana msaada wa fedha kutoka kwenye chanzo au vyanzo vyovyote;
(e) Mwanafunzi anayeendelea na masomo na amefaulu mitihani ambayo itamuwezesha kuendelea na hatua nyengine ya masomo.

Serikali imeanzisha sheria hii ya bodi ya mikopo ya elimu ya juu ili kutoa fursa kwa vijana wetu ya kupata mikopo na kuendelea na elimu ya juu katika vyuo mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi. tunatoa wito kwa bodi itakayoanzishwa ya kusimamia mfuko huu, itekeleze majukumu yake kwa uadilifu mkubwa ili kuepuka mivutano na tuhuma kutoka kwa waombaji wa mikopo hii. elimu ndio msingi wa maendeleo, napenda kutoa wito kwamba fursa iliyotolewa itumike vizuri ili kufikia azma iliyokusudiwa ya kuboresha na kuendeleza sekta ya elimu hapa Zanzibar

Mhe. Spika, mswada wa pili uliowasilishwa na kujadiliwa katika baraza lako tukufu kuhusu sheria ya mikataba ya amana na mali zinazohamishika na mambo mengine yanayohusiana na hayo ulikuwa na lengo la kufungua wigo mpya kwa wananchi hasa wale wasiokuwa na uwezo wa kumiliki mali zenye thamani kubwa, kuweza kupata mikopo kupitia mali wanazomiliki ambazo ni mali zinazohamishika.

Kwa mujibu wa sheria hii, serikali itaanzisha daftari la usajili wa haki za amana kwa mali zinazohamishika litakaloandaliwa na kutunzwa na Mrajis wa Masjala ya Haki za Amana. ni imani ya serikali kwamba utaratibu huu utawawezesha wananchi kiuchumi kwa kuweza kupata mikopo katika vyombo vya fedha bila ya masharti magumu kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza biashara zao, hasa katika sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara ndogo ndogo.

Mhe. Spika, mswada wa tatu uliowasilishwa na kujadiliwa katika Baraza hili tukufu ulikuwa mswada wa sheria ya kufuta sheria ya mpango wa taifa wa kujitosheleza kwa chakula *(mtakula)* nam. 3 ya 1988 na kutunga sheria ya uhakika wa chakula na lishe Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mswada huu umelenga kutoa misingi ya kisheria ya utekelezaji wa sera ya uhakika wa chakula na lishe, kukuza hadhi ya uhakika wa chakula na lishe kwa taifa na watu binafsi. Aidha, umeweka masharti ya kuanzisha na kuweka muundo na kazi za baraza la taifa la uhakika wa chakula na lishe, na kuweka masharti ya kuanzisha na kuweka muundo na kazi za kamati tendaji za sekta husika.

XXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXX

Sheria hii inaweka wajibu kwa serikali kuhusiana na haki ya chakula na utaratibu wa kulalamikia haki ya chakula pale inapovunjwa. Hivyo, sheria hii inataka kuanzishwa hifadhi ya chakula ya Zanzibar kwa madhumuni ya kuhakikisha usambazaji wenye uhakika wa chakula na kukabiliana na hali nyengine yoyote ya dharura inayosababishwa na ukame au mafuriko, au majanga mengine yoyote ya kimaumbile kama inavyoweza kuamuliwa na baraza. vile vile, sheria imetaja vyanzo vya fedha za kuendeshea hifadhi ya chakula ya Zanzibar ikiwa ni pamoja na fedha kutoka kasma ya serikali, fedha kutokana na mauzo ya akiba ya chakula, na fedha kwa njia ya misaada, mikopo au ruzuku.

Mhe. Spika, ni imani yangu kuwa kuanzishwa kwa sheria hii kutatoa msukumo mkubwa kwa wananchi kuzalisha chakula hapa nchini badala ya kutegemea uagizaji mkubwa kutoka nje. Serikali kwa upande wake itajitahidi kuimarisha huduma za utafiti na ushauri kwa wakulima, pamoja na huduma za kilimo cha matrekta na matumizi ya pembejeo bora za kilimo *(mbegu bora, madawa).*

Mhe. Spika, ripoti ya mdhibiti na mkaguzi wa hesabu Zanzibar ya 2008/2009 imeonyesha kuwa kuna uendelevu wa ukiukwaji wa taratibu na udhibiti wa fedha na mali za serikali kwa baadhi ya taasisi. Natoa agizo kwa makatibu wakuu, wakurugenzi, na wale wote wanaosimamia fedha za serikali wawajibike ipasavyo kwa kusimamia kwa ukamilifu mapato na matumizi ya fedha za serikali.*(Makofi)*

Hii itakwenda sambamba na sheria namba 9 ya mwaka 2005 ya manunuzi na kuziondoa mali za umma pamoja na kanuni za fedha zilizopo. aidha, ni wajibu wa mamlaka zote husika na usimamizi wa mapato kupanua wigo utakaosaidia uendeshaji mzuri wa serikali na kutoa huduma za maendeleo ya jamii na uchumi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nimefarajika sana kuona kuwa wajumbe wa baraza lako tukufu wametumia fursa hii kujadili kwa kina ripoti na miswada iliyowasilishwa katika mkutano huu. Aidha, nimefarajika zaidi kwa kuona jinsi semina, warsha na maonyesho ya asasi za kiraia jinsi yalivyoandaliwa vizuri kwa ajili ya waheshimiwa wajumbe wa baraza lako tukufu. Ilikuwa ni elimu tosha na ni matumaini yangu kwamba wajumbe tumejifunza mengi na kuelimika vya kutosha juu ya masuala yaliyokusudiwa. nasisitiza, warsha, semina na mafunzo mengine yatolewe zaidi kwa waheshimiwa wajumbe wa baraza hili kila inapobidi kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba nieleze machache kuhusu kadhia mbali mbali zinazolikabili taifa letu ambazo zikiachwa bila ya kuchukuliwa hatua madhubuti tunaweza kuhatarisha amani, umoja na mshikamano wa nchi yetu kutokana na wananchi kukata tamaa katika mustakabali wa maisha yao.

Mhe. Spika, serikali kupitia ofisi ya makamu wa pili wa rais, imekuwa ikiendelea kupokea malalamiko mengi ya migogoro ya ardhi katika kipindi hiki. Watu wetu wanavamia ardhi kwa ujenzi wa nyumba za makaazi, majengo ya kufanyia biashara au uwekezaji wa kilimo na masuala mengine ya kiuchumi. Suala la kuvamia ardhi halikubaliki kwa mujibu wa sheria na taratibu tulizojiwekea. Napenda kulieleza baraza lako tukufu kuwa serikali inaandaa utaratibu mzuri wa kulishughulikia suala hili, hata hivyo nawaagiza viongozi wa serikali za wilaya na mikoa kushughulikia migogoro midogo midogo ya ardhi katika maeneo yao. ni vyema ili serikali za mikoa na wilaya ziweze kutatua matatizo ya ardhi, wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya waepuke wao wenyewe kuingia katika migogoro hiyo, vyenginevyo watashindwa kutatua migogoro hiyo na hivyo kushindwa kuwatumikia wananchi na itaonyesha kuwa wameshindwa kazi na dhamana walizopewa.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuifahamisha jamii na hasa wale wananchi wanaofika serikalini kudai kurejeshewa maeneo yao kwamba, ardhi yoyote iliyochukuliwa na serikali kwa utaratibu maalum kwa matumizi ama ya taasisi za serikali, miradi ya maendeleo au ya kijamii au shughuli za ulinzi wa nchi yetu, ardhi hizo zitaendelea kutumika kwa shughuli hizo na wananchi hawapaswi kudai kurejeshewa ardhi hizo.*(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nitumie muda wako kidogo kwa kuelezea tatizo la kupanda kwa bei ya vyakula hapa nchini. Pamoja na hali yetu ya uchumi kuanza kuimarika, serikali inasikitishwa sana na upandaji wa bei za bidhaa mbali mbali za vyakula na mafuta ya kupikia jambo ambalo linasababisha kupanda kwa mfumko wa bei nchini na hivyo kusababisha hali ngumu ya maisha kwa wananchi walio wengi, chanzo kikuu cha tatizo hili ni kutokana na kupanda kwa bei za vyakula katika masoko ya kimataifa kwa kiasi kikubwa

katika kipindi cha miezi sita iliyopita yaani oktoba, 2010 hadi machi, 2011 na hivyo kusababisha kupanda kwa kiwango kikubwa cha wastani wa bei za watumiaji katika soko la Zanzibar.

Mfano bei ya mchele katika soko la kimataifa mwezi oktoba, 2010 ilikuwa us$ 480 lakini mwezi machi, 2011 bei hiyo ilipanda hadi kufikia us$ 620. sukari mwezi oktoba, 2010 ilikuwa us$ 700, lakini mwezi machi, 2011 bei ilifikia us$ 880 na unga wa ngano mwezi oktoba, 2010 bei ilikuwa us$ 420 lakini mwezi machi, 2011 bei ilifikia us$ 550. upandaji huo ndio uliosababisha bei ya bidhaa hizo kupanda hapa kwetu.

Mhe. Spika, sababu zilizofanya bei za vyakula kupanda duniani na hapa kwetu ni nyingi, miongoni mwa sababu hizo ni:-

- Machafuko yanayoendelea kuzikumba nchi za huba na kupelekea kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia.

- Mafuriko na majanga makubwa kama ukame yaliyozikumba nchi za mashariki ya mbali urusi na marekani ambao ndio wazalishaji wakubwa wa vyakula hivyo hasa ngano.

- Uharamia uliopo katika ukanda wa mashariki ya bahari ya hindi ambao husababisha kupanda kwa gharama za usafirishaji. tabia ya wafanyabiashara na waagiziaji wa Zanzibar kuagiza kiwango kidogo cha bidhaa ambacho hakiendani na mahitaji ya soko la Zanzibar au kuzuia kuingiza bidhaa hizo katika soko.

Mhe. Spika, kufuatia hali ya upandaji huo wa chakula, serikali imechukua juhudi za kufanya mkutano na wafanyabiashara na waagiziaji wa chakula kwa nia ya kuwaomba kuziangalia bei za vyakula hivyo zisiwaathiri sana wananchi, wapange bei zao kwa mujibu wa uwezo wa wananchi wetu ambao wengi wao huwa na vipato vya chini. Kimsingi, hivi sasa serikali na wafanyabiashara hao wameshafikia makubaliano juu ya uletaji wa chakula na mwenendo wa bei zake hapa Zanzibar, utaratibu huo unatarajiwa kutangazwa kwa wananchi hivi karibuni ili waweze kujua bei halisi ya bidhaa hizo kulingana na mwenendo wa soko, kwa kupitia baraza lako tukufu, Mhe. Spika, napenda kuwashukuru sana wafanyabiashara wetu hao kwa usikivu wao waliouonyesha.

Mhe. Spika, pamoja na hatua hizo ambazo serikali imechukua ili kupunguza utegemezi wa chakula kutoka nje, serikali inakusudia kuendeleza sekta ya kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji maji ili kuweza kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula utakaosaidia kupunguza bei za vyakula. Aidha, serikali

inakusudia kuanzisha mifumo ya akiba ya chakula nchini kwa madhumuni ya kupunguza ongezeko la mara kwa mara la bei za vyakula na kuwasaidia wananchi kwa kuwapunguzia makali ya maisha.

Mhe. Spika, sambamba na juhudi za serikali za kuwawezesha wananchi kiuchumi, tunatoa wito kwa wananchi, hasa vijana kujishughulisha na shughuli za uzalishaji mali, ikiwemo kilimo, ufugaji na biashara badala ya kukaa tu na kujiingiza katika vitendo vibaya kama vile wizi na kutumia madawa ya kulevya. Vitendo hivi havikubaliki na vinaongeza kasi ya umasikini kwao na kwa familia zao.

Aidha, serikali inakusudia kuwawezesha vijana katika kuanzisha miradi mbali mbali midogo midogo kwa nia ya kuongeza fursa za ajira kwa vijana hao, badala ya kutegemea sana ajira kutoka serikalini. serikali imeanzisha wizara ya kazi, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na ushirika kwa dhamira hiyo ya kuwasaidia vijana na wananchi kuondokana na umasikini, aidha, natoa wito kwa vijana mmoja mmoja au kupitia vikundi vyao watumie fursa zinazotolewa na serikali ili kuwaletea mabadiliko katika maisha yao na kuendeleza uchumi wa nchi yetu. Vile vile, serikali itaendelea na juhudi zake za kuimarisha michezo ili kujenga afya za vijana wetu pamoja na kuimarisha uhusiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mhe. Spika, kupitia hotuba yangu ya kufunga baraza ya januari, 2011 nilitoa onyo na leo narudia tena kusisitiza kupitia baraza lako tukufu kuhusu suala la uharibifu wa mazingira kwa baadhi ya wananchi kuchimba mchanga kiholela na kukata misitu na miti ovyo. Suala hili linasababisha athari kubwa katika nchi yetu kama vile kuongezeka kwa joto, ardhi kuwa ya mashimo na isiyofaa kwa kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi, na upungufu wa mvua, hali hii pia inapelekea kupungua kwa uzalishaji wa mazao na kuongezeka kwa umasikini nchini, natoa wito kwa mara nyingine tena kwa viongozi na wananchi sote tuhifadhi na tuyalinde mazingira yetu, kila mtu ana wajibu wa kutekeleza suala hili. Kwa upande wake serikali itawachukulia hatua kali watu watakaoendelea kuharibu mazingira, nachukua fursa hii kuwapongeza sana wananchi walioanzisha vikundi vya kuhifadhi mazingira kwa juhudi zao kubwa wanazozichukua katika maeneo yao mbalimbali, huu ni mfano mwema unaofaa kuigwa na wananchi wote.

Mhe. Spika, visiwa vyetu hivi karibuni vilipata janga la upepo mkali ulioanza tarehe 9 februari, 2011 na kuendelea takriban kwa wiki nzima, upepo huo ulileta athari kwa wananchi kwa kubomokewa na nyumba zao na miti kuanguka, jumla ya nyumba 206 za makaazi ya wananchi ziliathiriwa na upepo huo. Pia mabanda 10 katika kambi ya jku bambi yaliezuliwa mapaa. haya ni maafa yasiyotarajiwa, na serikali inawapa pole wananchi

wote walioathirika kwa njia moja au nyingine kutokana na upepo huo, aidha, serikali imo katika mchakato wa kuimarisha idara ya kukabiliana na maafa chini ya ofisi ya makamu wa pili wa rais, ili iweze kuwa na uwezo wa vifaa vya kukabiliana na maafa ya aina yoyote ile yanayoweza kutokea.

Mhe. Spika, kuhusu muungano wetu, zipo changamoto zinazokabili muungano huo. lakini nina furaha kueleza kwamba vikao vya kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vinaendelea, ikiwemo vikao vya wataalamu, vikafuatiwa na vikao vya makatibu wakuu na waheshimiwa mawaziri.

Masuala ambayo yalioonekana kuwa ni kero na kujadiliwa katika vikao hivyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Ushiriki wa Zanzibar katika jumuiya ya afrika ya mashariki bado haujawekwa wazi.
(b) Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia bado halijaamuliwa.
(c) Uvuvi katika ukanda wa bahari kuu.
(d) Ushirikiano wa Zanzibar na taasisi za nje.
(e) Ajira kwa watumishi wa Zanzibar katika taasisi za muungano.
(f) Mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada kutoka nje; kama vile mgao unaohusiana na faida ya benki kuu; hisa za serikali ya mapinduzi ya Zanzibar zilizokuwa katika bodi ya sarafu ya afrika mashariki.
(g) Uwezo wa serikali ya mapinduzi ya Zanzibar kukopa ndani au nje ya nchi.
(h) Malalamiko ya wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili.
(i) Utekelezaji wa sheria ya haki za binadamu Zanzibar.
(j) Ongezeko la gharama za umeme kutoka tanesco.

Mhe. Spika, katika masuala hayo, ninafuraha kusema kwamba yapo maeneo yameshapata ufumbuzi kwa kuchukuliwa hatua nzuri za utekelezaji kupitia kamati ya pamoja ya kushughulikia masuala ya muungano kama ifuatavyo:-.

- Suala la utekelezaji wa sheria ya haki za binadamu Zanzibar limepatiwa ufumbuzi kwani sheria ya tume ya haki za binaadamu na utawala bora imefanyiwa marekebisho, sasa tume ya haki za binadamu inafanya kazi zake pande zote mbili za muungano.

- Suala la malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili pia limepatiwa ufumbuzi, bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha taratibu zote za kiforodha kupitia kituo chochote rasmi cha forodha zitahesabika kuwa zimeingizwa ndani ya jamhuri ya muungano wa tanzania, na hazipaswi kulipiwa kodi mara mbili. Katika kuhakikisha kuwa tatizo hilo halijitokezi tena, mamlaka ya mapato tanzania itachukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wanaotumia vibaya fursa ya ukadiriaji wa thamani za bidhaa.
- Suala la mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada kutoka nje ya nchi pia limeshughulikiwa. serikali ya mapinduzi ya Zanzibar inapata asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti, aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2009/2010, serikali ya mapinduzi ya Zanzibar imeanza kunufaika na asilimia 4.5 ya mikopo ya kibajeti kupitia *general budget support*.
- Suala la uwezo wa Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi limepatiwa ufumbuzi na sasa serikali ya mapinduzi ya Zanzibar inaweza kukopa ndani ya nchi. aidha, smz inaweza kukopa nje ya nchi chini ya udhamini wa serikali ya jamhuri ya muungano wa tanzania.

Mhe. Spika, kwa hoja zilizobaki, hatua mbali mbali za kutafutiwa ufumbuzi zinaendelea. ni matumaini yangu kuwa muungano wa tanganyika na Zanzibar utaendelea kuimarika siku hadi siku na changamoto zinazojitokeza zitapatiwa ufumbuzi kwa haraka.

Mhe. Spika, umekuwepo wasi wasi kuhusu utaratibu wa kuandaa katiba mpya ya jamhuri ya muungano wa tanzania, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia hotuba yake ya mwisho wa mwezi aliyoitoa tarehe 31 Disemba 2010 katika vyombo vya habari, alitoa ufafanuzi wa kutosha kuhusiana na suala la mabadiliko ya katiba na hatua zitakazochukuliwa hadi kupelekea kuandikwa kwa katiba mpya. Aidha, katika hatua za awali kabisa, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwasiliana na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya azma hiyo, hivi sasa, wanasheria wetu wakuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar wanawasiliana ili kuweka utaratibu mzuri utakaowezesha kutoa haki sawa kwa kila upande wa Jamhuri ya Muungano, kutoa maoni na mapendekezo katika utayarishaji wa katiba mpya, ikiwa pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa kuratibu maoni hayo. Hivyo, napenda kuwahakikishia wananchi kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) inashirikishwa kikamilifu katika

mchakato wa kuandika katiba mpya kwa hivyo wajitokeze kuchukua fursa za kutoa maoni yao wakati utakapofika.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuliarifu baraza lako tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeamua sherehe za miaka 47 ya muungano wetu kwa mwaka huu zifanyike hapa Zanzibar. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tayari ameridhia Zanzibar kuwa mwenyeji wa sherehe hizo, ambazo zitafikia kilele tarehe 26 aprili 2011 katika uwanja wa amaan. Kamati ya maandalizi ya maadhimisho ya taifa iliyo chini ya ofisi ya waziri mkuu kwa kushirikiana na kamati tendaji ya sherehe na maadhimisho ya Zanzibar, iliyo chini ya ofisi ya makamu wa pili wa rais zinaendelea kufanya maandalizi yanayohitajika ratiba na mialiko rasmi itatolewa baadae kutoka ofisi ya waziri mkuu.

Mhe. Spika, mwezi februari 2011 kulitokea milipuko ya mabomu katika kambi ya jeshi ya Gongo la Mboto huko Dar es Salaam. katika tukio hilo jumla ya wananchi na watanzania wenzetu wapatao 24 walipoteza maisha, na watu wengi kujeruhiwa, na wengi wamepoteza nyumba zao pamoja na mali nyengine. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunaendelea kutoa pole kwa waathirika wote wa mabomu, na kwa rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na tukio hilo ni tukio la kusikitisha, lakini ni mipango ya mwenyezi mungu ambayo haina makosa, tuendelee kuwasaidia wenzetu walioathirika kwa hali na mali. Aidha, ninamuomba mwenyezi mungu atuepushie na majanga kama hayo na mengine katika nchi yetu. amin.

Vile vile, nachukua fursa hii kwa niaba ya serikali ya mapinduzi ya Zanzibar kutoa pole kwa waziri mkuu wa serikali ya jamhuri ya muungano wa tanzania na waziri wa habari, utalii, utamaduni na michezo wa serikali ya mapinduzi ya Zanzibar, wanafamilia na wananchi wote wa tanzania kwa msiba mkubwa uliotupata usiku wa tarehe 22 machi 2011 kwa kuwapoteza wasanii wetu 13 katika ajali ya gari huko Mikumi, Mkoa wa Morogoro. Tunamuomba mwenyezi mungu awalaze mahala pema peponi wenzetu wote waliotangulia mbele ya haki na tunawaombea wapone haraka wote waliopata majereha kutokana na ajali hiyo.

Mhe. Spika, hali ya usalama barabarani hapa kwetu Zanzibar bado si ya kuridhisha, vipando vya moto vya magurudumu mawili kama vile, pikipiki na vespa pamoja na kuwasaidia sana wananchi wetu kwa ajili ya safari zao za kila siku lakini wapo baadhi ya wananchi huvitumia vyombo hivi bila ya kufuata sheria zilizowekwa ili kunusuru maisha yao pindipo inapotokea kupata ajali. Mfano, sheria inasema kwamba watumiaji wa pikipiki na vespa ni lazima wavae kofia zilizoruhusiwa *(helmet)* ili kunusuru kuumia vichwa iwapo itatokezea kupata ajali, baadhi ya wananchi wetu hawafanyi hivyo na hivyo

huvunja sheria, aidha, waendesha baiskeli nao huendesha baiskeli nyakati za usiku bila ya baiskeli zao kuwa na taa. haya pia ni makosa kisheria.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuvipongeza sana vyombo vya dola polisi kwa hatua walizochukua hivi karibuni kuwakamata watumiaji wa vyombo hivyo kwa kuvunja sheria hiyo, naliomba jeshi la polisi liendelee na hatua zake hizo. Hapo hapo ningelipenda kuwasihi wananchi wanaotumia vipando vya pikipiki, vespa na baiskeli watii sheria zilizowekwa zinazohusiana na matumizi ya vipando hivyo.

Mhe. Spika, kumezuka mtindo siku hizi wa kufanya mashindano ya magari wakati wa usiku hasa katika manispaa ya mji wa Zanzibar katika maeneo ya Mombasa, Michenzani, Darajani, Mji Mkongwe, maeneo ya Forodhani na Shangani, vitendo hivi vinaweza kupelekea kuhatarisha maisha ya watumiaji wa barabara wakati wa usiku. Napenda kuliomba tena jeshi la polisi na hasa usalama barabarani kuliangalia suala hili na kuchukua hatua za kukomesha vitendo hivi kwa faida ya usalama wa maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, katika kujadili ripoti ya kamati ya fedha, biashara na kilimo suala la tanzania kujiunga na *OIC* limejitokeza, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba tangu mwaka jana sekretariate ya *OIC* ilivunjwa na kuundwa kamati mpya ambayo itaangalia upya muundo wake, katika yake na masharti mapya ya kujiunga na jumuia hiyo. Kamati hiyo itatoa ripoti yake baada ya mwezi wa juni, 2012 hivyo, kutokana na zoezi hilo *OIC* ilisitisha kupokea wanachama wapya mpaka hapo zoezi hilo litakapokamilika baada ya zoezi hilo kukamilika hapo mwakani, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utalitafakari tena suala hilo kwa kuzingatia muundo mpya, katiba mpya na masharti mapya ya kujiunga na jumuia hiyo.

Mhe. Spika, pamoja na changamoto zilizopo katika kuiletea nchi yetu maendeleo, imani yenu na ushirikiano wenu mnaoendelea kutoa kwa serikali, unatupa moyo na matumaini kwamba kwa pamoja tutaweza kukuza uchumi, kuongeza ufanisi katika utoaji huduma za jamii, na hatimae kupunguza umasikini kwa wananchi wetu, na kuleta maisha bora kwa wote.

Mhe. Spika, katika siku chache tulizokuwa nazo au zilizopita kamati saba za baraza lako tukufu ziliwasilisha ripoti zake kwa baraza na kujadiliwa kwa kina. Nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuzijadili ripoti hizo katika hali ya uwazi na ukweli, maoni yao na maelekezo yao yameipa serikali changamoto kubwa ili iweze kuzifanya shughuli zake kwa ubora na ufanisi zaidi.

Napenda kuliahidi Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwa mapendekezo na maelekezo yote yaliyotolewa kwa serikali yatafanyiwa kazi ipasavyo na taarifa ya kuwasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu katika kikao kijacho.

Mhe. Spika, kwa kumalizia napeda kukushukuru tena wewe Mhe. Spika, kwa kuliongoza baraza letu kwa umahiri mkubwa, aidha, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa baraza hili kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonyesha katika kipindi chote cha majadiliano. Nawatakia kila la kheri na safari njema ya kurejea katika maeneo yenu ya kuishi na kuendelea na kazi zenu za kuwatumikia wananchi katika majimbo yenu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu haya, sasa naomba kutoa hoja ya kuliahirisha Baraza lako tukufu hadi tarehe 15 Juni, 2011 saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika, tunashukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba hiyo ya kufunga mkutano wetu huu, baada ya hotuba hiyo ya Makamo wa pili wa Rais waheshimiwa wajumbe sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 2.10 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 15/6/2011 Saa. 3.00 Asubuhi)